# Mukh’tasari Wa Maneno Katika Nguzo Za Uislamu

Kimetungwa Na:

Prof. Abdallah Bin Muhammad Bin Ahmad Al Twayyaar

# خلاصة الكلام

# في

# أركان الإسلام

تأليف

الأستاذ الدكتور

عبدالله بن محمد بن أحمد الطيار

## Bismi LLahi Rahman Rahiim

Utangulizi

Kila sifa kamilifu zinamstahiki Allah Mtukufu, tunamtukuza na tunamuomba msaada na tunatubia kwake, na tunajilinda kwake kutokana na shari za nafsi zetu na matendo yetu mabaya, yeyote aliyeongozwa na Allah hakuna wa kumpoteza, na aliyepotezwa na Allah hakuna wa kumpoteza, nashuhudia ya kwamba hakuna Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah peke yake hana mshirika, na ninashuhudia ya kwamba Mtume Muhammad rehma na amani ziwe juu yake ni mja wake na ni Mtume wake.

Amesema Allah Mtukufu: {**Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu kama ipasavyo kumcha; wala msife ila nanyi ni Waislamu**}. [Al Iraan: 102].

Na amesema Allah Mtukufu: {**Enyi watu! Mcheni Mola wenu Mlezi aliye kuumbeni kutokana na nafsi moja, na akamuumba mkewe kutoka nafsi ile ile.**

**Na akaeneza kutokana na wawili hao wanaume na wanawake wengi. Na tahadharini na Mwenyezi Mungu ambaye kwaye mnaombana, na jamaa zenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwaangalieni**}. [Nisaa: 1].

Na amesema Allah Mtukufu: {**Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu na semeni maneno ya sawasawa**. **Apate kukutengenezeeni vitendo vyenu na akusameheni madhambi yenu. Na anaye mt›ii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, bila ya shaka amefanikiwa mafanikio makubwa**}. [Ahzaab: 7071-].

Baada Ya Kusema Hayo:

Allah ameweka sheria ya kuabudiwa na akaifanya kuwa lengo la kuumbwa viumbe, amesema Allah Mtukufu: {**Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu Mimi**}. [Dhaariyaat: 56].

Na ulikuwa ndiyo wito wa kila Mtume kwa uma wake akiwaambia: {**Muabuduni Mwenyezi Mungu, na muepukeni Shetani**}. [Al Nahli: 36], {**Muabuduni Mwenyezi Mungu. Nyinyi hamna mungu ila Yeye**}. [Al A'araaf: 65].

Amesema Sheykhul Islaam Bin Teymiyah Allah amrehemu kuhusu maana hiyo: “Hakika dini ya kweli ni ambayo mja anamuabudu Allah kwa namna zote, na kufanya hivo ni kupata mapenzi ya Allah kwa daraja zote, na ibada ya mja inapo kamilika ndiyo ukamilifu wa mapenzi ya mja kwa Mola wake, na ndiyo sababu ya Allah kumpenda mja wake…mapenzi yoyote ambayo hayapo kwa ajili ya Allah ni batili, na ibada yoyote ambayo haikusudiwi kupata malipo kwa Allah basi ibada hiyo ni batili”.[1]

Ni watu wengi wanao zembea kuzifahamu nguzo za uislamu, na wanazifanyia kazi kimakosa, na ndio sababu tunaona makosa mengi katika ibada mama kama vile Swala, Zaka, Funga na Hijja, na umma unaombwa kurejea katika chemchem iliyokuwa safi, pamoja na kusoma historia zawema waliotangulia, ili kupata viigizo vya kweli kwa watu wote, na hamna kuokoka wala kufalu wala kupata nguvu isipokuwa kwa kumuabudu Allah kama alivyo elekeza, na ibada zote zinazo pingana na mwongozo wa Mtume rehma na amani ziwe juu yake ni batili na ni zenye kurejeshwa, na huu ndio wito wa Mtume rehma na am-

1_ “Al Ubuudiyyah” Uk. 41.

ani ziwe juu yake uliogonga masikio ya watu, pindi aliposema: (Yeyote mwenye kufanya (kuzusha) ibada ambayo haipo katika dini, basi atarejeshewa mwenyewe).[2]

Lakini watu wengi hawakuujibu wito huo, na wakapotosha maana halisi ya ibada, na hiyo ndiyo sababu iliyo pelekea kusahihisha maana ya ibada na kubainisha nguzo za uislamu kwa njia nyepesi na yenye kufahamika, na hasa kwa watu ambao hawajasoma, na vituo vya kiislamu (Jaaliyaat) ambavyo vinahitaji vitabu kama hivi vyepesi viliandikwa kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.

Na Chuo Kikuu cha Imamu Uversity ndicho cha kwanza kutoa mtiririko wa vitabu vya mfumo huo, na uongozi wa tafiti za kielimu katika Chuo hocho uliniamuru niandike kitabu ambacho kitakacho kusanya nguzo za kiislamu kwa nkia nyepesi na ya uwazi, ili kiwe ni msaada kwa wahitaji wasiojua baadhi ya hukumu zinazo ambatana na nguzo za uislamu, na kwa maagizo niliyo pewa nimeandaa kitabu hiki, na ninatarajia kuwa kitawanufaisha wengi, na ninamuomba Allah anipe manufaa kwa elimu yangu, na anielimishe kwa niyoyajua, na amlipe thawabu

2_ “Sahihi Muslim” (4493).

aliyenielekeza na kunisaidia na kunihamasisha, hakika Allah ndiye msimamizi wa hayo na ndiye muweza.

Rehma na amani ziwe juu ya Mtume wetu Muhammad na Ali za Maswahaba zake na watu wote.

Kimeandikwa Na:Abuu Muhammad

Abdallah Bin Muhammad Bin Ahmad Al Twayyaar

Kingdom Of Saudi Arabia

Al Zilfi, P.o.box 148 Code 11932.

Somo La Kwanza: Imani

Somo Hili Linakusanya Vipengele Vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | Maana Ya Imani. | 2 | Nguzo Za Imani. |
| 3 | Misingi Ya Imani. | 4 | Kumuamini Allah. |
| 5 | Maana Ya Kumuamini Allah | 6 | Yanayo Ambatana Na Kumuamini Allah. |
| 7 | Kuamini Uwepo Wa Allah Mtukufu. | 8 | Kuamini Uungu Wa Allah. |
| 9 | Kuamini Majina Ya Allah Na Sifa Zake. | 10 | Matunda Ya Kumuamini Allah. |
| 11 | Kuamini Malaika. | 12 | Maana Ya Kuamini Malaika. |
| 13 | Namna Ya Kuamini Malaika. | 14 | Matunda Ya Kuamini Malaika. |
| 15 | Kuamini Vitabu. | 16 | Yanayo Ambatana Na Kuamini Vitabu. |
| 17 | Matunda Ya Kuamini Vitabu. | 18 | Kuamini Mitume. |
| 19 | Maana Ya Kuamini Mitume. | 20 | Yanayo Ambatana na Kuamini Mitume. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 21 | Matunda Ya Kuamini Mtume. | 22 | Kuamini Siku Ya Mwisho. |
| 23 | Maana Ya Kuamini Siku Ya Mwisho. | 24 | Yanayo Ambatana Na Kuamini Siku Ya Mwisho. |
| 25 | Matunda Ya Kuamini Siku Ya Mwisho. | 26 | Kuamini Qadari. |
| 27 | Maana Ya Kuamini Qadari. | 28 | Yanayo Ambatana na Kuamini Qadari. |
| 29 | Matunda Ya Kuamini Qadari. | 30 | Kwanini Aqiida Inapewa Umuhimu? |
| 31 | Malengo Ya Itikadi Ya Kiislamu. | 32 | Kupenda Na Kuchukia Kwaajili Ya Allah |
| 33 | Umuhimu Wake Katika Itikadi Ya Uislam | 34 | Mifano Ya Kuwapenda Makafiri. |

Imani

**Maana Ya Imani:** Ni kusadikisha kwa moyo, na kutamka kwa ulimi, na kutenda kwa viungo.

Amesema Allah Mtukufu: {**Mabedui wamesema: Tumeamini. Sema: Hamjaamini, lakini semeni: Tumesilimu. Kwani Imani haijaingia katika nyoyo zenu**}. [Al Hujraat: 14].

Na amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Imani ni kumuamini Allah na Malaika wake na Vitabu vyake na Mitume wake na Siku ya mwisho, na kuamini Qadari za Allah, kheri zake na shari zake).[3]

Amesema Hassan Al Baswariy Allah amrehemu: "Imani siyo kutamani wala kujipamba, bali imani ni kitu kilicho tulia katika moyo na inasadikishwa kwa vitendo".

Imani na Uislamu vinapokutana sentesi, hutafsiriwa uislamu kwa maana ya matendo ya wazi, na imani kwa maana matendo moyo.

Na linapokuja neno moja uislamu katika sentesi, makusudio yake ni uislamu wote na imani ikiwemo.

3_ "Sahihi Bukhary" Vol. 1، Uk. 20. Na "Sahihi Muslim" Vol. 1، Uk. 30.

Vilevile linapokuja neno imani pekee katika sentesi, makusudio yake pia ni uislamu wote.

Misingi Ya Imani

Misingi ya imani ambayo ni wajibu kuiamini ni sita, ameitaja Allah katika Qur'an tukufu, vilevile ameitaja Mtume katika Sunna.

Amesema Allah Mtukufu: {**Sio wema kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa mashariki na magharibi. Bali wema ni wa anaye muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho na Malaika na Kitabu na Manabii**}. [Al Baqara: 177].

Aya hiyo imekusanya imani tano za uislamu nazo:

1- Kumuamini Allah.

2- Kuamini siku ya mwisho.

3- Kuamini Malaika.

4- Kuamini Vitabu.

5- Kuamini Mitume.

Imebaki imani ya kuamini Qadari, ameitaja Allah Mtukufu katika kauli yake: {**Kwa hakika Sisi tumekiumba kila kitu kwa kipimo**}. [Al Qamar: 49].

Ama hadithi zinazo zungumzia misingi hiyo ni nyingi, tutataja baadhi ya hizo, na hadithi hiyo ni nguzo katika kubainisha misingi ya imani, uislamu na ihsani, nayo ni hadithi ya Jibril, na katika hadithi alisema kumwambia Mtume: Nieleze kuhusu imani? Mtume rehma na amani ziwe juu yake akamjibu: (Imani ni kumuamini Allah na Malaika wake na Mitume wake na Vitabu vyake na kuamini Siku ya mwisho, na kuamini Qadari ya Allah kheri zake na shari zake).[4]

Hizo ndizo nguzo za imani sita ambazo tutazieleza kwa ufafanuzi zaidi.

1. Kumuamini Allah:

**Maana ya kumuamini Allah**: Ni kukiri na kukubali habari za Allah na kunyenyekea kwa kufuata sheria zake, na kuamini ya kwamba ulimwengu huu una Muumbaji ambaye yupo na ndiye Mola wa pekee katika Uungu wake

4_ "Sahihi Bukhary" Vol. 1، Uk. 15.

na ibada zake na majina yake na sifa zake.

Na kwa maana hiyo inatubainikia ya kwamba kumuamini Allah kunaambatana na mambo yafuatayo:

(A) Kuamini Uwepo Wa Allah Mtukufu:

Kuna mambo manne yanayo nonyesha juu ya uwepo wa Allah:

1. Akili. 2. Hisia.

3. Maumbile. 4. Sheria.

Ya Kwanza: Dalili za kiakili juu ya kuwepo kwa Allah:

Ulimwengu huu na vilivyomo kama vile Mbingu, Ardhi, Bahari, Binadamu na vinginevyo, vyote hivyo ni dalili za kiakili juu ya kuwepo kwa Allah Mtukufu, hakika viumbe vya mbinguni na ardhini lazima viwe na aliye viumba na ndiye anaye viendesha, haiwezekani kuwepo viumbe hivyo bila kuwepo aliye viweka, amesema Allah Mtukufu: {**Au wao wameumbwa pasipo kutokana na kitu chochote, au ni wao ndio waumbaji?Au wao wameziumba mbingu na ardhi? Bali hawana na yakini**}. [Al Twuur: 3536-].

Na kwa ajili hiyo Jubeyri bin Mutw'imu Allah amrid-

hie kabla hajasilimu aliposikia Aya hizo alisema: “Moyo wangu ulikaribia kuruka”,[5] alipatwa na hali hiyo pindi imani ilipoingia katika moyo wake, na mara nyingi Allah Mtukufu anawaelekeza waja wake kwa kuwapa dalili za kujua alama zake za wazi ambazo ni viumbe vyake vya mbinguni na ardhini, kama alivyosema Allah Mtukufu: {**Na katika ardhi zipo Ishara kwa wenye yakini**}. [Dhaariyaat: 20], na maana ya Aya hiyo ni kwamba: Tazameni ardhi na vilivyomo ni miongoni mwa alama zinazo onyesha ukubwa wa Allah na uwezo wake wa ajabu.

Ya Pili: Dalili Za Hisia Juu Ya Kuwepo Kwa Allah:

Hakika mwanadamu anamuomba Mola wake Mtukufu yale anayo yataka katika mambo ya kidunia kwa kusema: Ewe Mola wangu, kisha anaomba kile anacho kitaka, hakai muda mrefu isipokuwa anajibiwa alicho kiomba, na majibu hayo anayaona kwa macho yake, je! Hiyo siyo dalili ya kuonyesha juu ya kuwepo kwa Allah? Na jambo hilo liko wazi wanalikubali makafiri na wenye kukanusha juu ya uwepo wa Allah.

5_ “Sahihi Bukhary” Vol. 2، Uk. 206. Na “Sahihi Muslim” (463).

Na ni uzuri ulioje wa kisa hiki nilicho kisikia kwa mmoja wa walinganiaji, alisema: “Tulipokuwa safarini kuelekea mji fulani, katika safari hiyo tulikuwa tumepanda ndege, mara kukatokea jambo katika ndege na wasafiri wakahisi wanaanguka, nikachukua Mas’hafu yangu nikawa nausoma, akaja karibu yangu bwana mmoja ambae anaamini kuwa Allah hayupo, akaniambia kwa sauti ya juu: Zidisha kusoma Qur’an, akasimama karibu yangu huku akiendelea kusema: Endelea kusoma na zidisha sauti huenda Allah akatuokoa, ninamshukuru Allah kwahakika tulinusurika kutokana na jambo hilo la hatari”.

Hakuna jambo hilo halishangazi kwani limesha fanywa na washirikina wengi kabla yake, na Allah amewazungumzia washirikina hao kwa kusema: {**Na wanapo panda katika marikebu, humwomba Mwenyezi Mungu kwa kumsafia ut›iifu. Lakini anapo wavua wakafika nchi kavu, mara wanamshirikisha**}. [Al A’nkabuut: 65].

Hizo ni dalili za hisia zinazo onyesha juu ya uwepo wa Allah Mtukufu.

Ya Tatu: Dalili Za Kimaumbile Juu Ya Kuwepo Kwa Allah

Kwa hakika watu wengi ambao fikra zao za kiitikadi hazija badilika wanaamini kuwa Allah yupo, na mpaka wanyama wasioweza kuongea wanaamini ya kwamba Allah yupo, maumbile yamelazimishwa kumjua Allah na kumpwekesha, amesema Allah Mtukufu: {**Na pale Mola wako Mlezi alipo waleta katika wanaadamu kutoka migongoni mwao kizazi chao, na akawashuhudisha juu ya nafsi zao, akawaambia: Je, Mimi si Mola Mlezi wenu? Wakasema: Kwani! Tumeshuhudia. Msije mkasema Siku ya Kiyama sisi tulikuwa tumeghafilika na hayo. Au mkasema: Hakika baba zetu ndio walio shirikisha kabla yetu, na sisi ni dhuriya zao tu baada yao. Basi utatuangamiza kwa sababu ya waliyo yafanya wapotovu?**}. [Al A’araaf: 172173-].

Aya hizo zinaonyesha ya kwamba maumbile ya mwanadamu yamelazimishwa kushuhudia juu ya kuwepo kwa Allah Mtukufu.

Ya Nne: Dalili Za Kisheria Juu Ya Kuwepo Kwa Allah

Mitume wamekuja na sheria mbalimbali za Allah zilizo kusanya mambo mbalimbali yenye maslahi kwa viumbe, na hiyo inaonyesha ya kwamba aliyewatuma ni Allah Mola wa viumbe vyote, na hasa Qur'an hii tukufu ambayo wanadamu na majini wameshindwa kuleta mfano wake.

Na miongoni mwa mambo yanayo onyesha juu ya kuwepo kwa Allah ni wanyama, majabali, mito, bahari na tofauti ya lugha wanazo ongea wanadamu na rangi zao, vilevile utofauti wa akili zao na ufahamu na harakati zao, pamoja na wema na uovu, na namna alivyo Allah alivyopangilia viungo vyao na kuviweka mahala panapo stahiki, na kwasababu hiyo Allah Mtukufu amesema: {**Na pia katika nafsi zenu - Je! Hamwoni?**}. [Dhaariyaat: 21].

Ni uzuri ulioje wa majibu ya bedui (Mwarabu wa mashambani) alipoulizwa kuhusu uwepo wa Allah Mtukufu, alijibu kwa kusema: "Utakasifu ni wa Allah Mtukufu, hakika kinga za kwato ni kwamba kuna ngamia, na athari za nyayo zinaonyesha kuwa kuna aliyepita, na mbingu zenye nyota na ardhi yenye njia nyingi, na bahari yenye mawimbi, yote hayo ni alama za uwepo wa Allah Mtukufu".

(B) Kumuamini Allah Kuna Ambatana Na Kuamini Uungu wake:

Na maana ya maneno hayo: Ni kuamini katika moyo wako pamoja na kukiri kwa ulimi wako ya kwamba Allah ni mmoja na Yeye ndiye Mola wa haki, hana mshirika katika Uungu wake, na vyote vinavyo abudiwa kinye na Yeye ni batili, amesema Allah Mtukufu: {**Hayo ni kwa kuwa Mwenyezi Mungu ndiye Wa Kweli, na kwamba wale wanao waomba badala yake, ni baat›ili, na hakika Mwenyezi Mungu ndiye Aliye Juu na ndiye Mkubwa**}. [Al Hajj: 62].

Na kuamini Uungu wa Allah kunampelekea mtu kuto kukifanyia ibada kitu chochote isipokuwa Allah, Yeye ndiye Mola wa kweli anayestahiki kuabudiwa, mja haruhusiwi kufanya ibada za kiroho wala ibada za maneno au za vitendo isipokuwa kumfanyia Allah peke yake, amesema Allah Mtukufu: {**Enyi watu! Muabuduni Mola wenu Mlezi aliye kuumbeni nyinyi na wale wa kabla yenu, ili mpate kuokoka**}. [Al Baqara: 21].

Na amesema Allah Mtukufu: {**Muabuduni Mwenyezi Mungu wala msimshirikishe na chochote**}. [Nisaa: 36].

Na amesema Allah Mtukufu: {**Na Mola wako Mlezi ameamrisha kuwa msimuabudu yeyote ila Yeye tu**}. [Al Israa: 23].

Na amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Amesema Allah Mtukufu: Mimi ninajitosha sihitajii mshirika, yeyote mwenye kunishirikisha na kitu kingine, nitamuacha na ushirikina wake).[6]

Jambo la wajibu juu ya mja ni kwamba chochote kisichokuwa Allah basi asikifanyie ibada, na akifanya hivo atakuwa amefanya shirki, na miongoni m,wa ibada hizo nikama vile, nadhiri, kuchinja, kuomba dua, kuomba nusra, kuomba msaada, kijidhalilisha, kunyenyekea, kuogopa, kutegemea, kuswali, kuhiji, kutoa zaka na mfano wa hizo.

(C) Kumuamini Allah Kuna Ambatana Na Kuamini Majina Yake Na Sifa Zake:

---

6- "Sahihi Muslim" (2294).

Na maana ya kuamini majina ya Allah na sifa zake: Ni kuthibitisha yale aliyo yathibitisha Allah mwenyewe katika Kitabu chake, au aliyo yathibitisha Mtume rehma namani ziwe juu yake, miongoni mwa majina na sifa kwa namna inayo stahiki, bila kubadilisha wala kugeuza wala kufananisha wala.

Amesema Allah Mtukufu: {**Na Mwenyezi Mungu ana majina mazuri kabisa, basi muombeni kwa hayo**}. [Al A'araaf: 180].

Na ni wajibu kwa mja ahisi ukubwa wa majina na sifa hizo, na amuabudu Allah kupitia majina hayo, hakika kuamini majina hayo kunamfanya mja awe na mapenzi, khofu na matarajio kwa Mola wake anaye muabudu.

Matunda Ya Kumuamini Allah Mtukufu

Kumuamini Allah Mtukufu kuna matunda makubwa, na miongoni mwa hayo:

1- Ni kuwa na tauhidi ya kweli na kumuabudu Allah peke yake.

2- Ni ukamilifu wa mapenzi ya Allah Mtukufu na kumtukuza kama yalivyo majina yake mazuri na sifa zake za juu.

3- Ni ukweli wa kumuabudu Allah kwa kufanya aliyo yaamrisha na kujiepusha na yale aliyo yakataza.

4- Ni kumkomboa mja kutokana na utumwa wa viumbe, na kumzuia asiwaogope wala kuwatarajia wala kufanya ibada kwa ajili yao, kwasababu kutokufanya hayo ndiyo ushindi wa kweli.

2- Kuamini Malaika

**Malaika ni viumbe gani?**: Malaika ni viumbe wanaoishi katika ulimwengu usio onekana, Allah aliwaumba kutokana na nuru na akawafanya ni wenye kumtii na wenye kujidhalilisha kwake, na kila mmoja ana kazi aliyopewa na Allah.

Jibril amepewa kazi ya kufikisha Wahyi kwa Mitume, na Israafiil amepewa kazi ya kupuliza Baragumu, naye ni katika Malaika walioibeba Arshi ya Allah tukufu, na Mikail amepewa kazi ya mvua na mimea, na kuna Malaika wamepewa kazi ya kutoa roho za watu na kiumbe chochote

chenye roho, naye ni Malakul Mauti na wasaidizi wake, na wengineo miongoni mwa Malaika ambao kazi zao zinajulikana.

Vipi Utawaamini Malaika?

1. Utawaamini ya kwamba wao ni viumbe wanaoishi katika ulimwengu usio onekana, hawaonekani, lakini wanaweza kuonekana, nao wameumbwa kutokana na nuru, ni wanyenyekevu kwa Allah ukweli wa kunyenyekea, amesema Allah Mtukufu: {**Hawamuasi Mwenyezi Mungu kwa anayo waamrisha, na wanatenda wanayo amrishwa**}. [Tahriim: 6].

2. Tunaamini majina ya Malaika tuliyo elezwa, na tunaamini ya kwamba wamepewa kwazi na Allah.

Matunda Ya Kuamini Malaika

1. Ni kujua ukubwa wa Allah na nguvu zake na utawala wake.

2. Kumshukuru Allah kutokana na ulinzi wake kwa wanadamu, kwasababu amewawakilisha Malaika wamlinde mwanadamu.

3. Malaika wanapenda ibada wanazofanya.[7]

3- Kuamini Vitabu

**Maana ya kuamni Vitabu:** Ni kusadikisha ya kwamba Vitabu vyote vimeteremshwa kutoka kwa Allah kwenda kwa waja wake kwa haki na uwazi na uongofu, na kuamini ya kwamba Vitabu hivyo ni maneno ya Allah Mtukufu na wala siyo maneno ya mwengine.

Kuamini Vitabu vya Allah kuna ambatana na mambo yafuatayo:

1. Kuamini ya kwamba Vitabu hivyo vimeteremshwa kutoka kwa Allah.

2. Kuamini Vitabu tunavyo vijua majina yake kama vile Qur'an aliyo teremshiwa Mtume Muhammad rehma na amani ziwe juu yake, na Tauraat aliyo teremshiwa Nabii Mussa amani iwe juu yake, na Injili aliyo teremshiwa Nabii Issa amani iwe juu yake, na Zaburi aliyo teremshiwa Nabii Daud amani iwe juu yake, na Vitabu tusivyo vijua majina yake tunaviamini kwa ujumla.

---

7- "Muhadhwaraati Fil Aqiidah Wa Addaawah" cha Shekh Swaleh Fauzan، Vol. 1، Uk. 281.

3. Ni kusadikisha yale yaliyoelezwa ndani ya Vitabu hivyo, kama vile habari za Qur'an na habari za Vitabu ambavyo havija badilishwa wala kupotoshwa katika Vitabu vilivyo tangulia.

4. Kuzifanyia kazi hukumu ambazo hazijafutwa, na kuridhia pamoja na kusalimu amri.

5. Vitabu vyote vilivyo tangulia vimefutwa na Qur'an tukufu.

Amesema Allah Mtukufu: {**Na tumekuteremshia wewe, kwa haki, Kitabu hichi kinacho sadikisha yaliyo kuwa kabla yake katika Vitabu na kuyalinda**}. [Maaida: 48], haifai kuifanyia kazi hukumu yoyote miongoni mwa hukumu zilizokuja katika Vitabu vilivyo tangulia, isipokuwa hukumu iliyo afikiana na hukumu ya Qur'an.

Matunda Ya Kuamini Vitabu

1. Ni kujua ulinzi wa Allah kwa viumbe wake, kwasababu aliteremsha kwa kila umma Vitabu vinavyo waongoza.

2. Ni kujua hekima ya Allah pindi kwa kuwapa kila watu sheria ninayo endana nao.

Amesema Allah Mtukufu: {**Kila mmoja katika nyinyi tumemwekea sharia yake na njia yake**}. [Maaida: 48].

3. Ni kushukuru neema za Allah kwa kuteremshwa Vitabu.

4- Kuamini Mitume

**Mitume ni akina nani?:** Mitume ni watu ambao Allah aliwachagua wawe wawakilishi baina ya Allah na waja wake ili wawafikishie sheria yake nay ale yanayo wapasa kufanya kwa ajili ya Allah, na mwengineyo katika mambo aliyo wafunulia Allah, na Mtume wa mwanzo ni Nabii Nuuh amani iwe juu yake, na wa mwisho ni Mtume Muhammad rehma na amani ziwe juu yake.

Amesema Allah Mtukufu: {**Muhammad si baba wa yeyote katika wanaume wenu, bali ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na Mwisho wa Manabii**}. [Ahzaab: 40].

Mitume ni viumbe walio umbwa, hawana sifa za Uungu wala hawatakiwi kuabudiwa, haifai kuwaomba nusra, wala kuwafanyia nadhiri, wala kuchinja kwa ajili yao, na mengineyo mfano wa hayo haifai kumfanyia yeyote

katika Mitume isipokuwa Allah peke yake.

Amesema Allah Mtukufu: {**Sema: Siimilikii nafsi yangu manufaa wala madhara, ila apendavyo Mwenyezi Mungu. Na lau kuwa ninayajua ya ghaibu ninge jizidishia mema mengi, wala ovu lisinge nigusa. Mimi si chochote ila ni mwonyaji na mbashiri kwa watu wanao amini**}. [Al A'araaf: 188].

Kuamini Mitume Kuna Ambatana Na Mambo Yafuatayo:

1. Kuamini ya kwamba Utume wao ni wa kweli, na kuamini kuwa wametumwa na Allah, yeyote mwenye kuukanusha Ujumbe wa yeyote katika wao atakuwa amewakufuru Mitume wote, Manaswara waliomkadhibisha Muhammad rehma na amani ziwe juu yake, na wakakataa kumfuata, kwa kitendo hicho wamemkadhibisha pia Nabii Issa bin Maria amani iwe juu yake na kukataa kumfuata, kwasababu Nabii Issa aliwabashiria juu ya ujio wa Mtume Muhammad rehma na amani ziwe juu yake.

2. Kuamini Mitume tunaowajua kwa majina kama vile Muhammad, Ibrahim, Issa, Mussa, Nuuh na wengineo

miongoni mwa walitajwa katika Qur'an, na Mitume ambao hawaja tajwa kwa majina tunawaamini kwa ujumla.

3. Kusadikisha yote waliyo kuja nayo kutoka kwa Mola wao.

4. Kuifanyia kazi sheria ya Mtume Muhammad rehma na amani ziwe juu yake, kwasababu yeye ndiye Mtume wa mwisho.

Matunda Ya Kuamini Mitume:

1. Ni kujua rehma za Allah na msaada wake kwa waja wake, kwasababu aliwatumia Mitume ili wawaongoze katika njia iliyo nyooka, na wawabainishie namna ya kumuabudu Allah.

2. Ni kumshukuru Allah kwa neema ya Mitume.

3. Ni kuwapenda Mitume na kuwatakia rehma na kuwatukuza pamoja na kuwasifu.

5- Kuamini Siku Ya Mwisho

**Makusudio ya siku ya mwisho:** Ni siku ya Qiyama ambayo Allah atawafufua waja wake kwa ajili ya hesabu

na malipo, na imeitwa siku ya mwisho, kwasababu ni siku ambayo hamna siku nyingine baada yake, watu wa Peponi watakuwa Peponi, na wa Motoni watakuwa Motoni.

Amesema Allah Mtukufu: {**Bali wema ni wa anaye muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho**}. [Al Baqara: 177], na amesema Allah Mtukufu: {**Na ambao wanayaamini yaliyo teremshwa kwako, na yaliyo teremshwa kabla yako; na Akhera wana yakini nayo**}. [AL Baqara: 4].

Hiyo ni nguzo ya tano katika nguzo za imani, yeyote mwenye kuzikadhibisha ni kafiri, amesema Allah Mtukufu: {**Walio kufuru wanadai kuwa hawatafufuliwa. Sema: Kwani? Naapa kwa Mola wangu Mlezi! Hapana shaka mtafufuliwa, na kisha hapana shaka mtaambiwa mliyo yatenda. Na hayo ni mepesi kwa Mwenyezi Mungu**}. [Taghaabun: 7].

Kuamini Siku Ya Mwisho Kuna Ambatana Na Mambo Yafuatayo:

1. Kuamini ya kwamba waja watahesabiwa na watalipwa, kwasababu Allah Mtukufu atawahesabu waja

kutokana na matendo yao, na kila mmoja atalipwa juu ya kile alicho kifanya, amesema Allah Mtukufu: {**Hakika ni kwetu Sisi ndio marejeo yao**. **Kisha hakika ni juu yetu Sisi hisabu yao!}.** [Al Ghaashiyah: 2526-].

2. Kuamini ya kuwa Pepo na Mota vipo, na kwamba katika Pepo na Moto ndiyo kwenye maisha ya milele, Allah ameiandaa Pepo kwa ajili ya watu wenye matendo mema miongoni mwa waumini wasemao kweli na wenye ikhlas, na Moto Allah ameuandaa kwa ajili ya watu wenye kufanya maasi miongoni mwa makafiri na wanafiki, amesema Allah akiizungumzia Pepo: {**Hakika walio amini na wakatenda mema, hao ndio bora wa viumbe**. M**alipo yao kwa Mola wao Mlezi ni Bustani za daima, zipitazo mito kati yake. Wakae humo milele. Mwenyezi Mungu yu radhi nao, na wao waradhi naye. Hayo ni kwa anaye mwogopa Mola wake Mlezi**}. [Al Bayyinah: 78-].

Na amesma Allah akiuzungumzia Moto: {**Na uogopeni Moto ambao umeandaliwa kwa ajili ya makafiri**}. [Al Imraan: 131].

Na amesema Allah Mtukufu: {**Hakika Mwenyezi Mungu amewalaani makafiri na amewaandalia Moto unao waka kwa nguvu**. **Watadumu humo milele. Hawampati mlinzi wala wa kuwanusuru**}. [Ahzaab: 6465-].

Kuamini Siku Ya Mwisho Kuna Ambatana Na Kuamini yote yanayokuwa baada ya kufa, kama vile:

**(a) Fitina za kaburi:** Inakusudiwa maswali anayo ulizwa maiti baada ya kuzikwa, maiti kaburini anaulizwa: Nani Mola wako? Ni ipi Dini yako? Nani Mtume wako?. Kama ni muumini anajibu kwa kusema: Mola wangu ni Allah! Dini yangu ni Uislamu! Na Mtume wangu ni Muhammad rehma na amani ziwe juu yake, na kama ni kafiri atasema: Ha..ha sijui.

**(b) Adhabu za kaburi na neema zake:** Watu wenye imani wata neemeshwa katika makaburi yao, na makaburi yatapanuliwa kiasi cha upeo wa macho, na kila mmoja ataona mafikio yake Peponi, ama makafiri na wanafiki na madhalimu wataadhibiwa katika makaburi yao, watabanwa na makaburi na utawashwa moto ndani yake,

na kila mmoja ataona mafikio yake Motoni, tunamuomba Allah atukinge na adhabu za kaburi.

Matunda Ya Kuamini Siku Ya Mwisho

1. Ni kuwahimiza watu juu kufanya twaa na kuwafanya wajutie kwa kupitwa na ibada.

2. Kuwatisha wanaofanya maasi na kuwaogopesha.

3. Kuwaliwaza waumini kutokana na mambo ya kidunia wanayo yakosa, na kwamba Akhera watapata neema nyingi.

6- Kuamini Qadari

**Maana ya uamini Qadar:** Hiyo ni nguzo ya sita miongoni mwa nguzo za imani, na maana ya kuamini Qadari: Ni kuamini ya kwamba Allah alipangilia vitu vyote toka zamani na akajua kwamba vitatokea katika wakati na sehemu maaalum aliyopanga Allah, na vitu vyote vinatokea kama alivyo panga Allah.

**Kuamini Qadari Kuna Ambatana Na Mambom Yafuatayo**:[8]

8_ "Sharhu Uswuulil Imaani" cha Shekh Muhamma bin Swaleh Al Utheymiin (Risaala Ndogo).

1. Kuamni ya kwa Allah ni mjuzi wa kila kitu kwa zama zote, anayajua yaliyo kuwa na yatakayo kuwa, na anajua yale ambayo hayajatokea lau yangelitokea anajua yangekuwaje.

2. Kuamini ya kwamba Allah aliandika kila kitu katika ubao wenye kuhifadhi vitu vyote (Lauhul Mahfuudhi), amesema Allah Mtukufu: {**Je! Hujui kwamba Mwenyezi Mungu anayajua yaliomo mbinguni na katika ardhi? Hakika hayo yamo Kitabuni. Hakika hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi**}. [Al Hajj: 70].

Na katika Sahihi Muslim, Mtume rehma na amani ziwe juu yake anasema: (Allah Mtukufu aliandika makadirio yote ya viumbe kabla hajaumba mbingu na ardhi kwa muda wa miaka elfu khamsini).[9]

3. Kuamini ya kwamba viumbe wote wapo kwa utashi wa Allah, amesema Allah Mtukufu: {**Na Mola wako Mlezi huumba na huteuwa atakavyo**}. [Al Qaswas: 68].

Na amesema Allah Mtukufu: {**Yeye ndiye anaye kuundeni ndani ya matumbo ya wazazi kwa namna apendayo**}. [Al Imraan: 6].

9- "Mukh'tasari Sahihi Muslim" Uk. 486, (1841).

4. Kuamini ya kwamba vitu vyote vimeumbwa na Allah Mtukufu, na kila kinacho patikana mbinguni na ardhini amekiumba Yeye, na amekiumbia pia harakati zake, hakuna Mola wala Muumbaji isipokuwa Yeye.

Amesema Allah Mtukufu: {**Mwenyezi Mungu ndiye Muumba wa kila kitu, na Yeye ndiye Mlinzi juu ya kila kitu**}. [Zumar: 62].

Na amesema Allah Mtukufu: {**Na hali Mwenyezi Mungu ndiye aliye kuumbeni nyinyi na hivyo mnavyo vifanya!**}. [Swaaffaat: 96].

Matuna Ya Kuamini Qadari:

1. Ni kumtegemea Allah Mtukufu katika kufanya asbaabu ili binadamu asitegemee sababu pekee, bali amtegemee Allah kasababu kila kitu kinaenda kwa kudra zake.

2. Mja asishangazwe na kile alichopata katika matarajio yake, kwasababu kupata kwake ni neema kutoka kwa Allah kutokana na yale aliyo mpangia miongoni mwa mambo ya kheri na mafanikio.

3. Ni kupata utulivu na raha katika nafsi kutokana na yale yanayo mtokea miongoni mwa kudra za Allah, mja asipate dhiki kwa kupitwa na kile anachopenda na kupatwa na jambo asilopenda, kwasababu yote yanatokea kwa uwezo wa Allah.

Umuhimu Wa Itikadi Sahihi

Kutilia Umuhimu Itikadi Sahihi

Katika maelezo yaliyo tangulia imetubainikia ya kwamba nguzo ya msingi ambayo mwanadamu anajengea matendo yake ni itikadi sahihi, kwani bila ya itikadi sahihi watu wanaingia katika giza la ushirikina na matamanio ya dunia, itikadi sahihi ndiyo mashine inayo ongoza maisha ya binadamu, kwasababu bila ya itikadi sahihi watu wanakuwa kama wanyama, anasema Allah Mtukufu akiwazungumzia watu waliokosa itikadi sahihi: {**Au wewe unadhani kwamba wengi wao wanasikia au wanaelewa? Hao hawakuwa ila ni kama nyama hoa tu, bali wao wamepotea zaidi njia**}. [Al Furqaan: 44].

Watu wanaihitajia zaidi itikadi sahihi kuliko wanavyo hitajia kula na kunywa, ndio maana ikawa hakuna budi

watu kuitilia umuhimu.

Malengo Ya Itikadi Sahihi Ya Kiislamu

1. Ni kuwa na ikhlas na kufanya ibada zote kwa ajili ya Allah, kwasababu Yeye ndiye Muumbaji na hana mshirika, ikawa ni wajibu ibada zote ziwe kwa ajili yake.

2. Ni kuzikomboz akili na fikra kutokana na fujo za wasiokuwa na itikadi sahihi, kwasababu asiyekuwa na itikadi sahihi moyo wake unakuwa wazi na anakuwa anaabudu kisichokuwa Allah, na hiyo ni sababu ya kuingia katika itikadi potofu.

3. Ni kuwa na raha ya fikra na mawazo, kwasababu itikadi sahihi inamfikisha mja kwa Mola wake.

4. Ni usalama wa niya na matendo, kwani mwenye itikadi sahihi haendi kinyume na Allah, kwasababu Mitume wameibainisha itikadi sahihi, na kufuata Mitume ni nguzo miongoni mwa nguzo za dini, atakaepotea katika kufuata Mitume atakuwa amepotea katika itikadi sahihi.

5. Ni kuwa na bidii na kutilia mkazo katika kufanya mambo, kwasababu mja kila anapopata fursa ya kufanya

ibada anatakiwa aifanye kwa haraka, na anapona sehemu yenye madhambi anatakiwa kujiepusha.

6. Ni kujenge umma wenye nguvu utakaotoa kila wanacho kimiliki katika kuithibitisha dini, na hawatajali hasara watakayo ipata katika njia ya Allah.

7. Ni kupata mafanikio ya duniani na Akhera, na kuitengeneza jamii pamoja na kujipatia thawabu.

Namuomba Allah Mtukufu aihakikishe itikadi sahihi kwa watu wote. Ameen.

Kupenda Na Kuchukia Kwa Ajili Ya Allah

Umuhimu wa kupenda na kuchukia kwa ajili ya Allah katika itikadi ya Uislamu:

Miongoni mwa misingi ya itikadi ya kiislamu ni kumpenda kila muislamu anayefuata itikadi hiyo, na kumfanyia uadui kila mwenye kuipiga vita itikadi hiyo, muislamu anatakiwa kuwapenda watu wa tauhidi, na awachukie washirikina na kuwafanyia uadui, na hiyo ndiyo dini ya Nabii Ibrahim amani iwe juu yake na walio muamini.

Amesema Allah Mtukufu: {**Hakika nyinyi mna mfano mzuri kwenu kwa Ibrahim na wale walio kuwa pamoja naye, walipo waambia watu wao: Hakika sisi tumejitenga nanyi na hayo mnayo yaabudu badala ya Mwenyezi Mungu. Tunakukataeni; na umekwisha dhihiri uadui na chuki baina yetu na nyinyi mpaka mtakapo muamini Mwenyezi Mungu peke yake**}. [Al Mumtahinah: 4].

Na amesema Allah Mtukufu: {**Enyi mlio amini! Msiwafanye Mayahudi na Wakristo kuwa ni marafiki. Wao ni marafiki wao kwa wao. Na miongoni mwenu mwenye kufanya urafiki nao, basi huyo ni katika wao. Hakika Mwenyezi Mungu hawaongoi watu wenye kudhulumu**}. [Al Maaida: 51].

Kupenda na kuchukia kwa ajili ya Allah ni msingi mkubwa miongoni mwa misingi ya dini, na katika mambo yenye kusikitisha zaidi ni kwamba watu wengi hawaujui msingi huu, ni mara ngapi unasikia watu wakihamasishana kuwa na ushirikiano katika dini, na wanasema kwamba wakristo ni ndugu zetu, bali wanadai ya kwamba mayahudi ni ndugu zetu, madai kama hayo yanamfanya mtu aritadi

na kutoka katika uislamu, amesema Allah Mtukufu: {**Bila ya shaka Dini mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu**}. [Al Imraan: 19].

Allah Mtukufu amewaharamishia waumini kuwapenda makafiri hata kama ni ndugu wa karibu au ndugu wa damu, amesema Allah Mtukufu: {**Enyi mlio amini! Msiwafanye baba zenu na ndugu zenu kuwa vipenzi vyenu ikiwa wanastahabu ukafiri kuliko Imani. Na katika nyinyi atakaye wafanya hao ndio vipenzi vyake, basi hao ndio madhaalimu**}. [Tauba: 23].

Kama Allah alivyo waharamishia waumini juu ya kuwapenda makafiri ambao ni maadui wa itikadi ya kiislamu, vilevile amelazimisha kuwapenda waumini, amesema Allah Mtukufu: {**Hakika rafiki yenu mlinzi ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na walio amini, ambao hushika Sala na hutoa Zaka nao wananyenyekea**. **Na atakaye fanya urafiki na Mwenyezi Mungu na Mtume wake na walio amini, basi hakika kundi la Mwenyezi Mungu ndilo lenye kushinda**}. [Al maaida: 5556-].

Mifano Ya Kuwapenda Makafiri:

1. Kujifananisha nao katika maongezi na mavazi, ni haramu kujifananisha na makafiri katika mambo yao, na miongoni ada zao na ibada zao: Kunyoa ndevu, kuvaa nguo ndefu iliyopita kongo mbili za miguu kwa wanaume, kujifananisha nao katika mavazi, kula na kunywa, na kuongea lugha yao isipokuwa kwa dharura.

2. Kuishi katika miji yao na kutohamia katika miji ya waislamu kwa ajili ya dini.

3. Kwenda katika miji yao kwa ajili ya utalii na matembezi.

4. Kuwasaidia na kuwanusuru dhidi ya waislamu.

5. Kuwatumia na kuwaamini na kuwapa vyeo ambavyo ndani yake kuna siri za waislamu, kuwapenda pamoja na kuwafanya ni washauri.

6. Kutumia tarehe zao na hasa tarehe zinazo ashiria sikukuu zao, kama vile tarehe za kizungu na kuacha kutumia tarehe za kiislamu.

7. Kushirikiana nao katika sikukuu zao na kuwasaidia

katika kuziandaa, au kuwapongeza na kuhudhuria.

8. Kujiita kwa majina yao na kuachana na majina ya kiislamu.

9. Kuwaombea msamaha wanapokufa pamoja na kuwatakia rehma, kwasababu hilo lina maana ya kuwapenda na kuifanya itikadi yao kuwa ni sahihi.[10]

Somo La Pili: Shirki Na Vigawanyo Vyake

Somo Hili Linakusanya Vipengele Vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | Maana Ya Shirki. | 2 | Vigawanyo Vya Shirki. |
| 3 | Shirki Kubwa. | 4 | Maana Ya Shirki Kubwa. |
| 5 | Uhatari Wa Shirki Kubwa. | 6 | Shirki Katika Ibada. |
| 7 | Shirki Katika Mapenzi. | 8 | Shirki Katika Matamanio |

10- "Muhaadhwaraat Fil Aqiidah" cha Shekh Swaleh Al Fauzaan, Vol. 2, Uk. 291.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 9 | Shirki Katika Kutii. | 10 | Shirki Ndogo. |
| 11 | Maana Ya Shirki Ndogo. | 12 | Aina Za Shirki Ndogo. |
| 13 | Uhatari Wa Shirki Ndogo. | 14 | Aina Za Shirki Ndogo. |
| 15 | Shirki Ndogo Ya Wazi. | 16 | Shirki Ndogo Iliyo Jificha. |
| 17 | Tofauti Kati Ya Shirki Kubwa Na Ndogo. | 18 | Kuyazuru Makaburi. |
| 19 | Kwanini Ni Sheria Kuyazuru Maburi. | 20 | Vigawanyo Vya Kuyazuru Makaburi. |
| 21 | Kuzuru Makaburi Kuliko Ruhusiwa Na Adabu Zake. | 22 | Kuzuru Makaburi Ambako Ni Bidaa. |
| 23 | Kuzuru Makaburi Ambako Ni Shirki. | 24 | Unafki Na Vigawanyo Vyake. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 25 | Maana Ya Unafki. | 26 | Aina Za Unafki. |
| 27 | Vigawanyo Vya Unafki. | 28 | Unafki Mkubwa. |
| 29 | Aina Za Unafki Mkubwa. | 30 | Unafki Mdogo. |
| 31 | Aina Za Unafki Mdogo. | 32 | Uchawi Na Viini Macho. |
| 33 | Ukweli Kuhusu Uchawi. | 34 | Je! Uchawi Unaathiri? |
| 35 | Madhara Ya Uchawi Katika Jamii | 36 | Mifano Hukumu Uchawi Na Wachawi. |
| 37 | Namna Ya Kijikinga Na Uchawi. | | |

Shirki Na Vigawanyo Vyake

**Maana ya shirki:** Ni kumfanyia Allah mshirika wakati ndiye aliye kuumba.

Na shirki imegawanyika sehem kuu mbili:

1- Shirki Kubwa

**Maana ya shirki kubwa:** Ni kumfanya Allah kuwa ana mshirika katika Uungu wake na ibada zake na majina yake na sifa zake.[11]

Na maana nyingine ya shirki: Ni mtu kujifanyia mungu kinyume na Allah ikawa anamuomba kama anavyo muomba Allah , na anamuogopa kama anavyo muogopa Allah, na anamtaraji na kumpenda kama anavyo mpenda Allah.[12]

Na kumfanya Allah kuwa ana mshirika katika Uungu wake, ni kama vile kuamini ya kwamba mshirika huyo anaweza kuumba, kutoa rizki, kuhuisha, kufisha na mfano wa hayo miongoni mwa sifa za Uungu.

11_ "Maarijul Qubuuli" Vol. 2، Uk. 483. Na "Allajnatu Daaimah" Vol. 1، Uk. 516.
12_ "Al Qaulu Sadiidi Fiy Sharhi Kitaabu Tauhiidi" cha Ibn Saad، Uk. 24.

Ama kumfanya Allah kuwa ana mshirika katika ibada, ni kama vile mja kumuabudu mshirika huyo kinyume na Allah, akarukuu na kusujudu na kuchinja na kufanya nadhiri pamoja na kumuomba kinyume na Allah.

Na kumfanya Allah kuwa ana mshirika katika majina yake na sifa zake, ni kama vile kuamini majina ya Laata, Uzza, Uzeyri na Yesu kuwa ni katika majina ya Allah, huo ni ushirikina katika majina, ama ushirikina katika sifa, ni kumfananisha Allah na kiumbe.

Shirki Kubwa Na Hatari Zake

Allah Mtukufu hamsamehe mwenye kufanya shirki kubwa isipokuwa akifanya toba, na mwenye kufanya shirki hiyo akifa bila ya kutubia ataishi Motoni milele.

Amesema Allah Mtukufu: {**Hakika Mwenyezi Mungu hasamehe kushirikishwa, na husamehe yaliyo duni ya hilo kwa amtakaye. Na anaye mshirikisha Mwenyezi Mungu basi hakika amezua dhambi kubwa**}. [Nisaa: 48].

Na mara nyingi wanaoingia katika shirki kubwa ni wale walio puuzia misingi ya dini, na kupuuzia kujifunza tauhidi pamoja na kutoifanyia kazi, na kuzembea kujifunza mambo yanayo haribu uislamu.

Shirki Kubwa Na Aina Zake

**1. Shirki Ya Ibada:** Nayo ni kumfanyia ibada asiyekuwa Allah, kama vile dua, nadhiri, kuchinja na mfano wa hizo miongoni mwa ibada.

**2. Shirki Katika Mapenzi:** Nayo ni mtu kuwa miungu kinyume na Allah, akawa anawapenda miungu hao kama anavyo mpenda Allah, amesema Allah Mtukufu: {**Na katika watu wapo wanao chukua waungu wasio kuwa Mwenyezi Mungu. Wanawapenda kama kumpenda Mwenyezi Mungu**}. [Al Baqara: 165].

**3. Shirki Katika Matamanio:** Nayo ni mtu kutanguliza matamanio yake kuliko kumtii Allah, ikiwa matamanio hayo ni katika shirki na ukafiri, basi hiyo ni kufuru na inamtoa mtu katika uislamu, na matamanio hayo ni katika maasi, hiyo inakuwa ni katika aina za ushirikina, kwasababu ameyashirikisha matamanio yake pamoja na

Allah, na aina hiyo haimtoi mtu katika uislamu isipokuwa maasi yote hayawi ila kwa kufuata matamanio, amesema Allah Mtukufu: {**Je! Umemwona aliye yafanya matamanio yake kuwa ndio mungu wake? Basi je, wewe utakuwa ni wakili wake?**}. [Al Furqaan: 43].

Kwa kupitia matamanio mwanadamu anaingia katika kumuasi Allah kwa kufanya madhambi kama vile bidaa na ushirikina, mwenye kufuata matamanio yake hawezi kuamrisha mema wala kukataza mabaya, bali anafuata matakwa ya nafsi yake.

**4. Shirki Katika Twaa:** Nayo ni mtu kumtii binadamu mwenzie katika kuhalalisha yale aliyo yaharamisha Allah, au kuharamisha yale aliyo yahalalisha Allah, hilo pia Allah amelifanya kuwa ni ushirikina, amesema Allah Mtukufu: {**Au hao wana miungu ya kishirikina walio watungia dini asiyo itolea idhini Mwenyezi Mungu?**}. [Shuura: 21], na amesema Allah Mtukufu: {**Wamewafanya makuhani wao na wamonaki wao kuwa ni marabi badala ya Mwenyezi Mungu**}. [Tauba: 31], imekuja riwaya katika tafsiri ya Ayah ii kwamba Adiyyi bin Haatim alisema: Ewe Mjumbe wa Allah! Hatukuwa tunawaabu-

du, Mtume rehma na amani ziwe juu yake akasema: (Je si walikuwa wanahalalisha haramu nanyi mnakubali, na wanaharamisha haramu nanyi mnakubali?) akajibu akasema: Ndio! Mtume rehma na amani ziwe juu yake akasema: (Basi huko ndiko kuwaabudu).[13]

Shirki Ndogo Na Aina Zake

Maana ya shirki ndogo : Ni ile iliyotajwa katika Qur'an na Sunna kuwa ni shirki lakini haijafikia shirki kubwa.

Aina Za Shirki Ndogo:

1. Ni kuapa kwa asiyekuwa Allah.

2. Ni mtu kusema: Akipenda Allah na ukipenda wewe.

3. Mtu kusema: Lau kama siyo Allah na fulani.

4. Kutafuta elimu kwa lengo la kidunia, kama vile kupata shahada na kazi.

5. Kutafuta elimu kwa lengo la kujionyesha.

Na mfano wa hayo miongoni mwa mambo yanayo

13_ Hadithi hiyo amaitoa Imamu Tirmidhiy katika "Tafsiirul Qur'an" Vol. 8، Uk. 248. Na Imamu Bayhaqiy، Vol. 10، Uk. 116. Na Sheykhul Islaam ameifanya Hadithi hii kuwa nzuri katika Kitabu chake "Al Imaan" Uk. 64.

pingana na ikhlas.

Shirki Kubwa Na Hatari Zake

Mwenye kufanya shirki ndogo haishi Motoni milele, lakini shirki ndogo ni sababu ya mja kupata adhabu kali, hivyo basi haitakiwi kwa mja kuipuuzia shirki ndogo, na wanao ingia katika shirki ndogo ni wengi hasa hasa watu wenye elimu na wenye vyeo, na wasiokuwa na elimu ndio wengi zaidi wanaofanya shirki ndogo, na shirki ndogo inampelekea mtu kuingia katika shirki kubwa, kwahiyo ni wajibu kuchukua tahadhari.

Vigawanyo Vya Shirki Ndogo

Shirki ndogo imegawanyika katika sehem kuu mbili: Shirki ya wazi, na shirki iliyo fichikana:

1. Shirki Ya Wazi: Shirki hii imegawanyika katika sehem mbili:

(a) Shirki Katika Vitendo.

(b) Shirki Katika Maneno.

Ama shirki katika vitendo, ni kama vile kuvaa Bangili,

Uzi, Hirizi, na kuweka talasim (michoro ya waganga) kwa ajili ya kujikinga kutokana na vijicho au majini au maradhi au misiba na mfano wa hayo, hiyo ni shirki ndogo kwa sharti, mtu akiamini kuwa vitu hivyo vina uwezo wa kuleta manufaa na kuzuia madhara, basi hiyo inakuwa ni shirki kubwa, lakini akiamini ya kwamba vitu hivyo ni sababu ya kuleta manufaa au kuzuia madhara basi atakuwa amekosea, kasababu hiyo siyo sababu, na akuwa kaingia katika shirki ndogo.

Na shirki katika maneno: Ni kama vile kuapa kwa asiyekuwa Allah, kama vile kuapa kwa jina la baba, au jina la mama, au jina la babu, au Al Kaaba, au maisha, au kuapa kwa uhai, au kuapa kwa jina la Mtume Muhammad rehma na amani ziwe juu yake, na baadhi ya watu husema: Tumepata mvua kwasababu ya nyota fulani, au kusema: Akipenda Allah na wewe, au kusema: Lau siyo fulani basi tungeibiwa, na maneno mfano wa hayo.

2. Shirki Iliyo Fichikana: Miongoni mwa vigawanyo vya shirki ndogo ni shirki iliyo fichikana, na makusudio yake: Ni shirki iliyopo katika makusudio ya mtu na niya, na hiyo ni miongoni mwa aina zinazo tokea mara

nyingi, kiasi kwamba haja salimika mtu katika shirki hiyo si mwanachuoni wala mjinga, isipokuwa yule aliye rehemewa na Allah, na shirki hiyo ina mlango mpana zaidi.

Tofauti Kati Ya Shirki Kubwa Na Shirki Ndogo

| Shirki Kubwa | Shirki Ndogo |
|---|---|
| Mfanyaji Ataishi Motoni Milele | Mfanyaji Hataishi Motoni Milele |
| Inaharibu Matendo Yote | Haiharibu Matendo Yote |
| Mfanyaji Ni Halali Kuuliwa Na Mali Yake Kuchukuliwa | Mfanyaji Si Halali Kuuliwa Na Mali Yake Si Halali Kuchukuliwa |
| Mfanyaji Akifa Bila Ya Kutubia Hasamehewi Madhambi Yake | Mfanyaji Anakuwa Chini Ya Utashi Wa Allah Akitaka Atamuadhibu Na Akitaka Atamsamehe |

**Kuyazuru Makaburi**[14]

Allah Mtukufu amehalalisha waja wake kuyazuru makaburi kwa kuwahimiza ili waweze kujianda na safari ya kifo, na kuwaliwaza kutokana na yale yanayo wapata duniani, lakini pamoja na kuhalalisha hilo aliwabaishia kwamba kuyazuru makaburi kupo aina mbili, kuna namna

14- "Maarijul Qubuuli" Vol. 1, Uk. 417423-.

inayo faa na isiyofaa.

Vigawanyo Vya Kuzuru Makaburi

Kuyazuru makaburi kumegawanyika katika sehem kuu tatu:

1. Kuzuru kuliko ruhusiwa kisheria.

2. Kuzuru ambako ni bidaa.

3. Kuzuru ambako ni shirki.

(a) Kuzuru makaburi kuliko ruhusiwa kisheria:

Dalili inayo jizisha kuzuru makaburi ni hadithi ya Bureydah, amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Nilikuwa nimekukatazeni kuayazuru makaburi, sasa yazuruni, kwasababu yanawakumbusha Akhera).[15]

Adabu Za Kuyazuru makaburi

1. Iwe ni kwa engo la kukumbuka Akhera pamoja na kupata mawaidha kwa kuyaona makaburi.

2. Akusudie kujiombea mwenyewe pamoja na kuwaombea ndugu zake waumini waokufa.

15- "Sahihi Muslim" (977). Na "Sunanu Tirmidhiy" (1054). Na "Sunanu Nasaai" (2034)

3. Mtu asisafiri kwa ajili ya kuyazuru makaburi, kwasababu Mtume rehma na amani ziwe juu yake amelikataza hilo, kutokana na hadithi ya Abii Said Al Khudriy radhi za Allah ziwe juu yake alisema: Alisema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Mtu asisafiri kwa ajili ya ziara isipokuwa Misikiti mitatu: Msikiti mtukufu wa Makka, na Msikiti wangu huu (Msikiti mtukufu wa Madina), na Msikiti mtukufu wa Aqswa).[16]

(b) Kuzuru ambako ni bidaa:

Makusudio yake ni kuzuru kuliko tofautiana na mwongozo wa Mtume rehma na amani ziwe juu yake, kama vile kuyazuru makaburi kwa lengo la kwenda kuwaomba waliokufa, au kwenda kuswali makaburini au kukaa itikafu, au kufanya tawasuli kwa vyeo vya baadhi ya waliokufa, wanasema: Ewe Allah ninakuomba kupitia cheo cha fulani, akidhani ya kwamba mtu huyo ana cheo kwa Allah, hilo kosa kwasababu Allah hajaelekeza aombwe hivo, na mwenye kufanya hivo atakuwa amefanya uzushi katika dini, na atakuwa amefanya uadui katika dua.

(c) Kuzuru ambako ni shirki:

16- "Mukh'taswar Sahihi Bukhary" cha Shekh Albaaniy، Uk. 280، (613).

Maana yake ni mtu kwenda kuzuru makaburi akikusudia kumuomba aliye zikwa badala ya kumuomba Allah Mtukufu, anamuomba aliyekufa ili amuondolee madhara na kumpa manufaa kama, vile kuponya mgonjwa na kumrejesha aliye toweka na mfano wa hayo, mwenye kufanya atakuwa amemshirikisha Allah shirki kubwa, na hatasamehewa isipokuwa akitubia.

Amesema Allah Mtukufu: {**Na wala usiwaombe wasio kuwa Mwenyezi Mungu ambao hawakufai kitu wala hawakudhuru. Ukifanya hivyo basi utakuwa miongoni mwa walio dhulumu**. **Na Mwenyezi Mungu akikugusisha madhara, basi hapana wa kukuondolea ila Yeye. Na akikutakia kheri, basi hapana awezaye kurudisha fadhila yake**}. [Yunus: 106107-].

Na amesema Allah Mtukufu: {**Na nani mpotofu mkubwa kuliko hao wanao waomba, badala ya Mwenyezi Mungu, ambao hawatawaitikia mpaka Siku ya Kiyama, na wala hawatambui maombi yao**}. [Ahqaaf: 5].

Unafiki Na Aina Zake

**Unafiki maana yake:** Ni kudhihirisha uislamu na kucha ukafiri, na katika Qur'an kuna Sura iitwayo Surat Tauba, inaitwa ni Sura ya kufedhehesha, Sura hiyo imebainisha matendo ya wanafiki na ikawatahadharisha waislamu kutokana na shari zao na yale wanayoficha kutokana na matendo yao machafu na uadui dhidi ya waumini.

Aina Za Unafiki

Unafiki umegawanyika sehem kuu mbili: Unafiki mkubwa na unafiki mdogo.

**(a) Unafiki Mkubwa:**Makusudio yake ni unafiki katika itikadi, na unafiki huo umeganyika sehem kuu sita:

1. Kumkadhibisha Mtume rehma na amani ziwe juu yake.

2. Kukanusha baadhi ya mambo aliyokuja nayo Mtume rehma na amani ziwe juu yake.

3. Kumchukia Mtume rehma na amani ziwe juu yake.

4. Kuyachukia baadhi ya aliyokuja nayo Mtume rehma

na amani ziwe juu yake.

5. Kufurahia kuporomoka kwa dini ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake.

6. Kuchukia dini ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake pindi inapo pata nusra.

**(b) Unafiki Mdogo:** Makusudio yake ni unafiki katika matendo, unafiki huo ni katika madhambi makubwa, lakini haumtoi mtu katika uislamu.

Miongoni mwa aina za unafiki mdogo:

1. Uongo.

2. Khiyana.

3. Kwenda kunyume na ahadi.

4. Ugomvi unao tokana na uovu.

Na ushahidi juu ya jamabo hilo ni maneno ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Alama za mnafiki ni tatu, anapo ongea husema uongo, na anapo ahidi hatimizi, na anapo aminiwa hufanya khiyana), na katika upokezi mwingine: (Anapogombana anakuwa muovu -ugomvi

hauishi kwa kujenga chuki moyoni- na anapo aminiwa hufanya khiyana).[17]

Na miongoni mwa unafiki ni mtu kuacha kuswali swala ya Alfajiri na swala ya Ishaa kwa jamaa bila ya udhuru wa kisheria, amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Swala nzito kwa wanafiki ni swala ya Ishaa na swala ya Alfajiri, na lau wangelijua thawabu zinazo patikana katika swala hizo wangeziendea hata kwa kutambaa).[18]

**Uchawi Na Viini Macho Na Mengineyo:**[19]

1- Ukweli Kuhusu Uchawi:

Uchawi upo na unatokea, na lau kama usingekuwepo basi zisingekuja dalili za kisheria zinazo kataza uchawi,

wala yasingekuja makemeo makubwa na adhabu kali ya kidunia na Akhera kwa mwenye kufanya uchawi, na mtu kuomba hifadhi kwa Allah kutokana na uchawi ni jambo lililo amrishwa na limeelezwa katika dalili.

---

17- "Sahihi Bukhary" Vol. 5, Uk. 289. Na "Sahihi Muslim" Vol. 8. Uk. 78.
18- "Sahihi Bukhary" Vol. 2, Uk. 116. Na "Sahihi Muslim" (437).
19- "Bilaadul Haramayni Al Shariifayni Wal Mauqifu Al Swaarimu Minas Sihri Was Sahrah".

Na Allah Mtukufu ameeleza ya kwamba uchawi ulikuwepo hata enzi za Firauni, na yeye Firauni alitumia uchawi kutaka kupinga muujiza wa Nabii Mussa amani iwe juu yake.

**2- Je! Uchawi Unaathiri?**:

Ndiyo! Uchawi unaathiri, kuna uchawi unaosababisha mtu kuugua, na uchawi unaosababisha mtu kufa, na uchawi mwingine humfanya mtu kuwa kichaa, na mwingine humfanya mtu kuwa kipofu, na kuna uchawi unao tengenisha baina ya mume na mke, lakini uchawi hauathiri wenyewe isipokuwa unaathiri kwa mipangilio ya Allah na Qadari zake, kwasababu Allah ndiye aliyeumba kheri na shari, na uchawi ni katika shari, na kwasababu hiyo amesema Allah Mtukufu: {**Wala hawawezi kumdhuru mtu isipokuwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu**}. [Al Baqara: 102].

**3- Madhara Ya Uchawi Kwa Jamii Nzima Na Mtu Mmoja Mmoja**:

Madhara ya uchawi kwa mwanadamu: Uchawi unamuathiri mwanadamu katika ya kidunia na ya kidini, kwasababu unamfanya mtu aache kumtii Allah na badala yake anamuasi Mola wa walimwengu, kwasababu mtu aliye rogwa anaenda kwa wachawi na watu wa viini macho kwa ajili ya kutafuta tiba ili apone, na kwasababu hiyo mtu huyo anaingia katika ushirikina, amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Mwenye kumuendea mganga na kusadikisha yale anayosema, atakuwa amekufuru yote yakiyo teremka kwa Muhammad).[20]

Na athari za uchawi za kidunia: Uchawi ni sababu ya mtu kuugua au kufa au mtu kutojielewa katika mambo yake, uchawi unamfanya mtu aharibikiwe katika mipango yake, maisha yake yote yanageuka kuwa ni maumivu na huzuni.

Ama athari za uchawi kwa jamii: Athari hizo zipo wazi kwasababu jamii inajengwa na mtu mmja mmoja, ikiwa mtu atapatwa na uchawi basi jamii itakosa nguvu kazi.

Hakika uchawi una athari mbaya na ya wazi katika

---

20- Ameipokea Ibni Khezeymah، Vol. 1، Uk. 209، na meisahihisha Shekh Albaaniy، Vol. 1، Uk. 105، (523).

jamii, uchawi unapandikiza mashaka katika nafsi za watu, na unaleta chuki, vifundo na husda, na hasa mtu anapojua kuwa fulani ndiye aliye mroga, jambo hilo linapelekea kuwepo kwa visasi kwa namna yoyote, na hapo ndipo jamii inapo anza kuharibika na kuenea uadui pamoja na mauaji, na ni chanzo cha kupotea kwa tabia za kiislamu ambazo ndiyo sababu ya kupatikana amani na utulivu, na badala yake itatawala khofu na vitendo vya jinai.

**4- Hukumu Ya Uchawi Na Wachawi**:

Allah Mtukufu ametoa hukumu katika Qur'an tukufu kwa mwenye kujifunza uchawi kwa kusema: {**Wala hao hawakumfundisha yeyote mpaka wamwambie: Hakika sisi ni mtihani; basi usikufuru**}. [Al Baqara: 102].

Kujifunza uchawi ni haramu, kujifunza huko iwe ni kwa ajili ya kuufanyia kazi au kwa ajili ya kujikinga, na Mtume rehma na amani ziwe juu yake ameuweka uchawi kuwa ni katika madhambi saba yenye kuangamiza, amsema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Jiepusheni na madhambi saba yenye kuangamiza),[21] na miongoni mwa madhambi hayo akataja uchawi.

21_ "Sahihi Bukhary" Vol. 3، Uk. 197، Na Vol. 7، Uk. 29، Na Vol. 8، Uk. 33.

Ama hukumu ya mchawi: Wanachuoni wamekubaliana kwamba mchawi hukumu yake katika uislamu ni kuuliwa, na hukumu hiyo ilipokelewa kwa Maswahaba Allah awaridhie, kutoka kwa Jundubi amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Hukumu ya mchawi ni kuuliwa kwa upanga).[22]

Na kutoka kwa Bajaalah bin Abdah alisema: "Omar bin Khatwaab aliandika barua akisema: Waueni wachawi wa kiume na wakike" Bajaalah akasema: "Tukawaua wachawi watatu",[23] na kutoka kwa Hafswa radhi za Allah ziwe juu yake: "Aliamrisha mjakazi auliwe kwa sababu ya uchawi".[24]

### 5- Vipi Utaikinga Nafsi Yako Kutokana Na Uchawi?[25]

Unatakiwa kuikinga nafsi yako kutokana na uchawi kwa kufuata mambo yafuatayo:

1. Ni kuwa na tauhidi ya kumpwekesha Allah mmoja:

22_ Ameipokea Imamu Tirmidhiy، Vol. 5، Uk. 156.
23_ "Muswannafu Abdul Razaaq" Vol. 10، Uk. 179. Na "Musnadi Imamu Ahmad" Vol. 1، Uk. 190.
24 "Al Bukhaariyyu Fiy Taariikhil Kabiir" Vol. 2، Uk. 222.
25_ "Bilaadul Haramayni Al Shariifayni Wal Mauqifu Al Swaarimu Minas Sihri Was Sahrah".

Na hilo linapatikana kwa mtu kuufanya moyo wake uambatane na Allah peke yake, pamoja na kujiepusha na shirki na aina zake zote, na kujiepusha kutokana na dhambi kubwa na ndogo, kwasababu mambo hayo yana athari kubwa katika kuzuia shari na uchawi kwa idhini ya Allah.

2. Ni kuwa na ikhlas: Kufanya ibada kwa ajili ya Allah ni njia pekee ya kujiepusha na shetani, amesema Allah Mtukufu akimzungumzia shetani: {**Akasema: Mola wangu Mlezi! Ilivyo kuwa umenitia makosani, basi nahakikisha nitawazaini hapa duniani na nitawapoteza wote**. **Ila waja wako walio safika**}. [Al Hijri: 3940-].

3. Ni kujilazimisha kuwa katika jamaa na kuto kujitenga, amesema Mtume rehma na amni ziwe juu yake: (Yeyote mwenye kutaka maisha mazuri ya Peponi basi ajilazimishe kuwa katika jamaa, kwasababu shetani yuko pamoja na mwenye kujitenga, na yuko mbali wenye kushikamana).[26]

26_ Ameipokea Imamu Tirmidhiy، na amesema hadithi ni nzuri na ni sahihi، Vol. 4، Uk. 465.

4. Ni kudum na swala tano kwa jamaa: Na hasa swala ya Alfajiri, kwasababu mtu kuipuuzia swala ya jamaa ni rahisi shetani kumpoteza.

5. Ni kushikamana na Qur'an na Sunna: Hii ni njia kubwa ya kujikinga na shetani, mwenye kujifunza Qur'an na Sunna na akavifanyia kazi inakuwa ni kinga kwake kutokana na shari za wachawi na maganga, amepokea Ibn Jauziy kutoka kwa A'amash alisema: "Alitueleza bwana mmoja aliyekuwa akiongea na majini, majini wakamwambia: Hakuna mtu makali na anaetupa shida kama mtu anaefuata Sunna, ama mtu anaefuata matamanio hakika sisi tunamchezea kila wakati ".[27]

6. Ni kumcha Allah na kumtegemea Yeye, amesema Allah Mtukufu: {**Na tukawaokoa walio amini na wakawa wanamcha Mungu**}. [Fusswilat: 18].

7. Ni kutubu toba ya kweli na kuyaepuka madhambi.

8. Ni kutoa sadaka na kufanya wema pamoja na kusaidia watu, miongoni mwa njia zinazo mkinga mtu kutokana na shari ni kuwapa masikini sadaka pamoja na wenye

27_ "Talbiis Ibiliis" Uk. 39.

kuhitaji, hakika kufanya hivo kunazuia shari nyingi.

9. Ni kufanya Ruqya ya kisheria: Na ili Ruqya iwe sahihi ni lazima yatimie masharti yafuatayo:

(a) Iwe ni kwa Maneno ya Allah au Majina yake na Sifa zake.

(b) Iwe ni kwa lugha ya kiarabu au lugha inayo julikana maana yake.

(c) Mtu aamini ya kwamba Ruqya haiathiri yenyewe bali ni sababu, lakini anaeponya ni Allah Mtukufu.

Somo La Tatu: Shahada Mbili

Somo Hili Linakusanya Vipengele Vifuatavyo:

1- Maana Ya Tauhidi.

2- Maana Ya Uislamu.

3- Haki Ya Allah Kwa Waja Wake.

4- Aina Za Ibada.

5- Aina Za Tauhidi.

6- Tauhidi Ya Kielimu Na Itikadi.

7- Tauhidi Ya Uungu.

8- Tauhidi Ya Ibada.

9- Tauhidi Ya Majina Ya Allah Na Sifa Zake.

10- Athari Ya Tauhidi Katika Ibada Na Ubora Wake.

11- Maana Ya Laa Ilaaha Ila LLah.

12- Maana Ya Muhammad Rasuulu LLah.

13- Ibada.

14- Ibada Ambazo Ni Sababu Ya Kuumbwa Kwa Mwanadamu.

15- Sharti Za Ibada.

16- Misingi Ya Ibada.

Shahada Mbili

**Elimu ya tauhidi:** Ni elimu inayo elezea mambo ya wajibu kwa Allah, kama vile Sifa zake zenye utukufu na zilizo kamilika, na inaelezea yale ambayo Allah hawezi kusifika nayo katika vitendo vyake, tauhidi inaeleza pia mambo yanayo wapasa waja kumfanyia Allah, kama vile kumtakasia ibada na kutekeleza haki zake na kutii amri zake pamoja na kujiepusha na makatazo yake, inaeleza pia mambo yaliyo ya wajibu kwa Mitume na mambo ambayo hayafai kufanyiwa Mitume na yanayo faa kuwafanyia, tauhidi vilevile inaelezea juu ya kuamini Mitume pamoja na Vitabu walivyo teremshiwa, na inaelezea pia juu ya kuamini Malaika watukufu, na kuamini siku ya kufufuliwa na kulipwa, na kuamini Qadari mipangilio ya A llah na hukumu zake.

Na Faida Ya Tauhidi: Ni kuisahihisha itikadi ya kiislamu kutokana na mambo mabaya na kupata mafanikio duniani na Akhera.

Maana Ya Uislamu

Uislamu ni kujisalimisha kwa Allah kwa kumpwekesha

na kunyenyekea pamoja na kutii, na kujiepusha na shirki.

Amesema Allah Mtukufu: {**Na nani aliye bora kwa dini kuliko yule aliye usilimisha uso wake kwa Mwenyezi Mungu**}. [Nisaa: 125].

Na amesema Allah Mtukfu: {**Na mwenye kuuelekeza uso wake kwa Mwenyezi Mungu, naye akawa anafanya wema, basi huyo hakika amekwisha kamata fundo lilio madhubuti**}. [Luqmaan: 22].

Na amesema Allah Mtukufu: {**Basi Mungu wenu ni Mungu Mmoja tuJisalimishieni kwake tu, na wabashirie wanyenyekevu**}. [Al Hajj: 34].

Na neno Uislamu linapo tamkwa linakuwa na maana ya Uislamu wote, anasema Allah Mtukufu: {**Bila ya shaka Dini mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu**}. [Al Imraan: 19].

Katika Aya hiyo Uislamu umekusanya nguzo tano, na dalili juu ya hilo ni hadithi ndefu ya Jibril pindi alipokuja kwa ajili ya kuwafundisha watu dini yao, akasema: (… Uislamu ni kushuhudia ya kwamba hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah, na kwamba Mu-

hammad ni Mtume wa Allah, na kusiamamisha swala, na kutoa zaka, na kufunda mwezi wa Ramadhan, na kuhiji Makka kwa mwenye uwezo).[28]

Haki Ya Allah Kwa Waja Wake

Haki ya Allah kwa waja wake ni kumuabudu na kutokumshirikisha na chochote, Allah amewaumba waja wake kwa lengo la kufanya ibada, amesema Allah Mtukufu: {**Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu Mimi**}. [Dhaariyaat: 56].

Na amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Haki ya Allah kwa waja wake ni wao kumuabudu na kuto mshirikisha na chochote).[29]

Maana Ya Ibada

Ibada ni jina lilikusanya kila anacho kipenda Allah, miongoni mwa kauli na vitendo, kama vile dua, swala, unyenyekevu, nadhiri, kuchinja, khofu, matarajio na mengineyo.

---

28_ "SAHIHI BUKHARY" VOL. 1، UK. 120. NA "SAHIHI MUSLIM" VOL. 1، UK. 30.

29_ "Sahihi Bukhary" Vol. 4، Uk. 84. Na "Sahihi Muslim" Vol. 1، Uk. 58.

Amesema Allah Mtukufu: {**Sema: Hakika Sala yangu, na ibada zangu, na uhai wangu, na kufa kwangu, ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote**. **Hana mshirika wake. Na hayo ndiyo niliyo amrishwa, na mimi ni wa kwanza wa Waislamu**}. [Al An'aam: 162163-].

Na ibada ina aina nyingi, miongoni mwa hizo: Ni dua, khofu, matarajio, kutegemea, kuhitaji, kuogopa, kuchinja, kutoa nadhiri, kurukuu, kusujudu, kutufu, kuapa, unyenyekevu, kuomba msaada, kuomba nusra na mfano wa hayo miongoni mwa ibada za kisheria.

Na Sura nyingi za Qur'an au Qur'an nzima imeamrisha juu ya tauhidi na haki zake na imeeleze malipo ya watu wa tauhidi, na imekemea ushirikina na washirikina na kubainisha malipo ya washirikina.

Mitume wote wametumwa kwa ajili ya kuilingania tauhidi, amesema Allah Mtukufu: {**Na kwa hakika kwa kila umma tuliutumia Mtume kwamba: Muabuduni Mwenyezi Mungu, na muepukeni Shetani**}. [Al Nahli: 36].

Yeyote mwenye kuipata tauhidi atakuwa amepata uongofu duniani, na atasamehewa madhambi yake na atasalimika siku ya Qiyama kutokana na adhabu ya milele.

Amesema Allah Mtukufu: {**Wale ambao wameamini, na hawakuchanganya imani yao na dhulma - hao ndio watakao pata amani na wao ndio walio ongoka**}. [Al An'aam: 82].

Na amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Haki ya waja kwa Allah ni kuto muadhibu yeyote asiye mshirikisha Allah).[30]

Aina Za Tauhidi

Tauhidi Ipo Aina Mbili:

**Aina Ya Kwanza:Ni tauhidi katika elimu na itikadi**: Na inaitwa tauhidi ya kielimu, na inaambatana na habari alizo zieleza Allah na maarifa, miongoni mwa Sura zinazo izunguzia tauhidi hiyo ni kauli Allah Mtuku-

30_ Ameipokea Imamu Bukhary na Muslim.

fu: {**Sema: Yeye Mwenyezi Mungu ni wa pekee. Mwenyezi Mungu Mkusudiwa. Hakuzaa wala hakuzaliwa. Wala hana anaye fanana naye hata mmoja**}. [Al Ikhlaas: 1-4], na aina hiyo inakusanya tauhidi ya Uungu na tauhidi ya Majina ya Allah na Sifa zake.

**Aina Ya Pili: Ni tauhidi katika utashi na makusudio**: Na inaitwa tauhidi katika makusudio, na Sura inayo elezea tauhidi hiyo ni Suratul Kafiruun.

Na aina hiyo inakusanya tauhidi ya Uungu na tauhidi ya ibada.

Aina Tatu Za Tauhidi

1. Tauhidi Ya Uungu.

2. Tauhidi Ya Ibada.

3. Tauhidi Ya Majina Ya Allah Na Sifa Zake.

**(a) Tauhidi Ya Uungu:** Ni kumpwekesha Allah kupitia vitendo vyake, kama vile kuumba, kutoa rizki, kupangilia mambo, kuhuisha, kufisha, kufufua, na mfano wa hayo, na washirikina wanaikubali aina hiyo, lakini kukubali kwao hakukuwanufaisha wala kuwafanya wawe waislamu,

amesema Allah Mtukufu: {**Na ukiwauliza: Ni nani aliye ziumba mbingu na ardhi. Bila ya shaka watasema: Mwenyezi Mungu**}. [Zumar: 38].

Na dalili ya aina hiyo ya tauhidi ni kauli ya Allah Mtukufu: {**Sifa njema zote ni za Mwenyeezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote**}. [Al Faatiha: 1].

Kukiri juu ya kuwepo kwa Allah na kukubali ya kuwa Yeye ndiye muumbaji, na ndiye mtoa rizki na mwenye kupangilia mambo, haitoshi kumuingiza mtu katika uislamu, kwasababu washirikina wengi wanaikubali tauhidi hiyo lakini haiwaingizi katika uislamu kwasababu ya kuto kukubali kwao tauhidi ya ibada, na watu wengi wanadhani ya kwamba Mitume walitumwa ili walinganie tauhidi ya Uungu, na wanadhani ya kwamba wakiithibisha tauhidi hiyo watakuwa wamempwekesha Allah, na hilo ni kosa la wazi, ndiyo maana wanaabudu kisichokuwa Allah na wanadai ya kuwa siyo shirki, kwasababu wanaamini ya kwamba shirki ni kujaalia ya kwamba Allah ana mshirika katika kuumba au kutoa rizki- ama kumshirikisha Allah katika ibada huo si ushirikina kama wanavyodai- basi kutokana na ujinga huo wanajikuta wanamshirikisha Allah waziwazi.

**(b) Tauhidi Ya Ibada:** Ni kumpwekesha Allah kwa kufanya ibada na kuto mshirikisha na kitu chochote, ibada zote zinatakiwa zifanywe kwa ajili ya Allah, yeyote mwenye kumfanyia ibada asiyekuwa Allah atakuwa ni mshirikina hata kama atakiri tauhidi ya Uungu.

Mitume wote wametumwa ili kuifikisha tauhidi ya ibada, na Vitabu vikateremshwa kwasababu hiyo, mwenye kuijua tauhidi hiyo ukweli wa kuijua basi atafahamu upotovu walionao watu wengi na namna wanavyo ipuuzia tauhidi na kutojua haki zake.

Na ijulikiane ya kwamba tauhidi siyo kuacha kuabudu asiyekuwa Allah pekee, kama vile masanamu na mizimu, bali lazima mtu aache ibada zote anazo zifanya kwa asiyekuwa Allah na ajiweke mbali, na ibada zake zote azifanye kwa ajili ya Allah.

Mwenye kumuabudu Allah kisha akawa hajakufuru vyote vinavyo abudiwa kinyume na Allah, mtu huyo atakuwa hajashikamana na uislamu.

Amesema Allah Mtukufu: {**Basi anaye mkataa Shet›ani na akamuamini Mwenyezi Mungu bila ya shaka amekamata kishikio madhubuti**}. [Al Baqara: 256].

Na katika Sahihi Muslim amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Mwenye kusema laa ilaha ila LLah na akakufuru yote yanayo abudiwa kinyume na Allah, mali yake itakuwa haramu kuchukuliwa, na ni haramu kumwagwa damu yake, na hesabu yake itakuwa kwa Allah).[31]

Yeyote asiyemkufuru twaghuuti atakuwa hajashikamana na laa ilaha ila LLah (Uislamu), bali atakuwa ameuacha uislamu na kuupuuza pamoja na kupoteza haki zake, vilevile damu yake itakuwa halali kumwagwa na mali yake ni halali kuchukuliwa.

Asili ya tauhidi ya Mitume waliyo ilingania ni kumpwekesha Allah katika ibada na kujiweka mbali na kila kinacho abudiwa kinyume na Allah, hiyo ndiyo dini ya Nabii Ibrahim ambayo Allah ameizungumzia kwa kusema: {**Hakika nyinyi mna mfano mzuri kwenu kwa Ibrahim na wale walio kuwa pamoja naye, walipo**

31- "Sahihi Muslim" Vol. 1، Uk. 53.

**waambia watu wao: Hakika sisi tumejitenga nanyi na hayo mnayo yaabudu badala ya Mwenyezi Mungu. Tunakukataeni; na umekwisha dhihiri uadui na chuki baina yetu na nyinyi mpaka mtakapo muamini Mwenyezi Mungu peke yake**}. [Al Mumtahinah: 4].

Na maesema Allah Mtukufu: {**Na pale Ibrahim alipo mwambia baba yake na kaumu yake: Hakika mimi ninajitenga mbali na hayo mnayo yaabudu**. **Isipo kuwa yule aliye niumba, kwani Yeye ataniongoa**. **Na akalifanya hili liwe neno lenye kubaki katika vizazi vyake ili warejee**}. [Zukhruf: 2628-].

Ukiangalia hali ya tauhidi ya ibada katika zama zetu hizi utakuta imepotea kwa watu wengi mpaka alama zake, na tutatoa mifano miwili:

**Mfano Wa Kwanza:** Kuchinja ni miongoni mwa ibada tukufu, Allah alimwambia Mtume wake kwa kusema: {**Basi sali na uchinje kwa ajili ya Mola wako Mlezi**}. [Al Kauthar: 2].

Ukishajua ya kwamba kuchinja ni ibada basi kuchinja kwa ajili ya asiyekuwa Allah ni shirki.

Katika Sahihi Muslim kutoka kwa Ally radhi za Allah ziwe juu yake alisema: “Mtume rehma na amani ziwe juu yake aliniambia mambo manne: Miongoni mwa hayo alisema: (Allah amemlaani mwenye kuchinja kwa ajili ya asiyekuwa Allah)”.[32]

Katika zama hizi limekithi jambo la kuchinja kwa ajili ya asiyekuwa Allah kwa watu wengi wasiojua tauhidi ya ibada, baadhi ya wajinga wanapo hamia katika nyumba wanachinja kwa ajili ya kujikurubisha kwa majini ili yasiwaudhi na mfano wa hayo, na kufanya hivo ni kushirikisha.

**Na Mfano Wa Pili:** Kumuomba asiyekuwa Allah: Dua ni kiashiria kikubwa cha utumwa wa mja kwa Allah, na miongoni mwa sababu kubwa na zenye nguvu katika kuleta manufaa na kuzuia madhara, na nia alama za mja kumuhitajia Mola wake, Allah Mtukufu ameamrisha waja wake wamuombe kwa kusema: {N**a Mola wenu Mlezi anasema: Niombeni nitakuitikieni**}. [Ghaafir: 6].

Na Mtume rehma na amani ziwe juu yake amesema :

---

32_ “Sahihi Muslim” Vol. 3، Uk. 1567.

(Dua ndiyo ibada).[33]

Ikiwa dua ni katika ibada tukufu basi kumfanyia asiyekuwa Allah ni ushirikina, lakini tazama hali za watu wengi wanao jinasbisha na uislamu namna wanavyo waomba watu waliokufa, wanaacha kumuomba Allah Mtukufu na badala yake wanawaomba walio makaburini, utawaona wakiwaomba kwa unyenyekevu kana kwamba wanawasikia, na wanawaomba msaada kana kwamba wapo hai na wana uwezo wa kuwasaidia, amesema Allah Mtukufu: {**Na hao mnao waomba badala yake hawamiliki hata ugozi wa kokwa ya tende. Mkiwaomba hawasikii maombi yenu; na hata wakisikia hawakujibuni. Na Siku ya Kiyama watakataa ushirikina wenu. Na hapana atakaye kupa khabari vilivyo kama Yeye Mwenye khabari**}. [Faatwir: 1314-].

Kuomba uombezi kwa waliokufa wakiwemo Manabii, watu wema na wengineo na kutaka msaada kwao ni shirki inayo pingana na tauhidi ya ibada, na mwenye kufanya hayo hana msamaha kwa Allah isipokuwa akitubia, na

33- "Sunanu Tirmidhiy" (3371). Na "Fathul Baariy" Vol. 11, Uk. 94. Na "Kanzul Ummaali" (3114).

mwenye kufa bila ya kutubia basi atakuwa ni katika watu watakao ishi Motoni milele, tunamuomba Allah atukinge na hayo.

**(c) Tauhidi Ya Majina Ya Allah Na Sifa Zake:** Maana ya kumpwekesha Allah katika Maji yake na Sifa zake: Ni Yeye Allah kuitwa na kusifika kwa Majina aliyo jiita mwenyewe na Sifa alizo jisifu mwenyewe, au Majina na Sifa alizo zieleza Mtume rehma na amani ziwe juu yake, bila kupotosha wala kubadilisha, na bila ya kugeuza wala nkufananisha.

Na ushahidi juu ya kuamini Majina ya Allah ni kauli ya Allah Mtukufu: {**Na Mwenyezi Mungu ana majina mazuri kabisa, basi muombeni kwa hayo**}. [Al A'araaf: 180].

Na amesema Allah Mtukufu: {**Mwenyezi Mungu! Hapana mungu isipo kuwa Yeye. Yeye ana majina mazuri kabisa**}. [Twaha: 8].

Na amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Hakika Allah ana majina tisini na tisa mwenye kuyahifadhi ataingia Peponi).[34]

---

34_ "SAHIHI BUKHARY" VOL. 11، UK. 180190_. NA "SAHIHI MUSLIM" (2677)

Na kuyakanusha Majina ya Allah na Sifa zake ni kumkanusha Allah mwenyewe na kumkataa, na mtu haingii katika uislamu mpaka ayaamini Majina ya Allah na Sifa zake.

Aina hiyo ya tauhidi ni wajibu kuizingatia na kuifahamu, baadhi ya Wanachuoni wamekosea katika kuifahamu tauhidi hiyo ikawa ni sababu ya wafuasi wao kupotea, wakakanusha Sifa za Allah ambazo amejisifu mwenyewe, wakidai kwamba kufanya hivo ni kumfananisha Allah na viumbe, wakapotea kutokana na ufahamu wao mbovu, na akapinga yale yaliyokuja katika Qur'an na Sunna na makubaliano ya wema walio tangulia.[35]

Tauhidi Athari Zake Na Ubora Katika Ibada

1. Mwenye kuwa na tauhidi ataingia Peponi bila kuhesabiwa wala kuadhibiwa.

2. Tauhidi ni sababu ya kusamehewa madhambi.

3. Tauhidi inamzuia mtu kuishi milele Motoni.

35- "Al Qaulur Rashiid fiy Haqiiqati Tauhiidi".

4. Tauhidi ni sababu ya mtu kupata uongofu na amani iliyo kamilika duniani na Akhera.

5. Ibada zote zinakubaliwa kwasababu ya tauhidi.

6. Tauhidi ni sababu ya kumpunguzia mja mambo mabaya na maumivu ya moyo, kwasababu anajua ya kwamba yote yanayo mpata yamepangwa na Allah.

7. Allah alichukua dhamana ya kuwapa ushindi na nusra watu wa tauhidi.[36]

Maana Ya Laa Ilaaha Ila ALLah

Laa ilaaha ila LLah iliyoelezwa katika Qur'an na Sunna maana yake: Hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Alla, na neno hilo tukufu limekusanya nguzo mbili:

1. Ni kukanusha vyote vinavyo abudiwa kinyume na Allah.

2. Ni kuthibitisha ya kwamba anaestahiki kufanyiwa ibada zote ni Allah peke yake.

Hakika Allah hana mshirika katika Ufalme wake,

36. "Al Qaulus Sadiidi Lisharhi Kitaabi Tauhiidi" cha Ibn Saadiy, Uk. 1619.

amesema Allah Mtukufu: {**Hayo ni kwa kuwa Mwenyezi Mungu ndiye Wa Kweli, na kwamba wale wanao waomba badala yake, ni baat›ili, na hakika Mwenyezi Mungu ndiye Aliye Juu na ndiye Mkubwa**}. [Al Hajj: 62].

Maana Ya Kushuhudia Ya Kwamba Muhammad Rehma Na Amani Ziwe Juu Yake Ni Mjumbe Wa Allah

Maana Yake: Ni kukiri kwa moyo na kutamka kwa ulimi ya kwamba Muhammad ni mja wa Allah na ni Mtume wake kwa walimwengu wote watu na majini, ametumwa akiwa ni shahidi kwao na mwenye kuwabashiria Pepo na kuwaonya kutokana na Moto, na ni mwenye kulingania katika njia ya Allah, na ni taa yenye mwangaza, ni wajibu kumsadikisha katika yote aliyo yaeleza miongoni mwa habari za watu walio tangulia na habari zitakazo tokea, na ni wajibu kumsadikisha kwa yale aliyo yahalalisha na yale aliyo yaharamisha pamoja na kutekeleza amri zake na kuacha yale aliyo yakataza, na ni wajibu kufuata sheria zake na Sunna zake pamoja na kuridhia yale yote aliyo kuja nayo pamoja na kusalim amri.

Amesema Sheykhul Islaam Muhammad bin Abdul Wahaab Allah amrehemu: “Na maana ya kushuhudia ya

kwamba Muhammad ni Mjumbe wa Allah: Ni kumtii kwa yale aliyo yaamrisha na kumsadikisha kwa yale aliyo yaeleza, na kujiepusha na yale aliyo yakataza, na aabudiwe Allah kama alivyo fundisha Mtume rehma na amani ziwe juu yake ”.[37]

Ibada

Amesema Allah Mtukufu: {**Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu Mimi**}. [Dhariyaat: 56].

Mwenye kuzingatia Aya hiyotukufu ataona kwamba Aya hiyo imebainisha malengo makubwa ya kuumbwa kwetu, na malengo hayo ni kumuabudu Allah pekee katika ardhi yake, hayo ndiyo majukumu ambayo mwenye kuyatekeleza atakuwa ametimiza malengo ya kuwepo kwake duniani, na mwenye kuzembea katika hilo atakuwa malengo ya kuumbwa kwake.

Ibada ambayo ni sababu ya kuumbwa wanadamu

**Na maana ya ibada hiyo:** Ni jina lililo kusanya kila analo lipenda Allah na kuliridhia miongo no mwa maneno na vitendo vya wazi na vya siri, pamoja na kujiweka mbali

37_ “Al Uswuulu Thalaatha”.

na kila kinacho pingana na ibada.

## Masharti Ya Ibada[38]

Ili ibada iwe sahihi ni lazima yatimie masharti matatu:

1. Azma ya kweli: Sharti hilo ni lazima liwepo katika ibada, na amaana yake ni kuacha uvivu na kufanya bidii katika kutekeleza ibada ili maneno yaendane na vitendo, amesema Allah Mtukufu: {**Enyi mlio amini! Kwa nini mnasema msiyo yatenda? Yanachukiza vikubwa mno kwa Mwenyezi Mungu kuwa mnasema msiyo yatenda**}. [Swaff: 23-].

2. Ni na ikhlas katika niya: Maana yake ni kwamba mja akusudie kupata radhi za Allah katika matendo yake yote ya siri na ya dhahiri, amesema Allah Mtukufu: {**Nao hawakuamrishwa kitu ila wamuabudu Mwenyezi Mungu kwa kumtakasia Dini, wawe waongofu**}. [Al Bayyinah: 5].

3. Ikubaliane na sheria aliyo iamrisha Allah, mja haruhusiwi kumuabudu Allah isipokuwa kwa kufuata sheria na taratibu zilizo wekwa, na kufuata sheria ya

38- "Maarijul Qabuuli" Vol. 1، Uk. 399.

Allah ndiyo uislamu, na mtu hatokubaliwa kufuata dini isiyokuwa uislamu, amesema Allah Mtukufu: {**Na anaye tafuta dini isiyo kuwa Uislamu haitakubaliwa kwake**}. [Al Imraan: 85].

Na kutoka kwa Aisha radhi za Allah ziwe juu yake alisema: Alisema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Mwenye kuzua katika dini yetu hii jambo ambalo halimo basi atarejeshewa mwenyewe).[39]

Hizo ni sharti tatu za ibada ambazo haikubaliwi ibada mpaka zikamilike.

Misingi Ya Ibada

Ibada Inajengwa Katika Misingi Miwili:

1. Mapenzi yaliyo kamilika.

2. Udhalili ulio timia.

Ibada haina manufaa ikiwa haitakusanya misingi yote miwili, kwasbabu hiyo wamesema baadhi ya walio tangulia: Mwenye kumuabudu Allah kwa mapenzi pekee mtu

39 _ "SAHIHI BUKHARY" VOL. 2، UK. 166. NA "SAHIHI MUSLIM" VOL. 5، UK. 132.

huyo atakuwa zindiiqi,[40] na mwenye kumuabudu Allah kwa matarajio pekee mtu huyo ni Murjia,[41] na mwenye kumuabudu Allah kwa khofu pekee mtu huyo Haruuriy,[42] na mwenye kumuabudu Allah kwa mapenzi, khofu na matarajio, huyo ndiye muumini wa kweli mwenye kumpwekesha Allah.[43]

Amesema Allah Mtukufu: {**Lakini walio amini wanampenda Mwenyezi Mungu zaidi sana**}. [Al Baqara: 165].

Na amesema Allah Mtukufu: {**Kwa hakika hao ambao kwa kumwogopa Mola wao Mlezi wananyenyekea**}. [Al Muuminun: 57].

Na amesema Allah Mtukufu: {**Hakika wao walikuwa wepesi wa kutenda mema, na wakituomba kwa shauku na khofu, nao walikuwa wakitunyenyekea**}. [Al Anbiyaa: 90].

40 - Zindiiq: Ni mnafiki anaedhihirisha uislamu na kuficha ukafiri.
41 - Murjia: Ni kundi lililo potea ambalo linaamini ya kwamba n imani haizidi wala haipungui, na muanzilishi wa kundi hilo ni Abdallah bin Sabai, Myahudi.
42 - Al Haruuriy: Ni katika makundi yaliyo potea yanayo jinasbisha na uislamu, na asili ya kundi hilo ni katika mji wa Kuufah Iraq, kundi hilo lilimuasi Ally bin Abii Twaalib radhi za Allah ziwe juu yake, na itikadi yao ni kwamba mwenye kufanya dhambi kubwa ni kafiri.
43- "Maarijul Qabuuli" Vol. 1, Uk. 397".

Somo La Nne: Swala

Somo Hili Linakusanya Vipengele Vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | Twahara. | 2 | Aina Za Twahara. |
| 3 | Twahara Ya Kimaana. | 4 | Twahara Ya Kuhisi. |
| 5 | Kukidhi Haja Na Adabu Zake. | 6 | Adabu Kabla Ya Kujisaidi. |
| 7 | Adabu Baada Ya Kujisaidia. | 8 | Kutawadha (Kushika Udhu). |
| 9 | Namna Ya Kutawadha. | 10 | Dalili Za Kutawadha |
| 11 | Ubora Wa Kutawadha. | 12 | Faradhi Za Udhu. |
| 13 | Sunna Za Udhu. | 14 | Mambo Ya Karaha Katika Udhu. |
| 15 | Sifa Za Udhu Unaofaa | 16 | Sifa Za Udhu Uliokamilika. |
| 17 | Vitenguzi Vya Udhu. | 18 | Mambo Muhimu Katika Udhu. |
| 19 | Kupaka Juu Ya Khofu Mbili. | 20 | Sharti Za Kupaka Juu Ya Khofu Mbili. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 21 | Muda Wa Kupaka. | 22 | Namna Ya Kupaka. |
| 23 | Yanayo Batitilisha Kupaka Juu Ya Khofu. | 24 | Kuoga |
| 25 | Yanayompasa Mtu Kuoga. | 26 | Namna Ya Kuoga. |
| 27 | Kutayamamu. | 28 | Muda Wa Kutayamamu. |
| 29 | Namna Ya Kutayamamu. | 30 | Hedhi Na Nifasi Na Damu Ya Ugonjwa. |
| 31 | Maana Ya Hedhi | 32 | Maana Ya Damu Ya Ugonjwa. |
| 33 | Baadhi Ya Hukumu Za Mwenye Hedhi Na Nifasi. | 34 | Hali Za Mwenye Damu Ya Ugonjwa. |
| 35 | Baadhi Ya Hukumu Za Mwenye Damu Ya Ugonjwa. | 36 | Swala. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 37 | Maana Ya Swala. | 38 | Hukumu Ya Mwenye Kuacha Kuswali |
| 39 | Nguzo Za Swala. | 40 | Sharti Za Swala. |
| 41 | Mambo Ya Wajibu Katika Swala. | 42 | Namna Ya Kuswali. |
| 43 | Swala Ya Jamaa | 44 | Ubora Wa Swala Ya Jamaa. |
| 45 | Hukumu Ya Swala Ya Jamaa. | 46 | Idadi Inayotakiwa. |
| 47 | Nyudhuru Za Kuacha Jamaa. | 48 | Hukumu Zinazo Ambatana Na Maamuma. |
| 49 | Hukumu Zinazo Ambatana Na Imamu. | 50 | Swala Ya Mgonjwa. |
| 51 | Swala Ya Ijumaa | 52 | Hukumu Ya Swala Ya Ijumaa. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 53 | Anaewajibikiwa Na Swala Ya Ijumaa. | 54 | Hekima Ya Swala Ya Ijumaa. |
| 55 | Sharti Za Kuswihi Swala Ya Ijumaa. | 56 | |
| 57 | Swala Ya Iddi Mbili. | 58 | Hukumu Za Swala Ya Iddi Mbili. |
| 59 | Muda Wa Swala Ya Iddi Mbili. | 60 | S e h e m u Inaposwaliwa |
| 61 | Namna Inavyo Swaliwa | 62 | Swala Ya Kupatwa Jua. |
| 63 | Hukumu Yake. | 64 | Namna Inavyo Swaliwa. |
| 65 | Swala Ya Sunna. | 66 | Swala Ya Jeneza. |
| 67 | Hukumu Ya Swala Ya Jeneza. | 68 | Sharti Zake. |
| 69 | Namna Inavyo Swaliwa. | 70 | Yanayo Husiana Na Swala Ya Jeneza. |

Twahara

Hukumu Yake:

Twahara ni jambo la waajibu (Lazima), kwa mujibu wa Qur'an na Sunna.

Amesema Allaah Mtukufu : {**Na mkiwa na janaba basi ogeni**}. [Al Maida: 6]. Na amesema tena: {**Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wanao tubu na huwapenda wanaojisafisha**}. [Al Baqara: 222].

Na amesema Mtume Rehema na Amani zimshukie: (Ufunguo wa swala ni Usafi).[44]

Aina Zake:

Usafi umegawanyika katika sehemu kuu mbili : Usafi wa kimaana (Ndani) na Usafi wa kuhisi (nje).

Usafi Wa Kimaana (Ndani):

Huu unakusudiwa kuisafisha nafsi kutokana na athari za madhambi na maaswi.Na hupatikana kwa kufanya toba ya kweli, na kuisafisha nafsi kutokana na ushirikina, shaka,

44_ Imepokelewa na Ahmad (1129 ،123\1)، Abu Daud ، Tirmidhiy، Ibnu Maajah na AL Haakimu.Imewafikiwa na Imam Adh Dhahabiy.

husda, chuki, khiyana, kibri, kupenda cheo na uongozi. Na usafi huu haupatikani ispokuwa kwa kuwa na Ikhlaswi (Utakaso), kupenda kheri, upole, unyenyekevu, ukweli, kutarajia radhi za Allaah katika matendo.

Usafi Wa Kuhisi (Nje):

Huu unakusudiwa kujisafisha kutokana na "Khubthi' na "Hadathi".

Kusafisha **"Khubthi"** kunakuwa kwa kuondosha najisi kwa maji safi, kutoka katika nguo ya Mwenye kuswali, mwili wake na sehemu anaposwalia.

Na kusafisha **"Hadathi"** kunakusudiwa kutawadha, kuoga na kutayammamu.

Kukidhi Haja(Kujisaidia) Na Adabu Zake:

Kukidhi haja (kujisaidia) kuna adabu zake, miongoni mwa hizo ni:

Kwanza: Kabla Ya Kujisaidia:

1. Kutafuta sehemu isiyo na watu (choo/faragha ), na isiyoonekana wakati wa kujisadia.

2. Kutoingia humo ndani yake na kitu ambacho ndani yake kuna utajo ( dhikri ) wa Allaah.

3. Kutanguliza mguu wa kushoto wakati wa kuingia humo.

4. Kusema – anapotaka kuingia - : **" Kwa jina la Allaah, Ewe Allaah, hakika mimi ninajilinda kwako kutokana na Mashetani wa kiume na Mashetani wa kike".**

5. Kutoinua (kutovua) nguo yake mpaka akaribie ardhini (tunduni)ili kusitiri utupu wake.

6. Asijisaidie haja kubwa au ndogo hali ya kuelekea Kibla au kukipa mgongo.

7. Asijisaidie haja kubwa au ndogo katika sehemu ya mapumziko ya watu, au njiani au katika maji yaliyotuama au chini ya mti wenye matunda.

8. Asiongee wakati wa kujisaidia.

Pili: Baada Ya Kujisaidia:

1. Asijisafishie mfupa au kinyesi cha wanyama, wala kitu chenye manufaa au kitu chenye heshima kama vile chakula n.k.

2. Asijisafishie kwa kutumia mkono wa kulia au kushika tupu yake kwa mkono huo.

3. Atumie jiwe au kinachosafisha- kama vile karatasi, kitambaa nk – kwa idadi ya witri (moja, tatu … ) mpaka uchafu uishe.

4. Ikiwa atatumia jiwe na maji, basi aanze kwa jiwe, kisha amalizie kwa maji.Na kama akitosheka na kimojawapo basi inafaa.

5. Wakati wa kutoka - chooni faraghani - atangulize mguu wake wa kulia.

6. Aseme - wakati wa kutoka -: “Naomba msamaha wako (Ewe Allaah)”.

Udhu

Kabla mtu hajaanza kuswali, ni wajibu juu yake kuwa msafi kutokana na uchafu mkubwa na mdogo. Na uchafu mkubwa huondoshwa kwa kuoga, na uchafu mdogo huondoshwa kwa udhu.

Kutayammamu huchukua nafasi ya udhu na kuoga katika kipindi cha dharura ya kukosekana kwa maji au kwa kuhofia madhara kwa kutumia maji.

**Maana Ya Udhu**:

Ni kutumia maji safi katika kusafisha viungo vinne : (Uso, mikono miwili, kichwa na miguu miwili), kwa namna maalumu iliyoelekezwa na Qur'an na Sunna.

**Dalili Yake** Kutoka Katika Qur'an :

Amesema Allaah mtukufu : {**Enyi Mlioamini! Mnaposimama kwa ajili ya Sala, basi osheni nyuso zenu na mikono yenu mpaka vifundoni, na mpake vichwa vyenu, na osheni miguu yenu mpaka vifundoni. Na mkiwa na janaba basi ogeni**}. [Al Maida: 6].

Na Katika Sunna :

Amesema Abu Hurayra Allaah amridhiye kuwa: Mtume Rehema na Amani zimshukie amesema: (Haikubaliki sala ya mtu yoyote anapojichafua mpaka atawadhe).[45]

Fadhila Za Udhu:

Hakika udhu una fadhila nyingi. Tutazitaja baadhi yake ili kubainisha fadhila zake.

Amesema Allaah mtukufu katika kubainisha fadhila zake: {**Allaah hapendi kukutieni katika taabu, bali anataka kukutakaseni na kutimiza neema yake juu yenu ili mpate kushukuru**}. [Al Maida: 6].

Ama dalili kutoka katika Sunnani nyingi sana, miongoni mwa hazo ni:

1. Kutoka kwa Abu Hurayra Allaah amridhiye amesema: Nilimsikia Mtume Rehema na Amani zimshukie akisema: (Hakika umati wangu wataitwa siku ya kiama hali ya kuwa wakiwa ni weupe waking'aa kutokana na athari ya udhu, basi atakayeweza miongoni mwenu kuz-

45- Imepokewa na Bukhari (135) na Muslim (225).

idisha mng'ao wake na afanye hivyo).[46]

2. Kutoka kwa Othman bin Affaan Allaah amridhiye amesema: Amesema Mtume Rehema na Amani zimshukie: (Yeyote atakayetawadha, na akafanya vizuri udhu wake, basi madhambi yake hutoka katika mwili wake mpaka chini ya kucha zake).[47]

3. Kutoka kwa Abu Hurayra Allaah amridhiye amesema: Amesema Mtume Rehema na Amani zimshukie: (Anapotawadha mja Mwislamu au Muumini akaosha uso wake, hutoka katika uso wake kila dhambi iliyoangaliwa na macho yake pamoja na maji au pamoja na tone la mwisho la maji, na anapoosha mikono yake, basi hutoka madhambi yote yaliyofanywa na mikono hiyo pamoja na maji au pamoja na tone la mwisho la maji, na anapoosha miguu yake, basi hutoka madhambi yake yote yaliyotembelewa na miguu hiyo pamoja na maji au pamoja na tone la mwisho la maji, mpaka anapomaliza huwa ni msafi kutokana na madhambi).[48]

46- Imepokewa na Bukhari (136) na Muslim (347).
47- Imepokewa na Muslim (245).
48- Imepokewa na Muslim (244).

4. Kutoka kwa Omar bin Khatwabi (Allaah amridhiye) amesema: Amesema Mtume Rehema na Amani zimshukie: (Hakuna yeyote miongoni mwenu anayetawadha, akaufanya vizuri udhu wake), kisha akasema baada yake: (Ninashuhudia kuwa hakuna Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ispokuwa Allaah peke yake asiye na mshirika, na ninashuhudia kuwa hakika Muhammad ni Mja wake na Mtume wake, ispokuwa mtu huyo hufunguliwa milango minane ya pepo, aingie kwenye mlango wowote autakao).[49]Na akaongezea Tirmidhiy kuwa : kisha akasema Mtu huyo: (Ewe Allaah ninakuomba unijaalie miongoni mwa wenye kutubu, na unijaalie miongoni mwa wenye kujisafisha).[50]

**Faradhi Za Udhu**:

Udhu una nguzo sita ambazo ni:

1. Kuosha uso mara moja tu, kuanzia juu ya paji la uso mpaka mwisho wa chini ya kidevu, na kuanzia kwenye sikio mpaka sikio lingine, kutokana na ushahidi wa kauli ya Allaah: {**Osheni nyuso zenu**}.[Al Maida: 6].

49- Imepokewa na Muslim (234).
50- Tirmidhiy (55). Lakini nyongeza hii Shekh Al Baaniy ameidhoofisha.

Na hapo inaingia katika hukumu ya uso kusukutua mdomo na kusafisha pua, kutokana na viungo hivyo kuzingatiwa ni katika uso, kama alivyosema Mtume Rehema na Amani zimshukie : (Anapotawadha mmoja wenu basi aweke mdomoni mwake maji kisha na ayapenge puani).[51]

2. Kuosha mikono miwili mpaka vifundoni, kwa ushahidi wa kauli ya Allaah: {**Na ( osheni ) mikono yenu mpaka vifundoni**}. [Al Maida: 6].

3. Kupaka maji kichwani kuanzia mwanzo wa paji la uso mpaka kisogoni, kwa ushahidi wa kauli ya Allaah: {**Na mpake vichwa vyenu**}. [Al Maida: 6].

4. Kuosha miguu miwili mpaka vifundoni, kwa ushahidi wa kauli ya Allaah: {**Na osheni miguu yenu mpaka vifundoni**}. [Al Maida: 6].

5. Utaratibu: Nao ni kwa kuanzia kuosha uso, kisha kuosha mikono miwili, kisha kupaka kichwa, kisha kuosha miguu miwili, kwa sababu ya kupatikana utaratibu huo katika amri ya Allaah.

---

51- Imepokewa na Muslim (237).

6. Kufululiza: Kwa maana kufanya matendo ya udhu kwa wakati mmoja bila kuachanisha kwa muda mrefu. Ispokuwa kama itakuwa hivyo kidogo tu haina madhara. Siyo kuachanisha kipindi kirefu mpaka kiungo kimoja kikauke maji.

**Sunna Za Udhu**:

1. Kupiga mswaki.

2. Kuanza kwa kusema **"Bismi LLah"** (Kwa jina la Allaah).

3. Kuanza udhu kwa kuosha viganja viwili mara tatu. Lakini ikiwa mtu ametoka kulala, anawajibika kuviosha viganja vyake kwanza mara tatu kabla ya kuviingiza katika maji ya udhu, kama alivyosema Mtume Rehema na Amani zimshukie: (Atakapoamka mmoja wenu usingizini basi aoshe viganja vyake mara tatu kabla ya kuviingiza katika chombo, kwani yeye hajui mikono yake ililala maeneo gani).[52]

---

52- Imepokewa na Bukhari (162) na Muslim (278). Na ameitoa Imamu Malik, Vol. 1, Uk. 21.

4. Kuanza kusukutua mdomoni na kupenga maji puani kabla ya kuosha uso pamoja na kupandisha sana maji mdomoni kwa asiyekuwa Mfungaji.

5. Kuesua ndevu nyingi ili maji yaingie ndani yake.

6. Kuanza upande wa kulia, kwa kuosha viungo vya kulia kwanza kisha vya kushoto.

7. Kuomba dua baada ya kumaliza udhu.

8. Kuswali rakaa mbili baada ya udhu, inaitwa Sunna ya udhu.

**Yasiyo Pendeza (Yasiyofaa) Katika Udhu**:

1. Kutawadha katika sehemu yenye najisi ili kuepusha isimrukie.

2. Kuzidisha zaidi ya mara tatu katika kutawadha.

3. Kufanya uharibifu wa maji (israfu).

4. Kuacha sunna moja au zaidi, miongoni mwa sunna za udhu, kwa sababu hapati malipo.

5. Kutawadha maji yaliyoachwa na Mwanamke (Yale maji aliyokwishatawadhia yakabakia katika chombo).

**Namna Ya Kutawadha**:

Udhu una namna mbili:

Ya Kwanza: Udhu unaotosheleza:

Nao ni kuanza kwa nia, kisha kusema: **"Bismi LLah",** kisha kusukutua na kupenga maji puani, kisha kuosha uso, kisha kuosha mikono miwili mpaka vifundoni, kisha kupaka kichwa pamoja na masikio, kisha kuosha miguuni mpaka vifundoni.

Kuosha viungo vyote hivi mara moja moja tu.Namna hii inatosheleza na udhu ni sahihi.

**Ya Pili: Udhu ulio kamili**:

Nao ni kuanza kwa nia, kisha kusema: **"Bismi LLah",**na kuosha viganja viwili mara tatu, kisha kusukutua mdomoni na kupenga maji puani mara tatu kwa michoto mitatu, kisha kuosha uso mara tatu, kisha kuosha mkono wa kulia mpaka kifundoni mara tatu, kisha kuosha mkono wa kushoto mpaka kifundoni mara tatu, kisha kupaka kichwani mara moja kuanzia mwanzo wa kichwa mpaka

kisogoni na kurudishia mpaka mwanzoni mwa kichwa tena na kuingiza vidole vyake ndani ya matundu ya masikio kwa vidole gumba nje yake na vidole shahada ndani yake, kisha kuosha mguu wa kulia pamoja na muundi mara tatu, kisha kuosha mguu wa kushoto pamoja na muundi mara tatu.Kisha akimaliza hivyo vyote aseme: “Ninashuhdia kuwa hakuna Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ispokuwa Allaah peke yake asiye na mshirika, na ninashuhudia kuwa hakika Muhammad ni Mja wake na Mtume wake”.

**Vitenguzi Vya Udhu**:

1. Kila kitokacho katika njia mbili (mbele na nyuma) kama vile mkojo, kinyesi na ushuzi.

2. Kuondokwa na akili kwa kuzimia, kulewa au uwendawazimu.

3. Kulala usingizi mzito usiojitambua.

4. Kugusa kushika utupu kwa matamanio kwa viganja vya mikono na vidole.

5. Kuritadi (Kuukana) Uislamu.

6. Kula nyama ya ngamia.

7. Kugusana Mwanaume na Mwanamke kwa matamanio.

**Tanbiihi: Mambo Muhimu Yanayo Paswa Kuyataja**:

**Jambo la Kwanza:** Mtu yoyote atakayekuwa na yakini ya kuwa msafi, kisha ikamuingia shaka juu ya kutenguka udhu, basi atatakiwa kuijengea yakini yake kuwa ni Msafi.

**Jambo la pili:** Mwenye kuwa na yakini ya kutenguka udhu, kisha akawa na mashaka juu ya usafi wake, atawajibika kujengea yakini ya kutokuwa safi na atajisafisha upya.

**Jambo la tatu:** Mkojo na kinyesi cha mnyama anayeliwa nyama yake , pia na manii ya Mwanadam ni safi (si najisi).

**Jambo la nne:** Mtu akiwa na mashaka ya usafi wa maji au kuwa yana najisi, basi atawajibika kuijengea yakini yake, na asili ya vitu ni usafi.

**Jambo la tano:** Ikiwa maji safi na maji najsi yatamchanganya mtu, ikawa hajui ni yapi yaliyo safi, basi

atalazimika kujitahidi katika kuyatambua, kisha ndipo atawadhe.

Kupaka Juu Ya Khof Mbili

Kwanza: Maana ya Khof mbili:

Ni vitu vinavyovaliwa miguuni vinavyotokana na ngozi au mfano wake kama katani, sufi n.k.

Pili: **Dalili ya kisheria juu uwajibu wa kupaka juu ya khof mbili**:

Zimekuja dalili nyingi sana katika Sunna zikibainisha jambo hili.Miongoni mwa hizo ni :

Amesimulia Abdullaah bin Omar kutoka kwa Sa'ad bin Abi Waqqaaswi Allaah awaridhiye kuwa Mtume Rehema na Amani zimshukie alikuwa akipaka juu ya khof mbili. Abdullaah bin Omar Allaah amridhiye naye alikuwa akiulizwa anasema: Ndiyo, ni kweli jambo hilo, kwani Sa'ad bin Abi Waqqaaswi Allaah awaridhiye akikuelezea jambo kutoka kwa Mtume Rehema na Amani zimshukie,

basi usimuulize mtu mwingine.[53]

Na amesema Amru bin Umayat Adhwamariyyu : Nilimuona Mtume Rehema na Amani zimshukie akipaka juu ya kilemba na khof zake.[54]

Na amesimulia Mughira bin Shuuba Allaah amridhiye kuwa aliambiwa na Mtume Rehema na Amani zimshukie - alipotaka kumvua khof zake ili atawadhe: (Ziache, kwani mimi nilizivaa wakati nikiwa twahara), kisha akapaka juu yake.[55]

Tatu : **Masharti ya kuswihi kupaka juu ya khof mbili** :

1. Kuzivaa hali ya kuwa tayari umo katika usafi (twahara), kutokana na hadithi ya Ur'wa bin Mughiira kutoka kwa baba yake, aliyesema: Nilikuwa na Mtume Rehema na Amani zimshukie safarini, nikaharakia kumvua khof zake ili atawadhe, akasema: (Ziache, kwani mimi nilizivaa wakati nikiwa twahara).[56]

---

53_ Imepokewa na Bukhari (202).
54_ Imepokewa na Bukhari (204).
55_ IMEPOKEWA NA BUKHARI (206) NA MUSLIM (274).
56_ kisha akapaka juu yake. Imepokewa na Bukhari (206) na Muslim (274).

2. Khof au soksi ziwe safi, ikiwa zitakuwa na najisi, basi haijuzu.

3. Ziwe zinasitiri sehemu ya lazima kupakwa.

Nne: **Muda wa Kupaka**:

Kwa mwenyeji ni mchana na usiku, na kwa msafiri ni michana mitatu na mausiku yake. Na hesabu ya kupaka inaanzia pale mtu anapoanza kupaka kwa mara ya kwanza (kwa kauli iliyo sahihi).

Tano: **Namna ya kupaka**:

Ni kuingiza mikono kwenye maji na kupaka juu ya khof kuanzia kwenye vidole vyake vya miguuni mpaka kwenye muundi mara moja tu, siyo kupaka chini yake au kwenye kisigino.

Sita: **Vitenguzi vya kupaka**:

1. Khof mbili zikivuliwa miguuni.

2. Ikitokea ulazima wa kuoga janaba.

3. Muda wa kupaka ukitimia.

Kuoga

**Vinavyo Wajibisha Kuoga**:

**1. Janaba**: Na inakusanywa jimai kukutana tupu mbili hata bila kushusha manii, pia na kushusha manii kwa mchupo wa ladha usingizini au kawaida, kwa mwanaume au mwanamke, kutokana na kauli ya Allaah: {**Na mkiwa na janaba basi ogeni**}. [Al Maida: 6]. Na Mtume Rehema na zimshukie amesema: (Zinapokutana tupu mbili, basi imewajibika kuoga).[57]

**2. Kukatika Kwa Damu Ya Hedhi Au Nifasi:**Kwa kauli ya Allaah mtukufu: {**Basi jitengeni na wanawake wakati wa hedhi.Wala msiwaingilie mpaka watwaharike, wakishatwaharika basi waendeeni alivyo kuamrisheni Allaah**}. [Al Baqara: 222]. Naye Mtume Rehema na Amani zimshukie alimwambia mmoja wa wanawake kuwa: (Jizuwie kusali kiasi cha unavyojizuia kipindi cha hedhi yako, kisha uoge).[58]

**Namna Ya Kuoga**:

---

57_ Imepokewa na Ahmad (26067) na Ibnu Maajah (608).
58_ Imepokewa na Muslim (785).

Kuna namna mbili za kuoga:

**Kwanza: Kuoga kwa ukamilifu;** nako ni kuanza kwa kusema: **"Bismi LLah",** hali ya kukusudia kuondoa uchafu mkubwa (Janaba, hedhi na nifasi) kwa kuoga huko, kisha kuosha viganja viwili mara tatu, kisha kustanji kwa kusafisha tupu na maeneo ya pembezoni mwake, kisha kutawadha ispokuwa miguu miwili, kwani ana khiyari ya kuiosha na udhu huo au kuichelewesha mpaka mwisho wa josho lake, kisha kujimwagia maji kuanzia kichwani pamoja na masikioni mara tatu kwa michoto mitatu, kisha kujimwagia maji kwa kuanzia upande wa kulia kuanzia juu mpaka chini, kisha upande wa kushoto hivyo hivyo, hali ya kufauatilia kwa kuosha sehemu zilizojikunja mwilini kama vile kitovuni, makwapani na magotini n.k.

**Pili: Kuoga kunakotosheleza:** nako kunakuwa kwa kujimwagia maji mwili wote pamoja na kusukutua na kupenga puani mara moja tu.

**Kutayammamu**:

**Kwanza: K**utayammamu ni katika mambo maalumu ya Umma huu wa kiislamu, na ni badala ya kutumia maji.

**Na maana yake ni**: Kumuabudu Allaah mtukufu kwa kukusudia kuutumia udongo safi kwa kupaka uso na viganja viwili.

Pili: Je muda wake wa kisheria ni upi?

Kutayammamu kunalazimika katika hali zifuatazo :

1. Maji yanapokosekana kabisa.

2. Ikiwa mtu ana jeraha mwilini, au ugonjwa au akahofia kudhurika kama atatumia maji.

3. Ikiwa maji yana baridi kali inayodhuru, na ikashindikana kuyachemsha na kuhofia kudhurika.

4. Ikiwa maji yatahitajika kwa kunywa au kunywesha vitu vingine kwa kuhofia kiu kikali chenye kuleta mauaji.

Tatu: **Vitenguzi vyake**:

1. Kupatikana (Kuwepo) kwa maji.

2. Kupatikana kitenguzi kimojawapo miongoni mwa vitenguzi vya udhu.

Nne: **Namna yake**:

Ni Kunuia, kisha kusema: **"Bismi LLah",**na kupiga udongo (mchanga) mara moja kwa matumbo ya viganja kisha kupaka kwenye uso na juu ya viganja viwili.

HedhiNa Nifasi Na Istihadhwa:

**Kwanza:Maana Ya Hedhi:** Ni damu inayotoka katika mfuko wa uzazi kuanzia kipindi cha balaeghe ya Mwanamke, na kutoka katika utupu katika kipindi maalumu. Uchache wake ni mchana na usiku tu, na wingi wake ni siku kumi na tano.

**Pili:Maana Ya Nifasi:** Ni damu inayotoka katika utupu wa Mwanamke kwa sababu ya kuzaa,na haina ukomo wa uchache wake, muda wowote Mwanamke (Mzazi)

akiona ukavu, atawajibika kuoga na kuanza kuswali. Na wingi wake ni siku arobaini.

**Tatu: Maana Ya Istihadha:** Ni damu ambayo inayomtoka Mwanamke katika utupu wake na haina mwisho wa kukatika kwa sababu ya ugonjwa.

Nne: Baadhi ya Hukumu za Wenye Hedhi na Nifasi:

1. Ni haramu kufanya tendo la ndoa (Jimai), kama alivyosema Allaah mtukufu: {**Wala msiwaingilie mpaka watwaharike**}. [Al Baqara: 222].

2. Ni haramu kwao kuswali na kufunga, ispokuwa funga tu ndiyo watalipa, ama swala hawalipi.

3. Ni haramu kwao Kuzunguka (kutufu) Alkaaba mpaka watakapotwaharika na kuoga.

4. Hairuhusiwi kwao kuushika msahafu ispokuwa wakiwa wameweka juu yake kizuizi cha gloves n.k.

Tano: Hali za mwenye Istihadhwa:

1. Ikiwa muda wake wa hedhi anaujua, basi atawajibika

kujizuwia kuswali na kufunga kwa muda huo, kisha ataoga na kuendelea kuswali na kufunga.

2. Ikiwa muda wake wa hedhi haujui, na hafahamu kabisa, basi atawajibika kujizuwia kuswali na kufunga kwa muda wa kawaida wa wanawake walio karibu yake. Ikiwa hana wanawake wa karibu naye, basi atawajibika kujizuwia aghalabu ya muda wa hedhi ambao ni siku sita au saba tu.

3. Ikiwa hana ada, lakini anao ubainifu (ujuzi) wa kujua damu ya hedhi kuwa ni nyeusi tofauti na damu nyingine, basi atawajibika kufatilia hivyo na kujizuia kipindi cha damu hiyo nyeusi (hedhi) na ikiondoka hali hiyo, basi ataoga na kuendelea na swala nk.

Sita: Baadhi ya hukumu za Mwenye Istihadhwa:

Mwenye Istihadhwa anatakiwa aoge, afunge na kuswali.Ispokuwa anawajibika kutawadha kwa kila swala.Na Mume wake anaruhusiwa kumuingilia. Kwa ujumla anaruhusiwa kufanya mambo yote aliyokatazwa kuyafanya wakati wa hedhi.

Swala

**Maana Ya Swala:** Swala katika lugha ya kiarabu ina maana ya dua (Maombi).

Na katika sheria: Ni ibada yenye maneno na matendo maalumu, inayofunguliwa kwa takbira (Allaahu Akbaru) na kumaliziwa kwa salamu (Assalaamu alaykum).

Nafasi ya swala katika Uislamu:

Swala ni kiunganishi kati ya Mja na Mola wake.Ndani yake Mja huonesha utiifu, mapenzi na unyenyekevu wake na kujisalimisha kwake.Nayo ni nguzo kubwa baada ya Shahada mbili katika nguzo za Uislamu, kwa sababu ndiyo msingi wa dini na nuru ya yakini.Ndani yake kuna usafi wa nafsi, na kufunguka kifua na utulivu wa moyo. Nayo ndiyo kizuwizi kikubwa cha kutofanya maovu na ni sababu ya kufutiwa madhambi.

Hukumu ya Mwenye kuiacha swala:

Ikiwa mtu atapinga uwajibu wake bila ya udhuru wa kisheria, basi huyo ni Kafiri, hata kama ataifanya kwa kukemewa kwake, kwa kuwa anakuwa amefanya jambo

kubwa la haramu ambalo katika dini halina mjadala, na pia ni kuonesha wazi wazi kumpinga Allaah na Mtume wake.Na mtu huyo huuwawa, kwa kauli ya Mtume Rehema na Amani zimshukie: (Yeyote atakayebadili dini yake (atakayeritadi) basi Muuweni).[59]Hivyo basi Mtu wa namna hiyo, hufanyiwa hukumu ya aliyeritadi katika Uislamu.

Na ikiwa anaamini uwajibu wake, lakini akaacha kwa uvivu mpaka muda wake ukaisha, basi katika hali kama hii, kuna Ikhtilafu ya Wanazuoni juu ya hukumu yake. Wapo waliosema: Huyo ni Kafiri na ameukana Uislamu, na inatakiwa auwawe ikiwa hatoonesha kutubu juu ya kosa hilo. Na wengine wakasema: Huyo ni Mtu muovu, hivyo atalinganiwa na atubie.Ikiwa hatotubu basi ndipo atauwawa kwa mujibu wa sheria ilivyoelekeza. Na wengine wakasema: Siyo Kafiri wala hauwawi, bali atapewa adhabu ya kutiwa adabu na kufungwa mpaka aswali au afie jela kifungo cha maisha.

Nguzo za Swala:

Nguzo za swala ambazo haitoswihi ispokuwa kwa kuzitekeleza, zipo kumi na nne:

59_ IMEPOKEWA NA BUKHARI (6922).

1. Kusimama pamoja na kuweza.

2. Takbira ya kuhirimia ( Mwanzo ).

3. Kusoma suratul Faatihat.

4. Kurukuu.

5. Kuitidali ( kulingana kutoka ) katika rukuu.

6. Kusujudu juu ya viungo saba ( Uso, viganja viwili, magoti mawili na ncha za miguu miwili ).

7. Kuitidali ( kulingana kutoka ) katika sijda.

8. Kukaa kati ya sijda mbili.

9. Kutulia katika kila nguzo.

10. Tashahudi ya mwisho.

11. Kukaa kwa ajili ya tashahudi ya mwisho.

12. Kumtakia rehma na amani Mtume Rehema na Amani zimshukie katika tashahudi ya mwisho.

13. Kufuata utaratibu katika nguzo hizi.

14. Kutoa salamu.

Masharti ya Swala:

Masharti ya swala yapo tisa:

1. Uislamu. Haikubaliwi swala ya kafiri, japokuwa atahesabiwa kwa kutoitekeleza kwa mujibu wa kauli sahihi.

2. Kuwa na akili. Asiye na akili si mwenye kuwajibika kisheria.

3. Kuwa mpambanuzi.

4. Kuingia wakati wake.

5. Kutwaharika na uchafu.

6. Kuepukana na najisi.

7. Kusitiri utupu.

8. Kuelekea Kibla.

9. Kuwa na nia.

Mambo Ya Wajibu Katika Swala:

**Wajibu:** Ni jambo lililoamrishwa kisheria kwa hali ya lazima, swala hubatilika kwa kuacha wajibu kwa kukusudia, na na kama ataiacha kwa kusahau atasujudu sijida mbili za kusahau.

Na mambo ya wajibu katika swala yapo manane:

1. Takbira zote ispokuwa takbira ya kuhirimia.

2. Kusema: “Samia LLaahu liman hamidahu”.

3. Kusema: “Rabbanaa walakal hamdu”.

4. Kusema: “Subhaana Rabbiyal adhwiim” katika rukuu.

5. Kusema: “Subhaana Rabbiyal a’alaa” katika sijda.

6. Kumuomba msamaha Allaah (Rabbighfir liy)kati ya sijda mbili.

7. Tashahudi ya kwanza.

8. Kukaa kwa ajili ya tahiyyaatu ya kwanza.

Sunna za Swala:

Tunakusudia matendo ya kisheria ambayo hayabatilishi swala kwa kuyaacha kwa makusudi au kwa kusahau.

Na sunna za swala zipo nyingi, miongoni mwa hizo ni:

1. Kuinua mikono miwili wakati wa takbira ya kuhirimia.

2. Kuinua mikono miwili wakati wa kurukuu.

3. Kuinua mikono miwili wakati wa kuinuka kutoka katika rukuu.

4. Kuweka kiganja cha mkono wa kulia juu ya kiganja cha kushoto juu ya kifua wakati wa kusimama.

5. Kuangalia tu sehemu ya kusujudia muda wote (ispokuwa wakati wa tashahudi kuangalia katika kidole shahada).

6. Kusoma dua ya ufunguzi wa swala.

7. Kujikinga kutokana na Shetani (Kwa kusema kwa siri: Audhu billahi minash shaytwanir Rajiim) kabla ya kusoma surat Faatihat. n.k.

Swala Ya Jamaa:

Fadhila zake:

Zimepatikana dalili nyingi katika kubainisha fadhila za swala ya jamaa.Miongoni mwa hizo ni:

1. Amesimulia Abdullaah bin Omar Allaah amridhiye kuwa: Mtume Rehema na Amani zimshukie amesema: (Swala ya jamaa (pamoja) ni bora kuliko ya mtu mmoja kwa daraja ishirini na saba).[60]

2. Amesimulia Abu Hurayra Allaah amridhiye kuwa: Mtume Rehema na Amani zimshukie amesema: (Swala ya mtu anapoiswali katika jamaa huzidi swala ya nyumbani kwake na ya sokoni kwake kwa zaidi ya daraja ishirini na tano).[61]

3. Amesimulia Abu Hurayra Allaah amridhiye kuwa: Alikuja mtu mmoja kipofu akasema: ewe Mjumbe wa Allaah, mimi sina mtu wa kuniongoza kuja msikitini, akamuomba Mtume Rehema na Amani zimshukie ruhusa ili aswalie nyumbani kwake. Mtume Rehema na Amani zimshukie akamruhusu. Alipoanza kuondoka tu, akamuita na kumuuliza: (Je huwa unaisikia Adhana ya Swa-

60- Imepokewa na Bukhari (645) na Muslim (249).
61- Imepokewa na Bukhari (647).

la?), akasema: Ndiyo. Basi Mtume Rehema na Amani zimshukie akamwambia: (Unawajibika kuiitikia - kuja kuswalia Msikitini-). [62]

Hukumu yake:

Swala ya jamaa ni lazima juu ya kila Mwanaume katika kipindi cha kuwepo au cha safari, kwa ushahidi wa kauli ya Allaah Mtukufu : {**Na unapokuwa pamoja nao, ukawasalisha, basi kundi moja miongoni mwao wasimame pamoja nawe**}. [Nisaa: 102].

Amesema katika kitabu cha sherehe ya Al Muntaha: "Na amri hiyo ni ya wajibu (lazima). Ikiwa amri hiyo ilikuja katika kipindi cha hofu, basi katika kipindi cha utulivu inakuwa ni lazima zaidi", pia na kwa ushahidi wa hadithi iliyosimuliwa na Abu Hurayra Allaah amridhiye kuwa Mtume Rehema na Amani zimshukie amesema: (Swala nzito kwa wanafiki ni swala ya Ishai na swala ya Alfajri.Na lau wangejua (malipo) yaliyomo ndani yake basi wangeziendea kwa kusota kwa magoti yao, na nimekusudia niamrishe ikimiwe swala, kisha nimuamrishe mtu awaswalishe watu, kisha Mimi nitoke pamoja na watu

62_ Imepokewa na Muslim (653).

wengine wakiwa na mizigo ya kuni ili tukazichome moto nyumba za watu ambao hawahudhurii swala ya jamaa).[63]

Vile vile tunapata ushahidi wa uwajibu wa swala ya jamaa kutokana na kauli ya Mtume Rehema na Amani zimshukie alipomwambia yule kipofu aliyemuomba ruhusa ya kuswalia nyumbani kwake: (Je unaisikia adhana?), akasema: Ndiyo. Akamwambia: (Unawajibika kuiitikia - kuja kuswalia Msikitini).[64]

Idadi Inayotakiwa Ili Kukubalika Jamaa:

Swala ya jamaa inathibiti kwa kuanzia na watu wawili tu : Imamu na Maamuma, hata kama akiwa Mwanamke, Kutokana na kauli ya Mtume Rehema na Amani zimshukie alipomwambia Maliki bin Al Huwayrithi: (Na awaswalisheni nyie - mlio wawili - mkubwa wenu).[65]

Nyudhuru Zinazo Ruhusiwa Kuacha Swala Ya Jamaa:

Mwenye hofu ya kutokewa na ugonjwa, na Mwenye kubanwa na haja mbili (kubwa na ndogo), na Mwenye kupotelewa na kitu anachotarajia kukipata kwa kukitafuta,

63_ IMEPOKEWA NA BUKHARI (644) NA MUSLIM (651).

64_ Imepokewa na Muslim (653).

65_ Imepokewa na Bukhari (631)، na Muslim (674).

au ana hofu ya kupotelewa mali yake, au kutoweka, au kupatikana madhara ndani yake, au akawa na hofu na mali iliyokodiwa ulinzi wake.[66]

Baadhi Ya HukumuZinazo Ambatana Na Maamuma:

1. Ni haramu kuswalisha kwenye msikiti wenye Imamu maalumu ispokuwa kwa idhini yake ikiwa muda si mfinyu.[67]

2. Inapokimiwa swala ya faradhi, hairuhusiwi kuanza swala nyingine ya sunna, kutokana na kauli ya Mtume Rehema na Amani zimshukie: (Inapokimiwa swala, basi hairuhusiwi swala yoyote ispokuwa swala ya faradhi tu iliyokimiwa muda huo).[68]

3. Ni haramu kwa Maamuma kurukuu au kusujudu kabla ya Imamu wake. Na ikiwa atafanya hivyo, basi ni lazima arudie swala. Na yoyote atakayemtangulia Imamu wake kwa kitendo miongoni mwa matendo ya swala, basi anapata dhambi, ispokuwa tu akiwa mjinga (hajui) au amesahau.[69]

66- Rejea: Al Mugh'niy: 283|.
67- "Sharhul Muntahala" Vol. 11، Uk. 257.
68- Imepokewa na Muslim (710).
69- "Mukh'taswarul Fiqhil Islamiy" Uk. 63.

4. Haikubaliki swala ya Maamuma mmoja nyuma ya swafu peke yake, ispokuwa ikiwa swafu imekamilika na hakuna nafasi, kutokana na kauli ya Mtume Rehema na Amani ya Allaah zimshukie: (Hakuna swala ya mtu mmoja nyuma ya swafu).[70]

Baadhi YaHukumu Zinazo Ambatana Na Imamu:

1. Mwenye haki ya kuwa Imamu ni anayejua kusoma vizuri Qur'an, kisha Mjuzi wa Sunna, kisha aliyetangulia kuhama, kisha aliyetangulia katika Uislamu, kisha aliye na umri mkubwa.[71]

2. Ni sunna kwa Imamu kukhafifisha katika swala yake kutokana na kuchunga hali za wagonjwa, wazee na wenye haja (matatizo ) mbali mbali.

Swala Ya Mgonjwa:

1. Ni lazima mgonjwa aswali swala ya faradhi hali ya kuwa amesimama, hata kwa kuegemea ukuta au fimbo. Ikiwa atashindwa, basi aswali hali ya kukaa. Na ni vizuri kwake anaposwali hali ya kukaa aswali kwa mkao

70- IMEPOKEWA NA IBNU MAAJAH (1003) NA AMEISAHIHISHA AL ALBAANIY KATIKA AL IR'WAAU (541).
71- "Al Mugh'niy" Vol. 2, Uk. 700.

wa **Tarabbui**, ikiwa atashindwa basi alalie ubavu, ikiwa atashindwa basi ataswali kwa hali anayoiweza yeye Mwenyewe hata kama kwa kulalia mgongo wake, kutokna na Kauli ya Allaah: {**Basi mcheni Mwenyezi Mungu kama mwezavyo**}.[Taghaabun: 16]. Na kwa kauli yake Allaah: {**Mwenyezi Mungu haikalifishi nafsi yoyote ila kwa kadiri ya iwezavyo**}. [Al Baqara: 286]. Na ikiwa atashindwa kabisa (hali zote hizo), basi ataashiria kwa kichwa chake, na akishindwa kabisa basi ataashiria kwa macho yake na kutia nia moyoni.[72]

2. Ikiwa mgonjwa atashindwa kuswali kila swala kwa wakati wake, basi anaruhusiwa kukusanya kati ya swala mbili na kuziswali kwa wakati mmoja wapo.Anaweza kukusanya Swala ya adhuhuri na alasiri, au Maghribi na ishai na kuziswali katika moja wapo ya nyakati zake. Na kilicho bora kwake ni kufanya lililo jepesi kwake katika kutanguliza au kuchelewesha.

3. Ikiwa mgonjwa atashindwa kutawadha, basi inaruhusiwa mtu mwingine kumtawadhisha. Na ikiwa yupo sehemu ambayo haina maji wala mchanga, wala mtu wa

72_ "Al Mugh'niy" Vol. 1، Uk. 813.

kumletea maji au mchanga hakuna, basi ataswali kwa mujibu wa hali aliyopo, na hatakiwi kuicheleweshaswala.[73]

4. Ni wajibu wa mgonjwa kuelekea kibla kwa hali atakayoweza, hata kama ni kuelekea kwa uso wake na miguu yake.Ikiwa atashindwa, basi ataswali kwa mujibu wa hali aliyo nayo.

Swala Ya Ijumaa

Hukumu yake:

Swala ya Ijumaa ni wajibu (Lazima). Na uwajibu huu umethibitshwa na Qur'an, Sunna na Ijmaai (Makubaliano ya Wanazuoni). Nayo ni nguzo ya lazima. Na swala ya adhuhuri huwa badala yake katika kipindi cha mtu anapopitwa na swala ya Ijumaa kwa udhuru wa kisheria.[74]

Je Swala Ya Ijumaa Ni Wajibu Juu Ya Nani?

Swala ya Ijumaa inawajibika kwa masharti manane :

1- Kuwa mwislamu.

2- Kubaleghe.

73_ Maneno hayo ameyaeleza Imamu Ibn Baazi katika Fat'wa yake.
74_ "Kitaabu Swalah" Uk. 206.

3- Kuwa na akili timamu.

4- Kuwa mwanaume.

5- Kuwa huru.

6- Kuwa mkazi.

7- Kutokuwa na nyudhuru za kutohudhuria jamaa.

8- Kuwa mkazi wa sehemu inayopatikana swala ya Ijumaa au kuwa karibu nayo.[75]

Hekima Ya Kuamrishwa Kuswali Ijumaa:

Allaah amewawekea sheria waja wake ya swala ya Ijumaa ili kuwazindua kutokana na ukubwa wa kuzikumbuka neema zake juu yao.Na akawawekea sheria ya Hotuba ndani yake kutokana na yanayokusanywa ndani yake katika ukumbusho wa neema hiyo, na kuwasisitiza juu ya kumshukuru yeye kwa neema zake.

Na katika swala ya Ijumaa kuna mafundisho mengi, maelekezo, mawaidha, ukumbusho, na msisitizo wa kuikumbuka ahadi ya kukutana pamoja na Allaah, na kuhuisha hisia za undugu, na kusisitiza mshikamano na kuon-

75- "Kitaabu Swalah" Uk. 207.

esha nguvu ya Umma wa kiislamu.[76]

Masharti Ya Kukubalika Swala Ya Ijumaa:

1- Kuingia wakati. Haikubaliki swala ya Ijumaa kabla ya wakati wake au baada yake , na haya ni makubaliano ya Wanazuoni wote.

2- Kuwepo jamaa. Hairuhusiwi Swala ya Ijumaa ya mtu mmoja.

3- Kuwa mkazi.

4- Kutanguliwa swala ya Ijumaa na khutba mbili.

Swala Za Iddi Mbili

Hukumu yake:

Wanazuoni wamekhitalifiana juu ya hukumu ya swala za idi mbili (Eidul Fitri na Eidul Adh'ha), baada ya kukubaliana kwao juu ya kuwa imo ndani ya sheria. Baadhi yao wakawa na mtazamo kuwa ni Faradhi ya kutoshelezana, na wengine wakawa na mtazamo kuwa ni Sunna iliyosisitizwa sana. Na kila kundi likawa na dalili zake ambazo

---

76- "Al Ibaadah Fil Islaami" cha Shekh Qardhwaawi, Uk. 223.

zimeelezwa ndani ya vitabu vya Fiqhi.[77]

Muda Wake:

Wanazuoni wameafikiana kuwa muda wake huanzia baada ya kuchomoza jua kiasi cha mkuki mpaka kupinduka kwake. Ni haramu kuswaliwa katika muda tu linapochomoza jua, na haipendezi ispokuwa mpaka liinuke kiasi cha mkuki.[78]

Sehemu Ya Kuswaliwa Idd:

Sunna ni kuiswali nje ya mji. Na hivyo alifanya Mtume Rehema na Amani zimshukie, na hufanywa hivyo ikiwa hakuna sababu zozote zinazozuwia kuswalia kwenye maeneo ya wazi (Viwanjani).[79]

77_ "Kitaabu Swalah" Uk. 331.
78_ "Al Mawaaidhwul Hasanah" cha Swiddiiq Hssan Khaan, Uk. 4344_.
79_ "AL MUGH'NIY" VOL. 3, UK. 260.

Namna Yake:

Swala ya idi ni rakaa mbili tu.Huanzwa kwa takbira ya kuhirimia kama swala zingine. Kisha hutolewa takbira sita baada yake, kisha husomwa surat Al Faatiha na Surat Al Aa'alaa au Surat Qaaf, akishamaliza kusoma hutoa takbira na kurukuu, kisha atakapokamilisha rakaa ya kwanza na kusimama kwa kutoa takbira kutoka katika sijda, atapiga takbira tano mfululizo. Akishamaliza takbira ataanza kusoma Surat Al Faatiha na Surat Ghaashiya, au Surat Al Qamar.

Ispokuwa kama atasoma katika rakaa ya mwanzo Surat Al Aa'alaa, basi katika rakaa ya pili atasoma Surat Ghaashiya. Na ikiwa katika rakaa ya mwanzo atasoma Surat Qaaf, basi katika rakaa ya pili atasoma surat Al Qamar.[80]

Swala Ya Kupatwa Kwa Jua Na Mwezi:

Kupatwa kwa jua na mwezi ni miongoni mwa alama kubwa miongoni mwa alama za Allaah mtukufu ambazo huwahofisha waja wake ili wajiangalie (wajichunguze) na kutubu kwake. Na matukio hayo ni mojawapo ya

80- Rejea: Zaadul Maadi: 1444 - 442\ ).

kuonekana kwa uwezo wa Allaah, Muumbaji aliyetukuka.

Na ifahamike kuwa kupatwa kwa jua na mwezi hakutokei kwa sababu ya uhai wa mtu au kifo chake, bali hutokea kwa sababu ya madhambi yanayofanywa na watu, hivyo Allaah huleta kuwahofisha waja wake watubu madhambi yao.

Namna yake:

Hutangazwa kwa ajili ya swala hiyo usiku au mchana kwa kusema (**SwalaatulJaamia**), kwa maana ya: “Njooni kwenye Swala ya mkusanyiko wa pamoja”.

Kisha imamu huanza kwa Takbira, na kusoma Surat Faatiha na sura ndefu kwa kisomo cha wazi, kisha atarukuu rukuu ndefu, kisha atainuka kutoka katika rukuu na kusoma tena Surat Faatiha na sura ndefu kuliko ya kwanza, kisha atarukuu rukuu ndefu kidogo kuliko ya kwanza, kisha atainuka na kwenda kusujudu sijda mbili ndefu ikitofautiana ya kwanza na ya pili.

Kisha atainuka kusimama kwenye rakaa ya pili na ku-

fanya kama katika rakaa ya kwanza ispokuwa atapunguza kisomo kuliko cha mwanzo.[81]

Swala Ya Kuomba Mvua

Allaah mtukufu amewawekea sheria waja wake waumini, katika hali ya ukame wa ardhi na kukosekana kwa mvua, wamuelekee yeye kwa kunyenyekea na kumuomba msaada wa kunyeshewa mvua.Na jambo hilo linatakiwa lifanyike kwa swala maalumu kwa jamaa (pamoja) au mmoja mmoja.Au wamuombe tu kwa dua katika hotuba ya Ijumaa.Kwa kufanya hivyo, kutadhihirisha unyonge wa wanadamu kwa Mola wao na mahitaji yao kwake.Amesema Allaah mtukufu: {**Enyi watu! Nyinyi ndiyo wenye haja ( shida ) kwa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kujitosha, Msifiwa**}. [Faatwir: 15].

Hukumu Yake:

Ni Sunna iliyosisitizwa sana na iliyothibiti kwa kufanywa na Mtume Rehema na Amani zimshukie, pamoja na Makhalifa wake waongofu.Vile vile Wanazuoni wote wameafikiana juu ya kuwa imo ndani ya sheria.[82]

81_ Rejea: Mukk'taswari wa Kitabu cha Fiqhul Islaamiy: Ukurasa wa 65.
82_ "Kitaabu Swalah" Uk. 354.

Namna Yake:

Swala ya kuomba mvua ni kama swala ya idi mbili, kwa kuwa ina rakaa mbili, na huswaliwa kwa kudhihirisha kisomo chake katika viwanja, na vile vile huswaliwa kabla ya hotuba ya Imaamu, n.k.

Swala Za Sunna:

Miongoni mwa hekima za Allaah mtukufu na rehma zake kwa waja wake, ni kuwawekea sheria ya swala za sunna.Na amejaalia kila ibada ina sunna zake katika jinsi yake, ili ziwe ni zenye kuziba upungufu uliopatiikana katika faradhi zake.

Na swala za sunna si lazima kwa mja kuzifanya, bali ni nyongeza katika kheri zake.

Na swala za sunna zimegawanyika katika sehemu kuu mbili:

1. Swala za Sunna zilizo tiliwa mkazo.

2. Swala za Sunna ambazo hazijatiliwa mkazo.

1. Swala Za Sunna Zilizo Tiliwa Mkazo:

Hizi ni zile ambazo Mtume Rehema na Amani zimshukie alizidumisha sana katika wakati wa kuwepo mjini (si katika safari), na akahimiza sana kuzifanya. Lakini alikuwa akiziacha kwa udhuru tu kama vile akiwepo safarini. Nazo zipo rakaa kumi na mbili: Rakaa nne kabla ya Adhuhuri, na rakaa mbilibaada yake, na rakaa mbili baada ya maghribi, na rakaa mbili baada ya ishai, na rakaa mbili kabla ya alfajri.

2. Swala za Sunna Ambazo Hazijatiliwa Mkazo:

Hizi ni zile ambazo Mtume Rehema na Amani zimshukie alikuwa baadhi ya nyakati anaziswali na wakati mwingine haziswali, kama vile: rakaa mbili au rakaa nne kabla ya Alasiri, na rakaa mbili kabla ya Maghribi, na rakaa mbili kabla ya Ishai.

Swala Ya Jeneza

Usheria Wake:

Swala ya jeneza imefaradhishwa na Allaah Mtukufu kwa ajili ya kuzikirimu roho za waislamu ambao wamehama katika maisha ya mji wa matendo (dunia) na kuelekea kwenye mji wa hesabu (akhera), nayo ni miongoni mwa

alama kubwaalizowaneemesha waja wake  waumini, na inayoonesha mapenzi baina yao, kwa sababu hudhihirisha undugu wa kweli inapotokea.Ndani yake kuna dua ya kuombeana waislamu wao kwa wao, na kulisindikiza jeneza mpaka kuzikwa. Na hali hii hudhihirisha nguvu ya mshikamano wa kidini uliopo baina yao. Eeh uzuri ulioje wa mshikamano huu na utukufu wake!! Tunamuomba Allaah mtukufu awarehemu maiti wa waislamu, hakika Yeye ni Msikivu wa dua, Aliye karibu kuitikia.

Hukumu Yake:

Swala ya jeneza ni nguzo ya kutoshelezana, wanapoisismamia baadhi ya waislamu, basi wengine wanasemehewa kwa kutokuwepo kwao, na vile vile imethibiti kwa kufanywa na Mtume Rehema na Amani zimshukie na maneno yake.[83]

Sharti Zake:

Sharti zake ni kama shari za swala ya faradhi, nazo ni: Kuwa na niya, kuwa baleghe, Mwenye akili, kuelekea

83_ “Al Mugh’niy” Vol. 2، Uk. 344.

kibla, kujistiri utupu, kuwa msafi wa mwili,nguo na sehemu ya ibada, na kuwa mwislamu.

Na vile vile ni sharti kwa maiti huyo (anayeswaliwa): Awe mwislamu, msafi (aliyeoshwa), na kuhudhurishwa mbele ya wanaomswalia ikiwa ni hapo hapo katika mji.

Nguzo Zake:

1. Kusimama kwa mwenye kuweza.

2. Kuleta takbira nne.

3. Kusoma surat Faatiha baada ya takbira ya kwanza.

4. Kumtakia rehma na amani Mtume Rehema na Amani ya Allaah zimshukie baada ya takbira ya pili.

5. Kumuombea dua maiti huyo baada ya takbira ya tatu.

6. Kufuata utaratibu wa nguzo.

7. Kutoa salamu.

Namna yake:

Atasimama Imamu kwenye usawa wa kichwa cha maiti mwanaume, na katikati ya maiti mwanamke.Kisha

Maamuma watasimama nyuma yake. Kisha ataanza kwa takbira ya kwanza na kusoma Surat Faatiha, kisha atatoa takbira ya pili na kumtakia rehma na amani Mtume Rehema na Amani zimshukie, kisha atatoa takbira ya tatu na kumuombea dua maiti huyo, na yeye mwenyewe na wazazi wake na waislamu wote, kisha atatoa takbira ya nne na kutulia kidogo hapo, kisha atatoa salaamu upande wa kulia mara moja.

## Baadhi Ya mambo Muhimu Katika Swala Ya Jeneza:[84]

1- Atakayepitwa na takbira yoyote basi atailipa.Na ikiwa hakuilipa na kutoa salamu pamoja na Imamu basi Swala yake ni sahihi.

2- Ikiwa yatachanganywa majeneza ya waislamu na makafiri pamoja, basi inaruhusiwa kuyaswalia yote lakini kwa nia tu ya kuswalia waislamu peke yao.

3- Kiporomoshi (mtoto mchanga) kikifikisha miezi minne na kufariki, basi huoshwa na kuswaliwa.

84_ "Mukh'taswaru Fiqhil Islaamiy" Uk. 7576_.

4- Maiti itakayopatwa na udhuru wa kutooshwa kwa sababu ya kuungua au kukatika katika katika viungo vyake, basi itatayamamishwa.Na inaruhusiwa kuswalia baadhi ya viungo vya maiti vilivyopatikana ikiwa haikupatikana kamili.

5- Atakayezikwa hali ya kuwa hajaswaliwa , basi ataswaliwa akiwa kaburini mwake wala hatofukuliwa.

## Somo La Tano: Zaka

Somo Hili Linakusanya Vipengele Vifuatavyo

Zaka

Maana Ya Zaka:

Maana yake ni kukua. Na inasemekana pia ina maana ya kukua na kusafisha, kwa sababu Zaka huikuza mali na kumsafisha mtoaji.

**Ama Zaka katika sheria**, ina maana ya: Haki ya lazima inayotolewa katika mali maalumu na kupewa watu maalumu katika muda maalumu ili kuhakikisha kupata radhi za Allaah na kuitakasa nafsi, mali na jamii.[85]

**Umuhimu Wake Na Hekima Ya Kuwa NiSheria**:

Zaka ina umuhimu mkubwa sana katika Uislamu.Kwa sababu hiyo, hekima ya kuwekewa sheria inadhihirika katika maeneo mengi.Tutayataja baadhi yake. Na yoyote mwenye kuzingatia, atauona umuhimu wa hii nguzo tukufu.

85_ "Kitaabu zakaah" cha Shekh Abdallah Al Twayyaar، Uk، 11،

Ubainifu Wa Baadhi YaHekima Za Kufaradhishwa Zaka:

1. Kusafisha nafsi za viumbe kutokana na uchafu wa ubakhili, ubinafsi na tamaa.

2. Kuwalewaza mafakiri na masikini kwa kuziba haja (shida) za wenye majanga, matatizo na wasiokuwa na mali.

3. Kusimamisha maslahi ya jamii ambayo yanaleta ustawi wa maisha bora na heshima zao.

4. Kudhibiti ulimbikizaji wa mali kwa matajiri na wafanya biashara, ili isijekuwa mali zinaishia kuwazungukia wao kwa wao tu.

5. Kuleta mshikamano wa jamii ya kiislamu na kuonesha kuwa ni jamii moja inayooneana huruma kwa mwenye uwezo kumhurumia asiye na uwezo.

6. Kuondosha chuki za mafakiri dhidi ya matajiri katika jamii.

7. Kuondosha makosa ya jinai yanayoweza kusababishwa na ubakhili wa matajiri, kama vile wizi,

uporaji au uteketezaji wa mali.

8. Kuitakasa mali na kuikuza katika baraka.

9. Hakika Zakaat ni sababu ya kueneza kheri katika jamii.[86]

Dalili za Uwajibu Wa Zaka:

Zimekuja dalili nyingi katika Qur’an na Sunna, zinazoonesha uwajibu wa Zakaat.

Na Mtume Rehema na Amani zimshukie ameibainisha kuwa ni miongoni mwa misingi mikubwa inayoujenga Uislamu.na kwa ajili hiyo, ikawa ni nguzo ya tatu katika nguzo kuu za dini hii.

Zifuatazo ni baadhi ya dalili zake:

Amesema Allaah mtukufu: {**Na simamisheni Sala, na toeni Zaka, na inameni pamoja na wanao inama**}. [Al Baqara: 43]. Na amesema: {**Na simamisheni Sala na toeni Zaka, na kheri yoyote mtakazo jitangulizia nafsi zenu mtazikuta kwa Mwenyezi Mungu.Hakika Mwenyezi Mungu anayaona mnayo yafanya**}. [Al Baqara: 110].

86- “Sharhul Mumtii Alaa Zaadil Mustaqnii” Vol. 6, Uk. 1214-. Na “Minhaajul Muslim” Uk. 367.

Na amesema tena: {**Na ikiisha miezi mitukufu basi wauweni washirikina popote mwakutapo, na washikeni na wazungukeni, na wavizieni katika kila njia.Lakini wakitubu, wakasimamisha Sala na wakatoa Zaka, basi waachilieni. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu**}. [Tauba: 5].

Na Ama Dalili Katika Sunna :

1. Hadithi ya Jibril iliyo mashuhuri, na ndani yake Mtume Rehema na Amani zimshukie, alisema: (Uislamu ni kushuhudia kuwa hakuna Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ispokuwa Allaah na hakika Muhammad ni mjumbe wa Allaah, na kusimamisha Sala, na kutoa Zaka, na kufunga mwezi wa Ramadhani na kuhiji katika Alkaaba ikiwa utaweza njia ya kuelekea huko).[87]

2. Kutoka kwa Abdi LLahi bin Omar radhi za Allah ziwe juu yake alisema: Alisema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Uislamu ujengwa juu ya mambo matano, kushuhudia kuwa hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah, na kwamba Muhammad ni Mjumbe wa Allah, na kusiamamisha Swala, na kutoa Zaka, na ku-

87- Imepokewa na Bukhari (8) na Muslim (120).

funga mwezi wa Ramadhan, na kuhiji katika Nyumba tukufu kwa mwenye kuweza).[88]

Hizo ni baadhi ya dalili kutoka katika Qur'an na Sunna zinazoonesha umuhimu wa Zaka kuwa ni mojawapo ya nguzo za Uislamu, na misingi yake mikubwa ambayo Uislamu wa mtu hauwezi kutimia bila nguzo hizo.[89]

Na kwa mujibu wa dalili hizi na zinginezo, Wanazuoni wote wameafikiana juu ya uwajibu wa Zaka.

**Tofauti kati Ya ZakaNa Kodi:**[90]

1. Zakainatolewa kwa niya ya kujikurubisha kwa Allah Mtukufu, tofauti na kodi ambayoinatolewa kwa lazima na kwa amri ya serekali.

2. Zaka ni haki iliyokadiriwa na Allah, kinyume na kodiambayo hupangwa na kiongozi kwa kuzidisha akipenda na kupunguza akipenda kwa mujibu wa maslahi ya nchi.

88- "Sahihi Bukhaary" Vol. 1، Uk. 8.
89- "Kitaabu Zakaah" Uk. 3435-.
90- "Kitaabu Zakaah" Uk. 57.

3. Zakainagawiwa kisheria kama alivyo pangilia Allah. Ama Kodi hukusanywa na kuhifadhiwa katika hazina ya nchi, kisha inatumika katika maslahi mbalimbali ya nchi.

4. Zaka ni nguzo ya lazima tangu kufaradhishwa kwake mpaka siku Qiyama. Ama kodi haina sifa ya kudumu.[91]

Je Kodi Inaweza Kutosheleza Kuliko Zaka?

Kwa mujibu wa tofauti tulizozieleza hapo juu, inabainika wazi wazi kuwa Kodi haiwezi kutosheleza kuliko Zaka.Kwa hiyo hairuhusiwi kabisa kuithamini Kodi kuliko Zaka, kwa sababu Zaka hutolewa na kupewa makundi maalumu yaliyotajwa kisheria na kuwawajibikia makundi maalumu na mali maalumu ambazo inalazimika kutolewa ili kuleta ustawi mzuri wa jamii husika, kinyume na Kodi ilivyo.

91_ "Kitaabu Zakaah" Uk. 57.

Tanbihi:

Kodi haiwezi kusimama badala ya Zaka. Na huu ndiyo msimamo wa Wanazuoni wote,[92] kwa sababu Zaka ni sheria ya Allaah na kodi ni kanuni za kuwekwa na viumbe.

Masharti Ya Zaka:

Masharti ambayo yanamuhusu Mtoaji Zaka ni:

1. Awe Mwislamu.

2. Aliye baleghe na akili timamu.

3. Aliye huru.

4. Mwenye nia thabiti.

Masharti Ambayo Yanaambatana Na Mali Yenyewe:

1- Umiliki uliotimia wa mali. Kwa maana mali iwe inamilikiwa na mtu mwenyewe na kusiwe na haki za watu wengine ndani yake, na awe anaweza kuitumia mwenyewe.

---

92_ "Majmuul Fatawa" cha Ibn Teymiyyah، Vol. 25، Uk. 93. Na "Muujaz Min Fiqhil Ibaadaat" Uk. 65. Na "Fiqhu Zakaah" cha Shekh Qardhwaawiy. Vol. 2، Uk. 1119.

2- Kukua kwa mali. Kwa maana mali ya Zaka inatakiwa iwe ni ile inayomletea faida mwenye nayo.

3- Mali ifikie kiwango cha kisheria.

4- Ipitiwe na Mwaka.

5- Iwe ni baada ya kukamilisha matumizi ya lazima, kama vile matumizi ya nyumbani, vifaa vya kivita, nguo za kuva yeye na familia yake n.k.[93]

Hukumu Ya Anayezuia Zaka:

Mwenye kuzuia Zaka ana moja ya mambo mawili:

**Jambo la kwanza:** Anaizuia kwa kukanusha kuwa Zaka siyo wajibu, na mtu huyo ana hali mbili:

**Hali ya kwanza**: Ima atakuwa ni mgeni katika uislamu (amesilimu), au ameishi vijijini. Katika hali kama hii, hatohukumiwa kuwa ni kafiri mpaka asimamishiwe hoja na kujulishwa uwajibu wa Zaka, kisha Zaka itakuchukuliwa kwa lazima, ikiwa ataendelea kupinga basi atahukumiwa kuwa ni kafiri na kupigwa vita mpaka ichukuliwe zaka kutoka kwake.

93_ "KITAABU ZAKAAH" UK. 33.

**Hali ya pili:** Na ima atakuwa ni mtu anaejua uwajibu wa Zaka, kwakuwa anaishi katik nchi ya kiislamu, katika hali kama hiyo mtu huyo atahukumiwa kuwa ni Kafiri, na atapigwa vita kwasababu ya kukataa kutoa Zaka.

**Jambo La Pili**: Ni kuzuia Zakaat kwa ubakhili hali ya kuwa anakubali uwajibu wake.

Katika hali hiyo, mtu huyo hatohukumiwa kuwa ni kafiri, bali itachukuliwa Zaka kutoka kwake kwa lazima na ataadhibiwa kwa adhabu atakayoiona kiongozi kuwa inamfaa.Hukumu hiyo itapaswa kutekelezwa na Kiongozi Muadilifu ambaye anasimamia mambo ya ugawaji wa Zakaat kisheria, na hatochukua zaidi ya fungu lililo wajibishwa.Ama ikiwa Kiongozi ni Dhalimu, basi mtu huyo hatoadhibiwa bali itachukuliwa zaka yake tu.[94]

94_ "Al Mugh'niy" Vol. 2، Uk. 435، Na "Kitaabu Zakaah" Uk. 7576_،

Mali Ambazo Zimewajibishwa Na Sheria Kutolewa Zaka:

Zaka inawajibika katika mambo vinne:

1. **Dhahabu na Fedha na vinavyosimama badala yake:**

Dhahabuinatolewa Zaka kwa sharti mbili:

(a) Lazima ipitiwe na mwaka.

(b) Lazima ifikie kiwango.

Kiwango chake ni kuanzia dinari ishirini, na kinachotolewa cha wajibu ndani yake ni Robo ya kumi.

Katika kila dinari ishirini itatotoewa nusu dinari, na kitakachokuwa kinazidi hupigiwa mahesabu hayo, sawa sawa kikiwa kichache au kingi.

Na imenithibitikia kuwa dinari ishirini ni sawa na gramu sabini za dhahabu,[95] kwa hivyo basikatika kila gram sabini za dhahabu (sawa na dinari ishirini) kiwango cha

95- Huo ni mtazamo wa mtunzi wa Kitabu، lakini Jamuhuri ya Wanchuoni wamekubaliana ya kwamba Dinari 20 ni sawa na gram 85 za dhahabu، na hiyo ndiyo fat'wa ya Jopo la Wanchuoni wa Saudi Arabia (Lajnatu Daaimah)، pamoja na Jopo la Wanachuoni wa Kiislamu (Majmaa Fiqhil Islaam).

wajibukinachotakiwa kutolewa katika Zaka ya dhahabu ni gramu 1,75, na hiyo ndiyo maana ya robo ya kumi.

2. Fedha: Masharti yake ni kupitiwa na mwaka, na kufikia kiwango.

Na kiwango chake ni kuanzia Auqia tano.

Na auqia moja ni sawa na dirhamu arobaini. Hivyo basi, kiwango cha Zaka ya fedha itakuwa ni Dirhamu mia mbili.

Na kiwango cha wajibukinachotakiwa kutolewa katika Zaka ya fedha ni robo ya kumi, kama ilivyo katika dhahabu.

Katika dirhamu mia mbili zitatolewa dirhamu tano na kitakachozidi hupigiwa mahesabu hayo hayo.

Na imenithibitikia kuwa kiwango cha fedha kwa gramu ni sawa na gramu mia nne na sitini (460 gm).[96] Kwa hiyo wajibu wa zaka yake ni robo ya kumi ambayo ni sawa na gramu 11,05.

Kutoa Zaka Ya Dhahabu Na Fedha Kwa Pesa Za

96- Huo ni mtazamo wa mtunzi wa Kitabu، lakini Jamuhuri ya Wanchuoni wamekubaliana ya kwamba Dirham 200 ni sawa na gram 595، na hiyo ndiyo fat'wa ya Jopo la Wanchuoni wa Saudi Arabia (Lajnatu Daaimah)، pamoja na Jopo la Wanachuoni wa Kiislamu (Majmaa Fiqhil Islaam).

Kawaida:

Ikiwa mtu atamiliki kiwango cha dhahabu na fedha na akataka kutoa zaka yake kwa pesa za kawaida , itamlazimu mambo yafuatayo :

1. Aulize bei ya gramu za dhahabu na fedha wakati wa kutaka kutoa zaka.

2. Akishajua bei ya dhahabu au fedha, atazidisha ile bei kwa kiwango cha fedha au dhahabu liyonayo, kisha atatoa robo ya kumi.

Kiwango cha Zaka kwa pesa za kawaida:

Mtu anaweza kudhani kwamba kwa kuwa hamiliki dhahabu wala fedha, basi hawajibiki kutoa zaka, kwa sababu dalili za kisheria zimezungumzia katika vitu hivyo tu.

**Tunamwambia:** Hii ni dhana potofu. Bali ukweli ni kuwa kila mwenye pesa zinazofikia kiwango cha gramu 70 za dhahabu au gramu 460 za fedha anawajibika kutoa zaka.[97] Atawajibika kutoa kiwango alichonacho kwa robo ya kumi (kwa maana asilimia mbili na nusu) ya pesa alizo nazo.

97_ Ufafanuzi wake umetangulia.

Zaka Ya Wanyama

Na wanyama tunaowakusudia hapa ni ngamia, ng'ombe, kondoo na mbuzi.

Masharti ya zaka ya wanyama:

1. Ifikie kiwango: Kiwango cha ngamia ni kuanzia ngamia watano, na kiwango cha kondoona mbuzi ni kuanzia arobaini, na kiwango cha ng'ombe ni kuanzia thelathini . Ama chini ya viwango hivyo hakuna zaka.

2. Wapitiwe na mwaka kwa mmiliki wake.

3. Wawe wanyama wanaofugwa na kuchungwa kwenye malisho kwa mwaka mzima.

4. Wasiwe wanyama wanaotumikishwa katika kazi kama za kilimo, au kubebea mizigo.[98]

Jeduwali Linalo Onyesha Viwango Vya Zaka Za Wanyama

98_ "Kitaabu Zakaah" Uk. 81.

## Zaka Ya Ngamia

| Kuanzia | Mpaka | Kinacho Wajibika Kutolewa |
|---|---|---|
| Ngamia 5 | Ngamia 9 | .Mbuzi mmoja |
| Ngamia 10 | Ngamia 14 | .Mbuzi wawili |
| Ngamia 15 | Ngamia 19 | .Mbuzi watatu |
| Ngamia 20 | Ngamia 24 | .Mbuzi wanne |
| Ngamia 25 | Ngamia 35 | .Ngamia mmoja mwenye mwaka mmoja |
| Ngamia 36 | Ngamia 45 | .Ngamia mmoja mwenye miaka miwili |
| Ngamia 46 | Ngamia 60 | .Ngamia mmoja mwenye miaka mitatu |
| Ngamia 61 | Ngamia 75 | .Ngamia mmoja mwenye miaka minne |
| Ngamia 76 | Ngamia 90 | .Ngamia wawili wenye miaka miwili |
| Ngamia 91 | Ngamia 121 | .Ngamia wawili wenye miaka mitatu |

## Zaka Ya Ngo’mbe:

| Kuanzia | Mpaka | Kinacho Wajibika Kutolewa |
|---|---|---|
| Ng’ombe 30 | Ng’ombe 39 | .Ng’ombe mmoja mwenye mwaka mmoja |
| Ng’ombe 40 | Ng’ombe 59 | .Ng’ombe mmoja mwenye miaka miwili |
| Ng’ombe 60 | Ng’ombe 69 | .Ng’ombe wawili wenye mwaka mmoja |
| Ng’ombe 70 | Ng’ombe 79 | Ng’ombe wawili mwenye miaka miwili .na mwenye mwaka mmoja |

## Zaka Ya Kondo/ Mbuzi:

| Kuanzia | Mpka | Kinacho Wajibika Kutolewa |
|---|---|---|
| Kondoo/ Mbuzi 40 | Kondoo/ Mbuzi 120 | .Mbuzi mmoja |
| Kondoo/ Mbuzi 121 | Kondoo/ Mbuzi 200 | .Mbuzi wawili |
| Kondoo/ Mbuzi 201 | Kondoo/ Mbuzi 399 | .Mbuzi watatu |
| Kondoo/ Mbuzi 400 | Kondoo/ Mbuzi 499 | .Mbuzi wanne |
| Kondoo/ Mbuzi 500 | Kondoo/ Mbuzi 599 | .Mbuzi watano |

Mali Ya Biashara

Maana yake:

Ni kila kilichoandaliwa kwa ajili ya biashara kwa malengo ya kupata faida.

Masharti yake:

1. Umiliki uliotimia wa biashara yenyewe.

2. Kufikia kiwango, nako ni kwa kufanya tathimini kwa imma dhahabu au fedha.

3. Kupitiwa na mwaka biashara yenyewe katika mzunguko wake.[99]

Kiwango cha wajibu ndani ya mali ya biashara:

Hutolewa robo ya kumi (asilimia mbili na nusu (2 ½%).[100]

99- "Kitaabu Zakaah" uk. 92.
100- "Kitaabu Zakaah" uk. 97.

Aina za mali za biashara:

Zipo aina mbili:

1- Mali zinazouzwa wala hazisubiri kupanda bei.

2- Mali zinazouzwa kwa kusubiri kupanda bei (kulimbikizwa).

Ikiwa ni mali ya kifungu cha kwanza, basi zaka yake itatolewa kama ilivyoelezwa hapo juu (kwa masharti yake na kiwango chake). Na ikiwa ni ya kifungu cha pili, basi zaka yake itatolewa katika kipindi itakapouzwa hata kama itasubiriwa kwa miaka kadhaa ili bei ipande.

Zaka Ya Nafaka Na Matunda

A- Vinavyotolewa:

Ni wajibu kutoa zaka ya nafaka na matunda katika Ngano, Shairi, Zabibu na Tende.

Wanazuoni wamekhitalifiana katika nafaka na matunda mengine yasiyokuwa hayo, je ni wajibu kutolewa zaka? Jamhuri ya wanazuoni (wanazuoni wengi) wanaona kuwa haiwajibiki kutolewa zaka vitu visivyokuwa hivyo

viliyotajwa hapo.

Ama sisi tunaona kuwa kila nafaka au tunda linaloliwa na kuwezekana kuwekwa (kuhifadhiwa) bila kuharibika basi ni wajibu kutolewa zaka.[101]

Ama mazao yasiyokuwa na sifa hizo basi si wajibu kutolewa zaka.

B- Kiwango chake:

Ni kuanzia Wasaq tano na zaidi, haiwajibiki kutoa zaka chini ya hapo, na ushahidi wa hayo ni kauli ya Mtume Rehma na Amani zimshukie: (Hakuna zaka katika mazao yaliyo chini ya wasaq tano.[102]Nacho ni kiwango kinachofikia kilogramu 675.

Uzinduo Juu Ya Zaka Ya Nafaka Na Matunda

1- Ni lazima nafaka na matunda hayo yawe yamekomaa na kuiva vizuri.

2- Ikiwa mazao hayo yamemwagiliwa bila gharama

101_ "Kitaabu Zakaah" uk. 97.
102_ Imepokewa na Bukhari (1459).

(maji ya ardhini tu), au yamemea yenyewe kwa maji ya mto au chemchem, basi zaka yake itawajibika kutolewa asilimia kumi. Na ikiwa mazao hayo yamemea kwa gharama za mkulima kwa kumwagilia maji nk, basi zaka yake ya wajibu kutolewa ni nusu ya kumi, kama ilivyoelekeza hivyo kauli ya Mtume Rehma na Amani zimshukie: (Katika mazao yaliyonyweshezwa na mvua na chemchem, basi hutolewa asilimia kumi, na yaliyonyweshezwa kwa gharama, basi hutolewa nusu ya kumi).[103]

3- Ikiwa yamemea kwa kunyweshezwa na mvua na gharama za mkulima, basi zaka yake hutolewa robo tatu ya kumi.

Mambo Muhimu Katika Zaka

Jambo la kwanza:

1- Mwenye kuwa na deni kwa mtu asiyelipa (msumbufu wa kulipa), zaka yake itatolewa atakapolipwa deni lake.

Na lililo bora ni kupanga hesabu ya zaka yake mapema kabla ya kulipwa.

Na kama anamdai mtu ambaye hana uwezo wa kulipa

103_ Imetolewa na Bukhari (1483).

kwa wakati kutokana na hali yake ya kipesa kuwa mbaya, basi atatoa Zaka pindi atakapo lipwa hata kama ni baada ya mwaka.[104]

Jambo la pili:

Vitu vilivyotolewa Waqfu ambavyo vinatoa huduma za mambo ya kheri kama vile Miskiti, mashule na mfano wake, havitolewi zaka.

Jambo la tatu:

Majumba, mashamba, magari, vifaa mbali mbali na mfano wake ambavyo vimewekwa kwa ajili ya biashara, basi hupigiwa thamani yake kila mwaka na hutolewa zaka ya robo ya kumi. Na ikiwa vimekodishwa, na vikapitiwa na mwaka katika hali hiyo, basi hutolewa zaka yake ya robo ya kumi.[105]

Jambo la nne:

Deni halizuii uwajibikaji wa zaka katika mali za wazi[106]

104_ "Mukh'taswarul Fiqhil Islaamiy" Uk. 79.
105_ "Mukh'taswarul Fiqhil Islaamiy" Uk. 79.
106_ "Mukh'taswarul Fiqhil Islaamiy" Uk. 79.

(Wanyama, mazao na matunda).

Jambo la tano:

Mtu atakayefariki na hajatoa zaka, basi warithi wake wtaitoa zaka yake kabla ya kurithi.[107]

Jambo la sita:

Atakayemiliki dhahabu ambayo haijafikia kiwango, na fedha ambayo haijafikia kiwango atazikusanya pamoja, ikiwa zitafikia kiwango, basi atatoa zaka kwa kila moja wapo kwa hesabu yake.

Na inafaa kutoa zaka ya dhahabu kwa niaba ya fedha, fedha kwa niaba ya dhahabu.

Na kuna ya Wanachuoni inayo sema kuwa haifai kukusanya dhahabu na fedha pamoja, na hiyo ndiyo kauli iliyo chaguliwana Sheikh wetu Muhammad Swaleh Al Uthaymiin Allaah amrehemu.[108]

Jambo la saba:

Katika Rikaaz: Ni mali iliyozikwa zamani kisha ikaokotwa:

107_ "Al Mugh'niy" Vol. 2، Uk. 466.
108_ "Al Mugh'niy" Vol. 2، Uk. 603604_. Na "Al Mumtii Fiy Sharhi Zaadil Mustaqnii" Vol. 6. Uk. 107108_.

Atakayekuta katika nyumba au ardhi mali iliyofukiwa katika mali za zamani, na ikawa ina thamani kwa kipindi hicho, basi atawajibika kutolea zaka ya asilimia tano kwa kuwapa mafakiri na masikini,[109] kwa ushahidi wa kauli ya Mtume Rehma na Amani zimshukie kuwa: (Katika mali iliyofukiwa hutolewa asilimia tano).[110]

Jambo la nane:

Je ni sharti mali ya kufukiwa zamani lazima kufikia kiwango na kupitiwa mwaka?

Kauli sahihi ambayo dalili nyingi zimethibitisha ni kuwa kinachozingatiwa ni kutopitiwa na mwaka wala kiwango, kwa kuwa mali hiyo hupatikana kwa mara moja tu, hivyo inakuwa kama mazao na matunda, muda yanapokomaa na kuiva tu wajibu wa zaka unapatikana hapo hapo.[111]

Jambo la tisa:

Zaka za Hisa na Mikataba ya kifedha ya riba:

**Hisa:** Ni haki za kimali zinazomilikiwa na watu katika makampuni au taasisi na kupata faida zake kwa mujibu

109- "Al Mugh'niy" Vol. 2، Uk. 585.
110- Imepokewa na Bukhari (1449).
111- "Al Mugh'niy" Vol. 2، Uk. 602.

wa utaratibu uliowekwa na kampuni au taasisi hiyo.

**Mikataba ya kifedha ya riba:**Ni kukiri kwa maandishi katika mikataba inayowekwa na makundi maalumu ya kibiashara kama vile Bank n.k, ili kupokea kiwango cha pesa maalumu kwa njia ya mkopo na kurejesha kwa riba, na mkataba huo unaainisha tarehe maalum ya kulipa deni hilo kwa riba iliyo kadiriwa.

Jinsi ya kutoa zaka katika Hisana Mikataba ya kifedha ya riba:

1- Zaka ya Hisa:

Mwenye muamala wa namna hiyo ana hiyari ya mambo mawili:

1. Kuutolea zaka mtaji wake kwa kila mwaka, na mtaji wake atautolea zaka kutokana na faida atakayoipata katika hisa, akipata faida hiyo atatoa zaka ya mwaka mmoja, na wametofautiana baadhi ya Wanachuoni katika jambo hilo.

2. Kuulizia mtaji wake kila mwaka kwa kujua fungu lake na kulitolea zaka kwa mujibu wa mahesabu atakayopewa na wasimamizi wa shirika au taasisi aliyomo.Sawa

sawa ikiwa kuna faida au hasara. Na zaka yake huwa kama ya dhahabu na fedha kwa kutoa robo ya kumi (asilimia mbili na nusu).[112]

2- Zaka ya Mikataba ya kifedha ya riba:

Tumetaja hapo nyuma kuwa haya ni madeni ya kucheleweshwa, na hivyo basi zaka yake inakuwa katika jumla ya zaka ya madeni, kwa maana ikiwa mtu anawadai watu wenye uwezo wa kulipa, mali anayodai ataitolea zaka kama mali zingine anazomiliki kwa sharti la kupitiwa na mwaka, na ikiwa anaowadai hawawezi kumlipa kwasababu ya kukosa pesa, zaka ya deni hilo ataitoa pindi atakapolipwa.[113]

Jambo la kumi:

Faida zinazo tokana na mali:

Na mali zinazo kusudiwa: Ni faida za kibiashara au ufugaji, faida hizo zinatolewa zaka kama ilivyo katika asili yake (yaani zaka ya mali kwa utaratibu wake, na zaka ya wanyama kwa utaratibu wake), kwasababu mambo

112_ "Kitaabu Zakaah" Uk. 106.

113_ UNAPO MDAI MTU ASIYEWEZA KUKULIPA KWASABABU YA UMASIKINI، NA PESA ILE IKAWA IMEFIKIA KIWANGO CHA KUTOA ZAKA، UTARATIBU WA KUITOLEA ZAKA PESA HIYO NI KWAMBA ITATOLEWA ZAKA SIKU YA KULIPWA، NA ZAKA YAKE NI MWAKA MMOJA.

mengine hayazingatiwi kupitiwa na mwaka kama vile zaka kwa wakulima.

Naatakayepewazawadiyamaliauakarithi,hatowajibika kutoa zaka mpaka ipitiwe na mwaka na kufikia kiwango chake.

Jambo la kumi na moja:

Je ni wajibu kutoa zaka kwa haraka?

Kauli iliyo sahihi ni wajibu kutoa zaka kwa haraka, wakati wowote kiwango kinapofikia na kupitiwa na mwaka, ni lazima zaka itolewe haraka, kwa sababu asili ya amri ni kutekelezwa kwa haraka.

Lakini kuna jambo lingine, nalo ni kuwa inaruhusiwa kuchelewesha ikiwa kuna maslahi ya kufanya hivyo.

**Kwa mfano**: Katika mwezi wa Ramadhan inakuwa vizuri kuitoa zaka kwa sababu ya kukithiri mafakiri na masikini, lakini mwezi wa Ramadhan huwa hauingii katika majira ya masika, kwasababu yiyo watu wanakuwa

na shida na wanaotoa zaka wanakuwa wachache, hivyo basi inaruhusiwa kuichelewesha kuitoa zaka kwa maslahi yanaoonekana, lakini kwa masharti mawili:

1- Aiweke wazi mali yake.

2- Aandike mkataba unaoweka wazi makusudio hayo.

Vile vile miongoni mwa sababu za kuruhusiwa kucheleweshа kutoa zaka ni kuhakiki wanaostahiki kupewa zaka,kwasababu ya kukithiri kupotea kwa amana katika zama hizi.

Wanaopewa Zaka

**Makusudio yake:** Ni kubainisha makundi ya watu wanaostahiki kupewa zaka, Allaah Mtukufu ameweka utaratibu wa kisheria kwa wanaostahiki kupewa zaka na kuwabainisha kuwa yapo makundi manane:

1. Mafukara.

2. Masikini.

3. Watendaji wake (Wanaosimamia ukusanyaji na ugawaji).

4. Wanaoliwazwa nyoyo zao.

5. Watumwa.

6. Wenye madeni.

7. Katika njia ya Allaah.

8. Wasafiri walio katikiwa njiani.

Kwanza: Mafakiri.

**Maana Ya Fakiri:** Ni mtu asiyejiweza kupata chochote kabisa.

Inasemekana pia ni Mtu anayepata kitu kichache sana katika mali lakini hakimtoshelezi.

Kinachozingatiwa katika ufakiri, siyo kinachomtosha mtu yeye pekee, bali na wale anaowasimamia, vile vile kinachozingatiwa siyo tu kile kinachomtosha mtu katika kula, kunywa, kuvaa na kuishi, bali kimekusanya mpaka cha kumtoshelezea mambo mengine ya msingi.

Kwa mfano: Ikitokea mtu anahitaji kuoa na akawa ana makazi, chakula, kinywaji na mavazi, ispokuwa akakosa mahari, basi anastahiki kupewa katika zaka kiasi kitakacho muwezesha mahitajio ya mahari hiyo ili aweze kuoa.[114]

Mas'ala muhimu Juu ya Fakiri:

Ikiwa mtu anaweza kufanya kazi na hana mali yoyote, na ikawa anahitaji kutafuta elimu, je anaweza kupewa katika zaka?

**Jawabu**: Ndiyo, anapewa katika zaka, kwa sababu kutafuta elimu ni sehemu katika sehemu ya Jihadi katika njia ya Allaah Mtukufu.[115]

114_ "Al Mumtii" Vol. 6. Uk. 220.
115_ "Arraudhwul Murbii Haashiyatu Ibn Qaasim" Vol. 2، Uk. 310. Na "Al Ikh'tiyaaraatu" cha Ibn Teymiyyah، Uk. 105.

Pili: Masikini:

**Maana Ya Msikini:** Ni yule ambaye ana uafadahli kuliko fakiri, lakini naye hana kinachoweza kumsaidia katika mahitaji yake muhimu.

Mtume Rehma na Amani zimshukie amembainisha kwa kusema: (Si masikini yule ambaye anazunguka kwa watu ili kupata tonge moja na matonge mawili, au tende moja na tende mbili, lakini masikini ni yule ambaye hapati cha kumtosheleza wala hata kufikiriwa na kupewa swadaqa, wala akawa hasimami na kuombaomba watu).[116]

Na masikini anamfuatia Fakiri katika hukumu zote.

Tatu: Watendaji wake (Wanaosimamia ukusanyaji na ugawaji):

**Maana Yake:** Ni wale ambao wanaotumwa na Kiongozi (Imaamu) kwa ajili ya kukusanya zaka.

Watatakiwa kupewa katika zaka kiasi kitachowatosha

116_ Imepokewa na Bukhari (1479).

wao na wasaidizi wao katika kipindi cha kazi yao hiyo, watapewa kwa kazi hiyo hata kama wanajiweza au sio wanao hitaji.

Nne: Wanao liwazwa nyoyo zao:

**Maana Yake:** Hao ni wale viongozi wenye heshima katika jamii, wanapewa zaka kwa ajili ya kulainisha nyoyo zao kutokana na mambo matatu muhimu:

1. Kutarajia kusilimu kwao, imma anaweza kuwa ni kafiri anayetarajiwa kusilimu, kama ni kafiri ambae hana dalili za kusilimu huyo hapewi zaka, na kafiri mwenye dalili za kusilimu anajulikana kwa baadhi ya dalili, na miongoni mwa dalili hizo, ni kafiri kuwa na mapenzi na waislamu au akawa anaomba vitabu vya kiislamu ili asome na mfano wa hayo.

2. Ni kupewa zakakwa ajili ya kuzuia shari zake, kama akiwa ni mwenye shari dhidi ya waislamu na mali zao au heshima zao, basi anapewa katika zaka kwa lengo la kuzuia shari zake.

3. Ni kupewa zaka kwa lengo la kuitia nguvu imani yake, kwa mfano: Kama akiwa ni mdhaifu wa imani katika

baadhi ya mambo ya wajibu, basi atapewa katika zaka ili kumtia nguvu.

Tano: Watumwa:

**Aina Za Watumwa:** Nao wamegawanyika katika makundi mbali mbali:

1. Wenye mikataba ambao wamepewa sharti la kujikomboa, basi hupewa zaka ili kuwawezesha kujikomboa na kuwa huru.

2. Awe mwislamu aliyetekwa katika mikono ya maadui, ikahitajika kumkomboa, basi hutolewa fungu hilo katika zaka.

3. Ikiwa ni mtumwa kabisa, ikahitajika kuachwa huru, basi itatolewa katika zaka ili kununuliwa na kuachwa huru.

Sita: Wenye Madeni:

**Maana Ya Wenye Madeni:** Nao ni wale ambao wenye madeni yasiyokuwa katika mambo ya kumuaasi Allaah na Mtume wake, na ikawawia ugumu wa kuyalipa, basi itatolewa katika zaka na kuwawezesha kulipa madeni hayo.

Aina Za Wenye Madeni:

Na hao wamegawanyika katika sehemu kuu mbili:

1- Katika kusuluhisha makundi mawili yaliyogombana ya waislamu, ikawa kuna uadui kati yao na ikahitajika mali katika kufanikisha suluhu yao, basi hutolewa katika zaka fungu la kufanikisha jambo hilo.

2- Ni kuwa mtu mwenyewe ana deni au madeni yanayomshinda kulipa kutokana na ufakiri alionao, basi atapewa katika zaka kiasi cha kulipia deni hilo.

Mas'ala Muhimu juu ya Kumsamehe Masikini mwenye madeni kwa nia ya kutoa Zaka:

Mfano wa jambo hilo: Ni mtu kumkopesha masikini kisha yule masikini akashindwa kulipa deni, na huyo mwenye mwenye kudai akawa na deni la zaka linalo lingana na pesa aliyo mkopesha masikini, je! Anaweza akahesabika kuwa ametoa zaka kwa kusamehe deni lake kwa yule masikini?

Jawabu: Usahihi ni kwamba haijuzu wala haitoshi,

kwasababu zaka ni kumpa mtu akapokea, na kufanya hivo ni kama vile kutoa kitu kichafu katika kitu kizuri.

Saba: Katika njia ya Allaah Mtukufu:

**Maana Yake:** Hao ni wapiganaji wa jihadi na silaha zao, na kila kinachohitajika katika kuitangaza dini ya Allaah, watu hao wanapewa zaka.

Vilevile baadhi ya Wanazuoni wameingiza matendo-mema na ya kheri kuwa ni katika njia ya Allah, jambo ambalo linatia wasi wasi, kwani ingekuwa ni sahihi, basi Qur'an na Sunna zingebainisha, hivyo basi msimamo sahihi ni kubakia tu katika mambo ya jihadi na kila linalosaidia kueneza dini ya Allaah.[117]

Nane: Msafiri:

**Maana Ya Wasafiri:** Ni wasafiri walio katikiwa na masurufu wakiwa katika safari ya halali, na ikawa hawana cha kuwasaidia kuwafikisha katika safari yao, basi hupewa katika zaka kinachowawezesha kufika katika safari yao na kuwaondoshea shida zao, hata kama wakiwa matajiri katika miji yao walikotokea.

117_ "Al Mumtii" Vol. 6، Uk. 241242_. Na "Kitaabu Zakaah" Uk. 115.

Wasioruhusiwa Kupewa Zaka

1. Matajiri.

2. Makafiri, kwa sababu ikiwa watapewa itakuwa wanasaidiwa katika ukafiri wao na kuonesha kuukubali.

3. Mwenye kutoa zaka hatakiwi kuwapa zaka watu wanao wahudumiakama vile mke, baba, mama, babu, bibi, watoto na wajukuu.

4. Familia ya Mtume Rehma na Amani zimshukie, nao ni Ukoo wa Hashimu na wa Abdul Mutwalib, na ikasemekana pia kuwa ni Ukoo wa Hashimu tu.

Zakaatul Fitri

Hukumu yake:

Ni wajibu juu ya kila muislamu, kama alivyosema Abdullaah bin Omar Allaah awaridhiye kuwa: (Mtume Rehma na Amani zimshukie aliifaradhisha zakaatu fitri katika mwezi wa Ramadhan kutolewa pishi ya tende au pishi ya shairi juu ya kila mtumwa na aliye huru, mwanaume na mwanamke, mdogo na mkubwa miongoni mwa waislamu).[118]

118- Imepokewa na Bukhari (1503).

Hekima ya kuwekwa sheria yake:

1. Ni kuwafanyia wema (Ihsaani) mafakiri, na kuwazuwia kutoomba omba katika masiku ya idi, na kuonesha ushirikiano wa pamoja na ndugu zao Matajiri katika furaha.

2. Ndani yake kuna kumsafisha mfungaji kutokana na upungufu uliopatikana katika funga yake miongoni mwa mambo ya upuuzi na madhambi madogo madogo.

Muda wa kuitoa:

Ni wajibu kuitoa usiku wa idi.

Na muda wa kuitoa umegawanyika katika sehemu mbili, muda unaoruhusiwa, na muda ulio bora.

**Ama muda unaoruhusiwa:** Ni kuitoa kabla ya idi kwa siku moja au mbili.

**Na ama muda ulio bora:** Ni kuitoa baada ya swala ya alfajri ya siku ya idi, na kabla ya kuswali idi.

**Wanaopewa zakaatul fitri:** Zakaat fitri hutolewa kwa mafakiri na masikini tu.

Je Zakaatul hii inawahusu mafakiri wa mji huo unaotolewa Zaka tu?

Kauli sahihi ni kuwa inaruhusiwa kuihamisha ikiwa kuna maslahi kwa waislamu wote kufanya hivyo.

Je inaruhusiwa kutoa pesa katika Zakaatil fitri?

Kauli sahihi ni kuwa hairuhusiwi kutoa pesa katika Zakaatil fitri, kwa sababu hii ni ibada iliyofaradhishwa katika makundi maalumu ya vyakula, hivyo basi hairuhusiwi kuitoa katika asili yake ya vyakula vilivyoainishwa.[119]

119- "Majaalisu Shahri Ramadhan" cha Shekh Muhammad bin Swaleh Al Utheymin، Uk. 228.

Somo La Sita: Swaumu

Somo Hili Linakusanya Vipengele Vifuatavyo:

1-Maana Ya Swaumu Katika Lugha Ya Kiarabu.

2- Maana Ya Katika Sheria.

3- Nafasi Ya Swaum Katika Uislamu.

4- Ubora Wa Swaum.

5- Dalili Za Swaumu.

6- Swaum Ni Wajibu Kwa Mtu Gani?

7- Kuonekana Kwa Mwezi Ramadhan Na Hukumu Zake.

8- Kufunga Siku Ya Shaka.

9- Nyudhuru Zinazo Mfanya Mtu Ale Mchana Wa Ramadhan.

10- Safari.

11- Asiyeweza Kufunga.

12- Mgonjwa Anaetarajiwa Kupona Na Hali Zake.

13- Mwenye Hedhi Na Nifasi.

14- Mwenye Mimba Na Mwenye Kunyonyesha.

15- Mambo Yanayo Haribu Swaumu.

16- Adabu Za Swaumu.

17- Mambo Ya Wajibu.

18- Mambo Ya Sunna.

19- Swala Ya Tarawehe Na Hukumu Zake.

20- Swaumu Ya Sunna.

21- Matunda Ya Swaumu Ya Sunna.

Swaum

Allah amefaradhisha Swaum na akaifanya kuwa ni nguzo ya nne katika nguzo za uislamu, na zikaja dalili nyingi katika Qur'an na Sunna zikibainisha na kuweka wazi hukumu zake, na tutazungumzia mambo machache yanayohusu Swaum katika kurasa zijazo.

Maana Ya Swaum Katika Lugha Ya Kiarabu:

Katika lugha ya kiarabu Swaum ina maana ya kujizuia kufanya chochote, amesema Allah Mtukufu akizungumzia Mariam: {**Hakika mimi nimeweka nadhiri kwa Mwenyezi Mungu ya kufunga; kwa hivyo leo sitasema na mtu**}. [Mariam: 26].

Maana Ya Swaum Katika Sheria:

Ni kujizuia kufanya mambo maalum kwa muda maalum, kwa mtu maalum na kwa masharti maalu, kwa niya ya kumuabudu Allah.

Na ushahidi wa hayo ni kauli ya Allah Mtukufu: {**Na kuleni na kunyweni mpaka ubainike kwenu weupe wa alfajiri katika weusi wa usiku. Kisha timizeni Saumu mpaka usiku**}. [Al Baqara: 187].

Swaum haiswihi isipokuwa kwa kutia niya tangu kuchomoza kwa alfajiri mpaka kuzama kwa jua, kwa masharti maalum ambayo ni lazima yakamilike.

Nafasi Ya Swaum Katika Uislamu

1. Swaum ni nguzo katika nguzo tano za uislamu, na ni katika ibada bora kwasababu Allah Mtukufu amejihusi-

sha nayo, amesema Allah katika hadithi Al Qudusiy: (Kila ibada za mwanadamu zina kisasi ndani yake siku ya Qiyama isipokuwa swaum, hakika swaum ni yangu na mimi ndiye nitakaye ilipa).[120]

2. Swaum ni ibada ya siri baina ya mja na Mola wake, ndani yake kuna uangalizi wa kweli katika nafsi ya muumini wa kweli, kwasababu swaum haina (riyaa) kujionyesha kwa hali yoyote, na inamfundisha muumini ahisi kuwa Allah anamuona na anatakiwa amuogope, na hayo ni malengo mazuri yanayo patikana katika swaum.[121]

3. Swaumu inaleta nidhamu, umoja, mapenzi, uadilifu na usawa katika jamii, na inaweka huruma na tabia njema katika moyo wa muumini, vilevile swaum inaihifadhi jamii kutokana na shari na mambo mabaya.

4. Hakika swaum inamfanya muislamu kuhisi maumivu ya ndugu yake, na hiyo inampelekea kuwafanyia wema masikini, na hilo linaleta mapenzi na udugu kati ya waislam.

5. Swaum ni mazoezi ya vitendo katika kuidhibiti nafsi

120_ "Sahihi Bukhary" Vol. 3، Uk. 22. Na "Sahihi Muslim" Vol. 3، Uk. 157.
121_ "Kitaabu Swiyaam" cha Abdallah Al Tawayyaar، Uk. 14.

na kuvumilia majukumu pamoja na mashaka.

Ubora Wa Swaum

Tunamshukuru Allah kwasababu hakuna ibada yoyote anayoifanya muislamu kumfanyia Mola wake isipokuwa ina ubora mwingi, Swala, Zaka, Hijja na Swam vina ubora mwingi.

Na miongoni mwa ubora wa swaum:

1. Ni kinga ya mwanadamu inayomzuia kuingia katika madhambi, na kwa kufanya ibada hiyo analipwa kheri nyingi, kutoka kwa Abuu Hureyra radhi za Allah ziwe juu yake hakika Mtume rehma na amani ziwe juu yake alisema: (Swaum ni kinga, na mmoja wenu akiwa kafunga basi asiseme machafu wala ujinga, na mtu akitaka kupigana nae au akamtukana, basi amwambie: Mimi nimefunga! Mimi nimefunga, naapa kwa Allah ambae nafsi yangu ipo mikononi mwake, harufu inayoka katika mdomo wa mtu aliyefunga ni nzuri zaidi kwa Allah kuliko harufu ya miski, anaacha chakula chake na kinywaji chake kwa ajili yangu, basi funga ni yangu na mimi ndiye nitakayeilipa,

na jema moja litalipwa mara kumi mfano wake).[122]

2. Swaum ni sababu ya kufutiwa madhambi, kutoka kwa Hudheyfa radhi za Allah ziwe juu yake alisema: Nilimsikia Mtume rehma na amani ziwe juu yake akisema: (Makosa anayofanya mtu kwa familia yake, na katika mali yake, na anayo mfanyia jirani yake, yanafutika pindi anapo swali, na anapofunga na kuto sadaka).[123]

3. Allah Mtukufu ameihusisha swaum na mlango ambao hataingia mtu Peponi kupitia mlango huo isipokuwa mfungaji, kutoka kwa Sahli radhi za Allah ziwe juu yake alisema: Alisema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Hakika Peponi kuna mlango unaoitwa Rayyaan, wataingia kupitia mlango huo wafungaji siku ya Qiyama, itatangazwa wako wapi wafungaji? Watasimama na kuingia katika mlango huo, hakuna ataeingia isipokuwa wafungaji, pindi watakapoingia wote mlango huo utafungwa na hataingia yeyote).[124]

122_ "Sahihi Bukhary" vol. 3، Uk. 22. Na "Sahihi Muslim" Vol. 3، Uk. 157.
123_ "Sahihi Bukhary" vol. 3، Uk. 22. Na "Sahihi Muslim" Vol. 3، Uk. 173.
124_ "Sahihi Bukhary" vol. 3، Uk. 23. Na "Sahihi Muslim" Vol. 3، Uk. 157.

Dalili Juu Ya Uwajibu Wa Swaum

Funga ya Ramadhan ni moja kati ya nguzo za kiislamu, na ni faradhi miongoni mwa faradhi muhimu za Allah, ni nguzo inayojulikana na Wanachuoni wote wamekubaliana juu ya uwajibu wake, na zimekuja dalili nyingi zinazo onyesha juu ya uwajibu wake katika Qur'an na Sunna na makubaliano ya Wachuoni.

Dalili Ya Uwajibu Wa Swaum Katika Qur'an:

Amesema Allah Mtukufu: {**Enyi mlio amini! Mmeandikiwa Saumu, kama waliyo andikiwa walio kuwa kabla yenu ili mpate kuchamngu**. **(Mfunge) siku maalumu za kuhisabika. Na atakaye kuwa miongoni mwenu mgonjwa au yumo safarini basi atimize hisabu katika siku nyengine. Na wale wasio weza, watoe fidiya kwa kumlisha masikini. Na atakaye fanya wema kwa kujitolea, basi ni bora kwake. Na mkifunga ni bora kwenu, kama mnajua**.**Mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa humo Qur›ani kuwa ni uwongofu kwa watu, na hoja zilizo wazi za uwongofu na upambanuzi. Basi ataye kuwa mjini katika mwezi huu naafunge. Na**

**mwenye kuwa mgonjwa au safarini, basi atimize hisabu katika siku nyengine. Mwenyezi Mungu anakutakieni yaliyo mepesi wala hakutakieni yaliyo mazito, na mtimize hiyo hisabu, na mumtukuze Mwenyezi Mungu kwa kuwa amekuongoeni ili mpate kushukuru**}. [Al Baqara: 183185-].

**Na Dalili Katika Sunna:** Kutoka kwa Abdi LLahi bin Omar radhi za Allah ziwe juu yake alisema: Alisema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Uislamu umejengwa juu ya nguzo tano: Kushuhudia ya kwamba hapana Mola apasae kuabudiwa isipokuwa Allah na Muhammad ni Mjumbe wa Allah, na kusimamisha Swala, na kutoa Zaka, na kufunga mwezi wa Ramadhan, na kuhiji katika nyumba tukufu kwa mwenye uwezo).[125]

**Dalili Katika Ijmaai Ya Wanachuoni:** Ni kwamba umma mzima umeafikiana kuwa swaum ni nguzo katika nguzo za uislamu, na jambo hilo linajulikana katika uislamu, na wamekubaliana ya kwamba mwenye kukanusha uwajibu wa swaum akuwa kafiri.[126]

125_ "Sahihi Bukhary" vol. 1، Uk. 8. Na "Sahihi Muslim" Vol. 1، Uk. 34.
126_ "Badaaiu Sunaaiu" Vol. 2، Uk. 75. Na "Al Majmuu" Vol. 6، Uk. 248. Na "Al Mugh'niy" Vol. 4، Uk. 324.

Swaum Ni Wajibu Kwa Mtu Gani?

Swaum ni wajibu kwa kila muislamu aliye baleghe, mwenye akili, mkazi asiyekuwa msafiri, mwenye uwezo wa kufunga, na asiyekuwa na pingamizi.

Na kubaleghe kunapatikana kwa moja kati ya mambo matatu:

1. Kutokwa na manii kwasababu ya kujiotea au kwasababu nyingine.

2. Kuota nywele za kinena.

3. Kutimiza miaka kimi na tano.[127]

Kuonekana Kwa Mwezi Ramadhan Na Hukumu Zake

1. Mwezi wa Ramadhan unaingiaje?

Mwezi wa Ramadhan unaingia kwa moja ya mambo mawili:

(a) Kwa kuonekana mwezi.

(b) Kutimia siku thalathini za mwezi wa Shaaban.

127_ "Al Mumtii Fiy Sharhi Zaadil Mustaqnii" cha Shekh Ibn Utheymiin، Vol. 2، Uk. 73. Na "Al Saylul Jiraar" Vol. 3، Uk. 308.

2. Mwezi wa Ramadhan unathibiti vipi kuonekana kwake?

Muandamo wa mwezi wa Ramadhan unathibiti kwa kuuona mtu mtu mmoja muadilifu, ama kuondoka kwa mwezi wa Ramadhan kunathibiti kwa kuuona watu wawili waadilifu, ili kukubaliwa habari ya kuuona mwezi wa Ramadhan anatakiwa aliyeuona awe ametimiza masharti yafuatayo:

(a) Awe ni muislamu.

(b) Awe amebaleghe.

(c) Awe na akili (asiwe mwendawazimu).

(d) Habari zake ziwe na uhakika kutokana na uaminifu wake, asiwe na matatizo ya macho.[128]

3. **Kufunga SikuYa Shaka**

Siku ya shaka ni siku ya thalathi ya mwezi wa Shaaban ikiwa mwezi haukuonekana kwasababu ya mawingu ama ukungu au kwasababu nyingine.

Ni wajibu kula katika siku hiyo ikiwa mwezi haukuon-

128. "Kitaabu Swiyaam" cha Shekh Abdallah Al Twayyaar, Uk. 47.

ekana kutokana na sababu hizo, na ndiyo kauli sahihi ya Wanachuoni, amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Na ikiwa kutakuwa na mawingu basi kadirieni),[129] na katika riwaya nyingine: (Timizeni siku thalathini za mwezi wa Shaaban).[130]

Nyudhuru Zinazo Mfanya Mtu Ale Mchana Wa Ramadhan

**1. Safari:** Amesema Amesema Allah Mtukufu: **{Na atakaye kuwa miongoni mwenu mgonjwa au yumo safarini basi atimize hisabu katika siku nyengine**}. [Al Baqara: 184].

Na hiyo ni dalili ya wazi inayo juzisha kula mchana wa Ramadhan kwa msafiri, lakini atalipa kwa kadri ya siku alizokula.

**2. Ni Mtu Asiyeweza Kufunga Katika Maisha Yake:** Amesema Allah Mtukufu: {**Basi mcheni Mwenyezi Mungu kama mwezavyo**}. [Al Taghaabun: 16], na amesema Allah Mtukufu: {**Mwenyezi Mungu haikalifishi nafsi yoyote ila kwa kadiri ya iwezavyho**}. [Al Baqara: 286].

129_ “Sahihi Bukhary” vol. 3، Uk. 24. Na “Sahihi Muslim” Vol. 3، Uk. 122
130_ “Sahihi Bukhary” vol. 3، Uk. 24. Na “Sahihi Muslim” Vol. 3، Uk. 122

Na mtu kama huyo ni wajibu kwake kila siku kumlisha masikini mmoja.[131]

**3. Mgonjwa Anaetarajia Kupona:** Mtu huyo sheria imemruhusu kula na atalipa akipona, na kipengele hiki kina hali tatu:

(a) Mgonjwa huyo ikiwa hapati tabu kufunga wala swaum haimdhuru, basi ni wajibu kwake kufunga.

(b) Mgonjwa huyo ikiwa kufunga kwake ni shida lakini swaum haimdhuru, basi anatakiwa afungue (ale) wala si wajibu kwake kufunga, kwasababu akifunga atakuwa anaiadhibu nafsi.

(c) Mgonjwa huyo ikiwa atapata madhara kwa kufunga basi ni wajibu kwake kufungulia (kula), na haijuzu kwa mtu huyo kufunga kama ailivyosema Allah Mtukufu: {**Wala msijiuwe. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwarehemuni**}. [Nisaa: 29].

**4. Mwenye Hedhi Na Nifasi:** Ni haramu kwa mwenye hedhi na nifasi, na hata wakifunga swaum zao haziswihi,

131_ "Tafsiir Ibn Kathiir" Vol. 1، Uk. 215. Na "Fat'hul Qadiir" Vol. 1، Uk. 180.

na ni wajibu kwao kulipa idadi ya siku walizokula.[132]

Ama dalili ya kutokufunga kwao ni hadithi ya Abii Said Al Khud'riy radhi za Allah ziwe juu yake alisema: Alisema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Je hufahamu ya kwamba mwanamke akiwa katika siku zake haswali wala hafungi? Basi huo ndio upungufu wa dini yao).[133]

Na dalili ya uwajibu wa kulipa kwa mwanamke huyo ni kauli ya Allah Mtukufu: {**Basi atimize hisabu katika siku nyengine**}. [Al Baqara: 185].

Vilevile hadithi ya Aisha radhi za Allah ziwe juu yake: (Tulikuwa tunapata hedhi zama za Mtume rehma na amani ziwe juu yake tunaamrishwa kulipa swaum na hatuamrishwi kulipa swala).[134]

**5. Mjamzito Na Mwenye Kunyonyesha:** Watu hao wana hali tatu:

(a) Pindi watakapo hofia nafsi zao na watoto wao, watafungua na kulipa, na ushahidi wa hilo ni maneno ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Hakika Allah

132_ "Majmuul Fataawah" cha Sheykul Islaam Bin Teymiyah، Vol. 25، Uk. 220.
133_ "Sahihi Bukhary" vol. 3، Uk. 36.
134_ "Sahihi Bukhary" vol. 1، Uk. 420.

amemuondoshea msafiri nusu ya swala na funga, na kwa mjamzito na mwenye kunyonyesha nusu ya swaum).[135]

(b) Wakila mchana kwa kuhofia watoto wao pekee, watalipa swaum na kafara, na hiyo ndiyo sahihi katika kauli za Wanachuoni- na ikiwa hawana uwezo wa kutoa kafara basi watalipa swaum bila ya kafara-.

(c) Wakila mchana kwa kuhofia nafsi zao pekee, watalipa swaum bila ya kutoa chochote.[136]

Mambo Yanayo Haribu Swaum

Swaum inaharibika kwa kupatikana moja kati ya mambo saba:

1. Kufanya tendo la ndoa mchana wa Ramadhani.

2. Kutokwa na manii.

3. Kula na kunywa kwa kusudia.

4. Nikufanya kitu chenye maana ya kula na kunywa, kama vile mtu kuchoma sindano yenye kumpa nguvu kiasi

---

135_ "Sunanu Abii Daud" Vol. 1، Uk. 796. Na "Sunanu Nasaai" Vol. 4، Uk. 190. Na "Sunanu Tirmidhiy" Vol. 2، Uk. 109.

136_ "Al Mumtii Fiy Sharhi Zaadil Mustaqnii" cha Shekh Ibn Utheymiin، Vol. 6، Uk. 360361_.

asitamani kula wala kunywa.

5. Kujitapisha kwa kukusudia, lakini akitapika bila ya kukusudia basi swaum yake ni sahihi.

6. Kufanya Hijaamah (Kuumika).

7. Kutokwa na damu ya hedhi au nifasi.[137]

Adabu Za Swaum

Swaum ina adabu zake na mambo ya wajibu na yaliyo ya Sunna:[138]

Adabu Za Wajibu Katika Swaum

1. Kujiepusha na uongo, kwasababu uongo ni haramu wakati wote, na kipindi cha swaum uharamu wake ni mkubwa zaidi.

2. kujiepusha kusema watu.

3. Kujiepusha na kusengenya, nako ni kuhamisha maneno baina ya watu kwa lengo la kuwagombanisha, na jambo hilo ni katika madhambi makubwa.

137_ "Kitaabu Swiyaam" cha Shekh Abdallah Al Twayyaar، Uk. 99108_

138_ "Kitaabu Swiyaam" cha Shekh Abdallah Al Twayyaar، Uk. 130.

4. Kujiepusha na udanganyifu katika kazi zote zikiwemo kuuza, kununua na katika mambo ya ufundi.

5. Mfungaji ajiepushe na kushuhudiamambo ya uongo, kwasababu kufanya hivo kunapingana na swaum kwa kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Yeyote ambae hakuacha maneno ya uongo na kuyafanyia kazi basi hana ya kuacha chakula chake wala kinywaji chake).[139]

Mambo Yanayo Pendeza Kwa Mtu Aliyefunga:

1. Kula Daku: Ni Sunna kwa mtu aliyfunga kula Daku kwa kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Kuleni Daku, hakika katika kula Daku kuna baraka).[140]

2. Kuchelewesha kula Daku: Kwasababu jambo hilo limethibiti kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake, kutoka kwa Zaid bin Thaabit radhi za Allah ziwe juu yake alisema: (Tulikula Daku pamoja na Mtume rehma na amani ziwe juu yake, kisha alipo maliza akaenda kuswali), Anasi bin Maalik akamuuliza Zaid: kulikuwa kuna muda gani kati ya Adhana na Swala ya Alfajiri? Akasema: (Kia-

139_ "Sahihi Bukhary" vol. 3، Uk. 130.
140_ "Sahihi Bukhary" vol. 2، Uk. 76. Na "Sahihi Muslim" Vol. 3، Uk. 130.

si cha kusoma Aya khamsini).[141]

3- Kuharakisha kufuturu: Amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Watu hawachi kuwa katika kheri kwa muda ambao wameharakisha kufuturu).[142]

4. Kuhifadhi ulimi kutokana na amaneno machafu.

5. Kuinamisha macho yasiangalie yale aliyo yaharamisha Allah, kwasababu macho mawili yanafunga kama viungo vingine, na funga ya macho ni kuyazuia yasitazame mambo ya haramu, na vilevile funga ya macho ipo aina mbili, kuna ile ya wajibu na ile iliyo pendekezwa.

6. Kukithirisha kusoma Qur'an na kufanya adh'kaar, kuomba dua, kuswali na kutoa sadaka.[143]

Swala Ya Tarawehe

Swala ya Tarawehe ni Sunna kwa wanaume na wanawake, inatekelezwa baada ya Swala ya Ishaa na muda wake unaendelea mapaka mwisho wa usiku, na inaswaliwa kwa jamaa na mtu mmoja mmoja, na kuswali kwa ja-

141_ "Sahihi Bukhary" vol. 3، Uk. 26. Na "Sahihi Muslim" Vol. 3، Uk. 131.
142_ "Sahihi Bukhary" vol. 3، Uk. 33. Na "Sahihi Muslim" Vol. 3، Uk. 131
143_ "Al Muhallah" Vol. 6، Uk. 541. Na "Al Majmuu" Vol. 6، Uk. 359. Na "Naylul Autwaar" Vol. 4، Uk. 107.

maa ni bora, na dalili ya ubora wa swala hiyo ni kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Mwenye kusimama usiku katika mwezi wa Ramadhan akimuamini Allah na kwa lengo la kupata thawabu, atasamehewa madhambi yake yaliyo tangulia).[144]

Idadi Ya Rakaa Za Tarawehe: Kauli iliyo sahihi zaidi ni kwamba idadi ya rakaa za swala ya Tarawehe ni kumi na moja au kumi na tatu au kumi na tatu zenye kisimamo kirefu, kwa ushahidi wa hadithi ya Aisha radhi za Allah ziwe juu yake pindi alipoulizwa kuhusu swala ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake katika mwezi wa Ramadhan alijibu kwa kusema: (Mtume rehma na amani ziwe juu yake katika mwezi wa Ramadhan na miezi minginehakuwa akizidisha zaidi ya rakaa kumi na mija, alikuwa anaswali rakaa nne usiulize kuhusu uzuri na urefu wa swala hiyo, kisha anaswali rakaa nne usiulize kuhusu uzuri na urefu wake! Kisha anaswali rakaa tatu).[145]

Ama kuhusu rakaa kumi na tatu, ni kutokana na hadithi ya Abdi LLahi bi Abas radhi za Allah ziwe juu yake

144_ "Sahihi Bukhary" vol. 3، Uk. 39. Na "Sahihi Muslim" Vol. 3، Uk. 177.
145_ "Sahihi Bukhary" vol. 3، Uk. 40.

alisema: Ilikuwa swala ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Ni rakaa kumi tatu usiku).[146]

Swaum Ya Sunna

Makusudio ya swaum ya Sunna: Ni swaum ambazo zimeelezwa katika Qur'an na Sunna kuwa ni bora kufunga, na swaum hizo:

1. Swaum ya siku za mwezi wa Shawwaal:Kutokana na kauli ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Mwenye kufunga mwezi wa Ramadhan kisha akafuatisha siku sita za Shawwaal, atakuwa ni kama amefunga mwaka mzima).[147]

2. Funga ya siku ya Arafah kwa mtu ambaye hajaenda hijja: amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Swaum ya siku ya Arafah Allah anasamehe madhambi ya mwaka uliopita na mwaka ujao).[148]

3. Kufunga siku ya Ashuraa na siku moja kabla yake au baada yake: Amesema Mtume rehma na amani ziwe

146_ "SAHIHI BUKHARY" VOL. 2، UK. 46. NA "SAHIHI MUSLIM" VOL. 2، UK. 178.
147_ "Sahihi Muslim" (1164).
148_ "Sahihi Muslim" (1162).

juu yake akiizungumzia swaum ya Ashuraa: (Allah anasamehe madhambi ya mwaka uliopita).[149]

4. Kufunga masiku meupe: Nayo ni tarehe kumi na tatu, kumi nne na kumi na tano za kila mwezi, amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake katika kuelezea ubora wake: (Funga ya siku tatu za kila mwezi, malipo yake ni sawa na kufunga mwaka mzima)[150]

5. Swaum ya Jumatatu na Alkhamis: Amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Matendo ya mja napandishwa mbinguni katika siku mbili Jumatatu na Alkhamis, basi ninapenda matendo yangu yapandishwe hali ya kuwa nimefunga).[151]

6. Kukithirisha kufunga katika mwezi wa Shaaban na katika mwezi wa Muharram, amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Swaum iliyo bora baada ya Ramadhan ni swaum katika mwezi wa Muharram…),[152] na kwa kauli ya Aisha radhi za Allah ziwe juu yake: (Mtume rehma na amani ziwe juu yake hakuwa anafunga sana

149- “Sahihi Muslim” (1134).
150- “Sahihi Bukhary” vol. 4, Uk. 192. Na “Sahihi Muslim” (1159).
151- “Sunanu Tirmidhiy” (747).
152- “Sahihi Muslim” (1163).

kama anavyo funga katika mwezi wa Shaaban…).[153]

7. Kufunga siku moja na kufungua siku ninayofuata: Amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Swaum inapendeza zaidi kwa Allah ni swaum ya Nabii Daud amani iwe juu yake, alikuwa anafunga siku moja na kufungua siku inayo fuata).[154]

Athari Zinazo Patikana Kwa Kufunga Sunna

Miongoni mwa athari zinazo patikana kwa kufunga Sunna:

1. Ni katika ibada zinazo mkurubisha mja kwa Mola wake, kwasababu mja kufunga baada ya Ramadhan ni alama ya kukubaliwa ibada.

2. Kufunga baada ya Ramadhan ni alama ya mja kumshukuru Mola wake, kwasababu kufunga mwezi wa Ramadhan kwa imani na kutaka thawabu kunamfanya mja asamehewe madhambi yake yaliyo tangulia, kwasababu hiyo Allah ameweka sheria ya kufunga baada ya Ramadhan kwa ajili ya kushukuru neema hiyo.

---

153- "Sahihi Bukhary" vol. 3، Uk. 186. Na "Sahihi Muslim" Vol. 2، Uk 811.
154- "Sahihi Bukhary" vol. 3، Uk. 13. Na "Sahihi Muslim" Vol. 2، Uk 826، (189).

3. Kufunga Sunna ni ahadi ya nmuislamu kwa Mola wake, kwasababu nyakati za ibada zinaendelea, na maisha ya mwanadamu yote ni ibada.

4. Kufunga Sunna ni sababu mja kupendwa na Allah, na kujibiwa dua zake pamoja na kusamehewa madhambi yake.

Tunamuomba Allah Mtukufu atuzidishie malipo na aturehemu kwa rehema zake, hakika Yeye ni msikivu na yupo karibu na ni mwenye kujibu dua.

Somo La Saba: Hijja

Somo Hili Linakusanya Vipengele Vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | Maana Ya Hijja. | 2 | Dalili Za Kufaradhishwa Kwa Hijja. |
| 3 | Fadhila Za Hijja. | 4 | Malengo Ya Hijja. |
| 5 | Sharti Za Hijja. | 6 | Mipaka Ya Hijja |
| 7 | Mambo Muhimu Kuhusu Mipaka Ya Hijja. | 8 | Mwenye Kupita Katika Mipaka Bi ya Kuhirimia. |
| 9 | Mwenye Kuishi Ndani Ya Mipaka. | 10 | Mwenye Kusafiri Kwa Ndege. |
| 11 | Mwenye Kuvuka Mipaka Bila Ya Kuhirimia | 12 | Ibada Ya Hijja. |
| 13 | Kuhirimia. | 14 | Hukumu Ya Kuhirimia. |
| 15 | Aina Za Kuhirimia. | 16 | Mambo Ya Wajibu Katika Kuhirimia. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 17 | Mambo Ya Sunna Katika Kuhirimia. | 18 | Yasiyofaa Kwa Mwenye Kuhirimia. |
| 19 | Kuleta Talbiyah. | 20 | Maana Ya Kuleta Talbiyah. |
| 21 | Hukumu Ya Kuleta Talbiyah. | 22 | Kufanya Twawaafu. |
| 23 | Maana Ya Kufanya Twawaafu. | 24 | Hukumu Ya Kufanya Twawaafu. |
| 25 | Sunna Za Twawaafu. | 26 | Kufanya Saayi. |
| 27 | Hukumu Ya Saayi. | 28 | Sharti Za Saayi. |
| 29 | Kusimama Arafah. | 30 | Hukumu Ya Kusimama Arafah. |
| 31 | Hukumu Ya Mwenye Kuchelewa Kusimama Arafah. | 32 | Mambo Yanayo Ambatana Na Kusimama Arafah. |
| 33 | Kulala Muzdalifah. | 34 | Hukumu Ya Kulala Muzdalifah. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 35 | Hukumu Ya Mwenye Kuacha Kulala Muzdalifah. | 36 | Kurusha Mawe. 54- Makosa Ya Baadhi Ya Mahujaji. |
| 37 | Hukumu Ya Kurusha Mawe | 38 | Muda Wa Kurusha Mawe. |
| 39 | Sharti Za Kurusha Mawe | 40 | Hukumu Ya Kuwakilisha Katika Kurusha Mwawe. |
| 41 | Kunyoa Au Kupunguza. | 42 | HukumuYaKunyoa Au Kupunguza. |
| 43 | Muda Wa Kunyoa | 44 | Yanayoambatana Na Kunyoa. |
| 45 | Kuchinja Mnyama. | 46 | Makusudio Ya Kuchinja |
| 47 | Vigawanyo Vyake. | 48 | Tofauti Yake. |
| 49 | Sharti Zake. | 50 | Kulala Mina. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 51 | Hukumu Yake. | 52 | Anaesamehewa Kulala Mina. |
| 53 | Kulala Mina Kunako Takiwa. | 54 | |
| 55 | Umraha Na Hukumu Zake. | 56 | Sifa Zake. |
| 57 | Nguzo Zake. | | Mambo Ya Wajibu. |

Hijja

**Maana Ya Hijja:** Ni kukusudia kwenda katika nyumba tukufu katika muda maalum kwenda kutekeleza ibada, ikiwemo Kutufu, kufanya Saayi, kusimama Arafahna mengineyo.[155]

Dalili Za Kufaradhishwa Kwa Hijja

Zimekuja dalili katika Qur'an na Sunna zinazo onyesha kuwa Hijja ni faradhi, na Wanachuoni wamekubaliana

155_ "Haashiyatu Ibni A'bidiina" Vol. 3، Uk. 454. Na "Haashiyatu Dusuuq" Vol. 3، Uk. 2. "Rawdhwul Murbii" Vol. 3، Uk. 500.

juu ya jambo hilo, na miongoni mwa dalili katika Qur'an tukfu:

Amesema Allah Mtukufu: {**Na kwa ajili ya Mwenyezi Mungu imewajibikia watu wahiji kwenye Nyumba hiyo, kwa yule awezae njia ya kwendea. Na atakaye kanusha basi Mwenyezi Mungu si mhitaji kwa walimwengu**}. [Al Imaraan: 97].

Na dalili katika Sunna: Hadithi ya Abdi LLahi bin Omar radhi za Allah ziwe juu yake alisema: Alisema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Uislamu umejengwa juu ya mambo matano), na katika mambo hayo akataja Hajji.

Vilevile hadithi ya Abuu Hureyra radhi za Allah ziwe juu yake alisema: Alitukhutubia Mtume rehma na amani ziwe juu yake akasema: (Enyi watu Allah amekufaradhishieni Hijja basi nendeni mkahiji), mtu mmoja akasema: Ewe Mjumbe wa Allah ni kila mwaka? Mtume rehma na amani ziwe juu yake akakaa kimya, yule mtu akauli mara tatu, Mtume rehma na amani ziwe juu yake akasema: (Laiti ningesema ndiyo, basi ingekuwa ni wajibu lakini msingeweza).[156]

156_ "Sahihi Muslim" Vol. 2، Uk. 102.

Ama kuhusu makubaliano ya Wanachuoni juu ya uwajibu wa Hijja, Wanachuoni wote wamekubaliana juu ya faradhi ya Hijja, na miongoni mwao ni Al Kaasaaniy[157] na Ibni Qudaamah.[158]

Fadhila Za Hijja

Hijja ina ubora mkubwa ulio bainishwa katika Qur'an na Sunna, na tutataja baadhi ya dalili zilizo elezwa juu ya ubora huo:

1. Hijja inafuta madhambi yaliyokuwa kabla yake, ikiwemo shirki, ukafiri na madhambi mengine:

Na ushahidi wa hilo ni hadithi ya Amru binil A'swi alisema: … Allah alipouweka uislamu katika moyo wangu, nilimuendea Mtume rehma na amani ziwe juu yake nikamwambia: Nyoosha mkono wako wa kulia ili nifanye mafungamano na wewe ya utawala (Bay'ah), Mtume akanyoosha mkono wake wa kulia, akasema: Nikashika mikono yangu, Mtume rehma na amani ziwe juu yake akasema: (Una nini ewe Amru?), Amru akasema: Nimetaka nikupe sharti, Mtume akasema: (Unaweka sharti la

157_ "Badaaiu Swanaaii" Vol. 2، Uk. 118.
158_ "Al Mugh'niy" Vol. 5، Uk. 6.

nini?). Nikasema: Nataka nisamehewe madhambi yangu, Mtume rehma na amani ziwe juu yake akasema: (Kwani hukufahamu ya kwamba uislamu unafuta madhambi yote yaliyo tangulia, na mtu kuhama kutoka Makka kwenda Madina anasamehewa madhambi yake, na kufanya Hijja mtu anasamehewa madhambi aliyofanya kabla?).[159]

2. Aliyeenda Hijja anarudi akiwa hana madhambi kama siku aliyo zaliwa na mama yake:

Kutoka kwa Abuu Hureyra radhi za Allah ziwe juu yake alisema: Alisema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Mwenye kuhiji kisha akawa hakufanya upuuzi wala uovu, atarudi nyumabani kwake kama aliyo zaliwa na mama yake).[160]

3. Hijja ni katika aina bora za Jihadi:

Kutoka kwa Aisha radhi za Allah ziwe juu yake alisema: Nilisema: Ewe Mjumbe wa Allah! Jihadi ndiyo ibada bora unaonaje tukapigana Jihadi? Mtume akajibu akasema: (Hapana! Jihadi bora ni Hijja iliyo takasika).[161]

---

159_ "Sahihi Muslim" Vol. 1، Uk. 78.
160_ "Sahihi Bukhary" Vol. 2، Uk. 164. Na "Sahihi Muslim" Vol. 3، Uk. 107.
161_ "Sahihi Bukhary" Vol. 2، Uk. 164.

4. Ni kufaulu kwa kupata Pepo:

Kutoka kwa Abuu Hureyra radhi za Allah ziwe juu yake alisema: Alisema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (…Na Hijja iliyo takasika haina malipo isipokuwa ni Pepo).[162]

Malengo Ya Hijja

Allah Mtukufu ameifaradhisha Hijja kwasababu ya malengo makubwa, na lau tukitaka kuhesabu malengo hayo hatuwezi, lakini tutataja baadhi ya malengo, na miongoni mwa hayo:

1. Hijja ndani yake kuna kutekeleza amri za Allah na kuitika wito wake, kutekeleza na kuitika huko ni kudhihirisha utii na dini ya kweli.

2. Hijja ina mafungamano na Ufunuo (Wah'yi), kwasababu nyumba takatifu ndiyo sehemu ulipo teremka Ufunuo, na waislamu kila wanapofika katika maeneo hayo matukufu ndivyo wanavyozidi karibu na kizazi kulichoisha na Mtume rehma na amani ziwe juu yake, kizazi kilicho

162_ "Sahihi Muslim" Vol. 3, Uk. 107.

pigana Jihadi katika njia ya Allah na kufikisha sheria yake.

3. Katika kuna tangazo la vitendo baina ya watu juu usawa, na hilo linadhihiri pindi watu wanapo simama sehem moja katika viwanja vya Arafah, huwezi kuona tofauti baina yao.

4. Katika Hijja kunathibiti ibada ya watu kujuana na kusaidiana, kiasi kwamba watu wanajuana na kushauriana pamoja na kubadilishana mawazo, na jambo hilo linaufanya umma uendelee na kuufanya kuwa juu katika ngazi za utawala.

Sharti Za Hijja

Hijja ina masharti matano:

1. Uislamu: Haiswihi Hijja kwa mtu kafiri, kwasababu imepangilia kwamba ili mtu afanye ibada ni lazima atamke shahada mbili (awe muislamu).

2. Kuwa Na Akili: Ibada haiswihi kwa mwendawazimu, kwasababu akili ni sharti la kufanya ibada, na mwendawazimu hana akili kwa maana hiyo ibada siyo wajibu kwake.

3. Kubaleghe: Mtoto mdogo ambaye hajabaleghe halazimishwi kufanya Hijja, na akihiji basi hija yake ni sahihi, isipokuwa Hijja hiyo haitoshelezi kuwa ametimiza nguzo ya uislamu.

4. Uhuru: Kuwa mtumwa kunaondoa uwajibu wa kuhiji, lakini mtumwa akihiji Hijja yake ni sahihi.[163]

5. Uwezo: Miongoni mwa sharti za uwajibu wa Hijja ni mtu kuwa na uwezo, kama alivysema Allah Mtukufu: {**Na kwa ajili ya Mwenyezi Mungu imewajibikia watu wahiji kwenye Nyumba hiyo, kwa yule awezae njia ya kwendea**}. [Al Imraan: 97].

Uwezo Umegawanyika Sehem Mbili.[164]

Kigawanyo cha kwanza wanashirikiana wanaume na wanawake, na kigawanyo cha pili ni wanawake peke yao.

(a) Wanaume na wanawake wanashirikiana katika mambo manne:

1. Uwezo wa safari na matumizi.

2. Afya ya kimwili.

163_ "Al Mugh'niy" Vol. 5. Uk. 44. Na "Sunanu Tirmidhiy" Vol. 3، Uk. 266.
164_ "Kitaabul Hajji" cha Abdallah Al Twayyaar، Uk. 35.

3. Amani katika safari.

4. Uwezekano wa kusafiri.

(b) Mambo yanayo wahusu wanawake peke yao nayo ni mawili:

1. Kuwa na mahrim.

2. Mwanamke asiwe katika Eda.[165]

Mipaka Ya Hijja

Mipaka ya Hijja maana yake: Ni sehemu ambazo muislamu anaanzia ibada ya Hijja au Umrah pamoja na kuhirimia.

Nyakati na mipaka aliyo iweka Allah kwa ajili ya Hijja na Umrah ipo aina mbili:

1. Muda maalum wa utekelezaji wa Hijja:

Na muda unaanzia mwezi wa Shawwaali (mfungo mosi) mpaka siku ya kumi ya Dhul Hijj (mfungo tatu), amesema Allah Mtukufu: {**Hija ni miezi maalumu. Na anaye kusudia kufanya Hija katika miezi hiyo,**

165_ "Shuruutwul Istitwaah Fiy Ahkaamil Qur;an" Vol. 1، Uk. 288. Na "Al Jaamiu Liahkaamil Qur'an" Vol. 4، Uk. 184. Na "Adhw'waaul Bayaani" Vol. 5، Uk. 74.

**basi asiseme maneno machafu wala asifanye vitendo vichafu wala asibishane katika Hija**}. [Al Baqara: 197].

Ama ibada ya Umrah haina wakati maalum, muislamu anaweza kufanya ibada ya Umrah muda wowote anaotaka.

2. Mipaka na sehem za kuhirimia:

Na makusudio ya mipaka: Ni sehem ambazo haijuzu kwa mweye kuhiji au kufanya Umrah kuzivuka sehemu hizo na kuingia katika mji wa Makka bila ya kuhirimia, na mipaka hiyo ni:

**1- Dhul Huleyfah:** Nao ni mpaka wa watu wa Madina.

**2- Al Juhfah:**Nao ni mpaka wa watu wa Sham, Misri na Morocco.

**3- Qarnul Manaazil:** Nao ni mpaka wa watu wa Najdi, na kwa sasa unaitwa: Assaylul Kabiir.

**4-Yalamlam:** Nao ni mpaka wa watu wa Yemen.

**5. Dhaatu I'rqi:** Nao ni mpaka wa watu wa Iraqi na watu wa Mashariki (watu wa Khurrassaani).

Baadhi Ya Mambo Muhimu Kuhusu Mipaka Ya Hijja

1. Katika mipaka iliyo tajwa wanahirimia watu wa maeneo yaliyo tajwa na wanaopitaitia hapo kutoka katika maeneo mengine ikiwa wanaenda kufanya Hijja au Umrah.

2. Wale ambao makazi yao yapo ndani ya mipaka iliyo tajwa, wakitaka kuhiji au kufanya Umrah, wanahirimia katika majumba yao, na mwenye kuhiji katika watu wa Makka wanahirimia wakiwa makwao, na hawahiji kutoka kwenda katika mipaka kwa ajili ya kuhirimia, ama wakihitaji kufanya Umrah watatoka kwenda katika mpaka ulio karibu kwa ajili ya kuhirimia.

3. Mwenye kusafiri kwa ndege atahirimia pindi ndege inapofika usawa wa moja ya mipaka hiyo wakiwa angani, ni makosa kuchelewesha kuhirimia mpaka ndege itakafika Jidda kama wanavyofanya baadhi ya Mahujaji, kwasababu Jidda siyo mpaka wala siyo sehem ya kuhirimia, mwenye kufanya hivo atakuwa ameacha jambo la wajibu na anatakiwa kutoa fidia.

4. Mwenye kuvuka mpaka bila ya kuvaa ihram analazimika kurudi katika mpaka na kuhirimia, kwasababu ni jambo la wajibu na anaweza kulifanya, na kama hakurudi

basi atatoa fidia.

Ibada Ya Hijja Na Nguzo Zake

1- Kuhirimia

Kuhirimia ni nguzo ya kwanza miongoni mwa nguzo za Hijja, na maana yake ni kuweka niya ya kuingia katika ibada ya Hijja, na imeitwa kuhirimia kwasababu muislamu anajiharamishia mwenyewe yale yaliyokuwa halali kwake kabla hajaingia katika ihram, ikiwemo kuoa, kupaka marashi, kunyoa nywele na baadhi ya mavazi.

Aina Za Kuhirimia: Kuhirimia kupo aina tatu:

1. Tamattuu: Maana yake ni kunuiya kufanya ibada ya Umrah pekee katika miezi ya Hijja, kisha akimaliza kufanya Umrah anakuwa huru, na tarehe za kuhiji zikifika atanuiya kuingia katika ibada ya Hijja.

Na namna ya kuta niya mwanzo wa ibada hii ni kusema: "Labayka Umrah mutamattian biha ilal Hajji".

2. Qiraan: Nayo ni kutekeleza Hijja na Umrah kwa pamoja na kwa niya moja na safari moja, na katika kutia niya atasema: "Labayka Umrah wa Hajjan".

3. Ifraad: Nayo ni kunuiya kutekeleza ibada ya Hijja pekee, na atanuiya kwa kusema: “Labayka Hajjan”.

Tanbiihi

Ni wajibu kwa mwenye kuhiji Tamattuu na Qiraan kuchinja mnyama, ama mwenye kufanya Ifraad halazimiki kuchinja.

Mambo Ya Wajibu Kwa Mwenye Kuhirimia

Kuhirimia kuna mambo ya wajibu yanayo wahusu wanaume, ama kwa wanawake ni wajibu kwao jambo moja, na mambo hayo ya wajibu ni kama ifuatavyo:

1. Kuhirimia katika mipaka, kwasababu Mtume rehma na amani ziwe juu yake aliamrisha jambo hilo kwa wanaume na wanawake.

Na mwenye kuacha kuhirimia (kutia niya ya ibada ya Hijja) katika mipaka iliyowekwa, ni wajibu kwake kuchinja, hana fidia nyingine.

2. Nikuvaa ihram kwa wanaume.

Ifahamike ya kwamba mwanaume mwenye kuhiji

akipita katika mpaka na nguo za kawaida zisizokuwa iharam, itampasa kutoa fidia, na fidia hiyo mtu ana hiyari ya kufanya moja ya mambo matatu:

(a) Kufunga siku tatu.

(b) Kuwalisha masikini sita.

(c) Kuchinja mnyama, mbuzi au kondoo kisha kugawa nyama kwa masikini wa Makka.

Sunna Za Ihram

1. Kuoga: Yeyote mwenye kutaka kuhirimia inapendekezwa kuoga hata kama ana hedhi au nifasi.

2. Kukata kucha na kuondoa nywele za kwapani, na kupunguza sharubu na kunyoa nywele sehem za siri pamoja na kupaka manukato kabla ya kuhirimia.

3. Kuvaa shuka mbili nyeupe chini na juu.

4. Kufanya talbiyah (kusema: Labayka Allahuma labayka..), kuazia baada ya kuhirimia mpaka atakapo anza twawaafu.

5. Kuhirimia baada ya swala, na ni bora ikawa swala ya faradhi.[166]

Mambo Yasiyofaa Kwa Mwenye Kuhirimia

(a) Mambo ya haramu kwa wanaume na wanawake:

1. Kunyoa nywele kichwani na mwili mzima.

2. Kukata kucha za mikononi na miguuni.

3. Kupaka manukato nguoni na mwilini.

4. Kufanya tendo la ndoa na vinavyo sababisha tendo hilo, kama vile kufunga ndoa, kumtazama mwanamke kwa matamanio na mfano wa hayo.

5. Kuvaa gloves mikononi.

6. Kuua mnyama anaewindwa.

(b) Mambo yaliyo ya haramu kwa wanaume pekee:

1. Kuvaa nguo zilizo shonwa, kama vile kanzu, shati na suruali.

2. Kufunika kichwa kwa kuvaa kilemba, kofia na mfano wake.

166. "Sharhil Idhwaahi" cha Imamun Nawawiy, Uk. 145.

(c) Mambo yaliyo ya harammu kwa wanawake pekee:

Ni haramu kwa mwanamke kufunika uso wake kwa niqabu au mfano wake, na akitaka kufunika uso wake basi afunike kwa ushungi.[167]

Al Talbiyah

**Maana Ya Talbiyah:** Ni Sunna kuleta Talbiyah baada ya kuhirimia, na mwisho wake ni pindi anapoanza kufanya Twawaafu. Mwenye kufanya Hijja au Umrah akisha maliza kuhirimia ataanza kuleta talbiyah, nayo ni kusema: "Labayka Allahuma labayka, labayka laa shariika laka labayka, innal hamda wa nneemata laka wal Mulku laa shariika laka".

**Hukumu ya maneno hayo:**

2- Kufanya Twawaafu

**Maana Yake:** Kufanya Twawaafu ni kuizunguka Al Kaaba mara saba kwa niya ya kumuabudu Allah, anaanzia upande wa Hajarul As'wadi (Jiwe jeusi), na anaishia hapo, na anaefanya Twawaafu Al Kaaba inakuwa upande

167_ "Badaaiu Swanaaii" Vol. 3، Uk. 183. Na "Bidaayatul Mujtahidi" Vol. 4، Uk. 375. "Al Majmuu" Vol. 6، Uk. 249. Na "Al Mugh'niy" Vol. 5، Uk. 53.

wake wa kushoto.

**Hukumu Ya Twawaafu:** Twawaafu ina aina tofauti na hukumu zake ni tofauti:

1. Twawaafu ya kufika Makka: Hukumu ya Twawaafu hiyo ni Sunna kwa mwenye kuingia katika Msikiti mtukufu wa Makka.

2. Twawaafu ya Umrah na Twawaafu ya Hijja: Zote mbili ni nguzo katika nguzo za Hijja na Umrah.

3. Twawaafu ya kuaga: Twawaafu hiyo ni wajibu miongoni mwa mambo ya wajibu ya Hijja.

Sharti Za Kutufu

1. Niya ya kuingia katika Twawaafu.

2. Kujitwaharisha kutokana na hadathi na uchafu.

3. Kusitiri uchi.

4. Kutufu nadani ya Msikiti.

5. Twawaafu iwe ni kuizunguka Alkaaba.

6. Alkaaba iwe upande wake wa kushoto.

7. Aanzie usawa wa Hajaril As'wadi (Jiwe jeusi), akianzia sehem tofauti na hiyo Twawaafu yake haiswihi, na akianzia kabla ya Jiwe jeusi itaanza kuhesabika akifika usawa wa Jiwe jeusi.

8. Azunguke mara saba.

9. Afuatanishe mzunguko baada ya mwingine, isipokuwa kwa dharura, kama vile swala au kuchoka.

Sunna Za Twawaafu:

1. Kutembe kwa haraka wakati wa kutufu katika mizunguko mitatu ya mwanzo, na hiyo ni Sunna kwa wanaume katikaTwawaafu ya kuingia Makka.

2. Inatakiwa bega la kulia liwe wazi wakati wa kufanya Twawaafu.

3. Kubusu Hajaril Asw'adi (Jiwe jeusi).

4. Kutokuzungumza wakati wa kutufu isipokuwa kwa dharura.

5. Kuomba dua na kufanya dhikri na mfano wa hayo.

6. Kuigusa Ruknul Yamaani, na kutokuibusu.

7. Kuswali rakaa mbili baada ya kumaliza Twawaafu.

8. Kunywa maji ya Zamzam baada kuswali rakaa mbili.

3- Kufanya Saayi Baina Ya Swafaa Na Mar'wa

**Hukumu Yake:** Kufanya Saayi ni nguzo katika nguzo za Hijja, na Hijja haikamiliki bila ya kufanya Saayi.

Sharti Za Kufanya Saayi:

1. Saayi ifanyike baada ya Twawaafu.

2. Ni mpangilio, mtu anaanzia Swafaa na kumalizia Mar'wa.

3. Saayi iwe ni mara saba.

4- Kusimama Katika Viwanja Vya Arafah

**Hukumu yake:** Ni nguzo miongoni mwa nguzo za Hijja, na haikamiliki Hijja isipokuwa kwa mtu kusimama Arafah, amesema Mtume rehma na amani ziwe juu yake: (Hijja ni Arafah).[168]

Hukumu Ya Mtu Aliyepitwa Na Kisimamo Cha Arafah

Mwenye kupitwa na kisimamo cha Arafah atahalalika

168_ "Swahihi Sunani Abii Daud" Vol. 1، Uk. 367.

kwa kufanya Umrah, maana yake ni kwamba Hijja yake itageuka kuwa Umrah, na yataporomoka kwake matendo yote ya Hijja, kama vile kusimama Arafah, kulala Muzdalifah, kulala Mina na kurusha mawe, na badala yake mtu huyo atafanya Twawaafu, Saayi na kunyoa nywele au kupunguza, na atawajibika kuilipa Hijja iliyompita hata kama ilikuwa ni Hijja isiyo ya wajibu kwake, na atatakiwa kuchinja mnyama, na kama hakupata kichinjwa atafunga siku tatu akiwa Makka na siku saba akirejea katika mji wake.

Baadhi Ya Mambo Yanayo Ambatana Na Kisimamo Cha Arafah

1. Mwenye kuondoka Arafah kabla ya kuzama jua atalazimika kutoa fidia kwasababu ameacha jambo la wajibu.

2. Mwenye kuchelewa kwenda Arafah akasimama katika viwanja hivyo usiku mtu huyo hana fidia yoyote, kwasababu ana udhuru.

3. Inafaa kusimama Arafah kwa mwenye hedhi na nifasi na mwenye hadathi, kwasababu kuwa twahara siyo

sharti la kusimama Arafah.

5- Kulala Muzdalifah

**Hukumu Yake:** Kulala Muzdalifah ni wajibu miongoni mwa mambo ya wajibu ya Hijja, na mwenye kuacha kulala Muzdalifah atalazimika kulipa fidia.[169]

Hukumu Ya Mwenye Kuacha Kulala Muzdalifah

Mwenye kuacha kulala Muzdalifah kwa udhuru kama vile mtu aliyeenda kusimama Arafah usiku mtu huyo hana fidia yoyote na Hijja yake ni sahihi.

Na akiacha kulala Muzdalifah bila ya udhuru atalazimika kulipa fidia, na hiyo ndiyo kauli jamuhuri ya Wanachuoni.

**6- Kurusha Mwe**[170]

**Hukumu Yake:** Jamuhuri ya Wanachuoni wamesema kuwa kurusha mawe Jamaraati ni wajibu, na mwenye kuacha atawajibika kutoa fidia.

Muda Wa Kurusha Mawe

169_ “Badaaiu Swanaaii” Vol. 2، Uk. 135. Na “Al Muqnii” Vol. 1، Uk. 469.
170_ “Adhw’waaul Bayaani” Vol. 5، Uk. 588. Na “Kashaaful Qinaai” Vol. 2، Uk. 498. Na “Haashiyatu Ibn A’bidiina” Vol. 2، Uk. 513. “Al Nihaayah” Vol. 1، Uk. 292.

Ama nguzo kubwa (Jamratul Aqabah) mwanzo wa kurusha mawe ni baada ya kuchomoza jua siku ya Iddi, muda huo unaendelea mpaka jua linapo zama, na hiyo kwa wale wasiokuwa na udhuru, ama watu wenye udhuru kurusha mawe kunaanza tangu mwezi unapozama usiku wa kuamkia Iddi.

Ama kuhusu siku tatu za Tash'riiq, kurusha mawe kunaanza baada ya kupinduka kwa jua (mwanzo wa muda wa adhuhuri) mapaka kuzama jua, na haifai kurusha mawe kabla ya muda huo.

Na inajuzu kurusha mawe usiku wa kuamkia siku ya Iddi, na vilevile katika siku mbili za Tash'riiq, kutokana na msongamano wa watu, na hiyo ndiyo fat'wa ya Wanachuoni wa sasa.

Sharti Za Kurusha Mawe

1. Ni kurusha mawe saba kwa kila nguzo.

2. Kurusha mawe mara saba, na akirusha yote saba kwa mara moja au mara mbili inahesabika ni jiwe moja.

3. Ni sharti yawe mawe madogo madogo, ama kurusha

kisichokuwa mawe haifai.

4. Ahakikishe jiwe alilorusha lidondoke katika nguzo.

5. Mpangilio katika kurusha mawe, aanze katika nguzo ndogo ya mwanzo kisha nguzo ya katikati na atamalizia katika nguzo kubwa ya mwisho.

Hukumu Ya Kumuwakilisha Mtu Kurusha Mawe

(a) Inafaa kwa msimamizi wa mtoto mdogo kumrushia mawe akikhofia msongamano wa watu.

(b) Inafaa kwa asiyeweza kurusha mawe kwasababu ya uzee, ugonjwa, mimba na mfano wa hayo, kumuwakilisha mtu wa kumrushia mawe kwa sharti la aliye wakilishwa awe ni katika mahujaji.[171]

Kunyoa Nywele Au Kupunguza

**Hukumu yake:** Ni wajibu miongoni mwa mambo ya wajibu katika Hijja, na ikiwa mtu hakunyoa nywele au kupunguza itamlazim kutoa fidia ya kuchinja mnyama, amesema Allah Mtukufu: {**Bila ya shaka nyinyi mtauingia Msikiti Mtakatifu, Inshallah, kwa amani, na**

171_ "Kitaabul Hajji" Uk. 117.

**hali mmenyoa vichwa vyenu na mmepunguza nywele. Hamtakuwa na khofu**}. [Al Fat'hi: 27].

Muda Wa Kunyoa Nywele

Kunyoa nywele kunaanza siku ya kuchinja mpaka mwisho wa siku za Tash'riiq, na inajuzu kucheleweshа kunyoa mpaka siku ya mwisho ya Tash'riiq.

Baadhi Ya Mambo Muhimu Katika Kunyoa Nywele Au Kupunguza

1. Wanachuoni wamekubaliana ya kwamba inafaa kunyoa au kupunguza, na kufanya moja ya hayo inatosha katika ibada ya Hijja.

2. Wanachuoni wamekubaliana ya kwamba kunyoa ni bora kuliko kupunguza, isipokuwa kwa mwenye kuhiji Hijja ya Tamattuu atapunguza nywele baada ya kufanya Umrah kisha atanyoa akimaliza Hijja.

3. Kauli sahihi zaidi ni kunyoa au kupunguza kichwa kizima, kwasababu kufanya hivo ndiyo kutekeleza ibada hiyo, na Mtume rehma na amani ziwe juu yake alinyoa kichwa kizima.

8- Kuchinja Mnyama

**Maana ya kuchinja mnyama:** Ni mnyama anayechinjwa na mwenye kufanya Hijja au Umrah kwa ajili ya kujikurubisha kwa Alla, wanyama hao ni ngamia, ng'ombe na kondoo au mbuzi.[172]

Vigawanyo Vya Wanyama

Wanyama wanaochinjwa wamegawanyika katika sehemu kuu mbili:

**(a) Ni mnyama anayechinjwa kwa ajili ya kumshukuru Allah:**Mnyama huyo ni wajibu kuchinjwa kwa mwenye kuhiji Hijja ya Tamattuu na Qiraan, kwa ajili ya kumshukuru Allah kwa kumuwezesha kutekeleza ibada ya tukufu ya Hijja.

**(b) Ni mnyama wa lazima:** Mnyama huyo anachinjwa kwa ajili ya kuziba pengo lililojitokeza kwa mwenye kuhiji au kufanya Umrah, kwasababu ya kuacha wajibu au kufanya mambo yaliyo haramishwa, au kuchinja kwa mtu aliyepata dharura inayomzuia kufanya Hijja hali ya kuwa amesafiri kwa ajili hiyo, ni kichinjwa hicho ni wajibu.

172- "Al Majmuu" Vol. 8, Uk. 268.

Na tofauti iliyopo katika kuchinja kwa kumshukuru Allah, na kuchinja kwa ajili ya kuziba mapungufu:

Aliyechinja kwa ajili ya kumshukuru Allah inafaa kula nyama ya alicho kichinja, ama aliyechinja kutokana na mapungufu haifai kula nyama ya alicho kichinja, na badala yake atagawa nyama hiyo kwa masikini wa Makka.

Sharti Zinazo Paswa Kukamilika Kwa Mnyama Anaechinjwa

1. Awe ni katika wanyama wanaoruhusiwa kuchinjwa kisheria, kama vile ngamia, ng'ombe na mbuzi au kondoo.

2. Mnyama awe amesalimika kutokana na aibu.

3. Wanyama wanaochinjwa wawe wametimiza miaka inayo ruhusiwa kisheria:

(a) Ngamia ni miaka mitano na kuendelea.

(b) Ng'ombe ni miaka miwili na kuendelea.

(c) Mbuzi ni mwaka mmoja na kuendelea.

(d) Kondoo ni miezi sita na kuendelea.

9- Kula Mina

**Hukumu ya kulala Mina:** Jamuhuru ya Wanachuoni wamekubaliana kuwa ni wajibu, namwenye kuacha kulala Mina siku zote au hata siku moja, atalazimika kutoa fidia.[173]

Watu Ambao Siyo Wajibu Kwao Kulala Mina

Mgonjwa na anaye muhudumia hawawajibiki kulala Mina, vilvile wafanyakazi rasmi wanao simamia mambo ya Hijja, na hilo linapangwa na jopo la Wanachuoni.

**Makusudio ya kulala Mina:** Ni mwenye kuhiji kulala Mina kuanzia tarehe kumi na moja mpaka tarehe kumi na mbili kwa mwenye kutaka kufanya haraka, na tarehe kumi na tatu ni kwa asiyekuwa na haraka.

## Makaosa Wanayofanya Baadhi Ya Mahujaji[174]

Yafuatayo ni makosa yanayofanywa na baadhi ya Mahujaji:

1. Ni mtu kukusudia katika Hijja yake kufanya biashara au kujionyesha au kujifakharisha.

2. Ni mwanamke kusafiri bila ya Mahrim, na hilo

173_ "Al Hidaayah" Vol. 1، Uk. 149. Na "Al Mugh'niy" Vol. 5، Uk. 325. Na "Zaadul Maadi" Vol. 2، Uk. 285.

١٧٤ _ "Kitaabul Hajji" cha Abdallah Al Twayyaar، Uk. ١٥٥.

linatokea sana kwa wanawake wanaofanya kazi za ndani nchini Saudia wanakuja bila mahrim na msimu wa Hijja wanaenda Makka kuhiji, vilevile baadhi ya mashirika wanaopeleka watu Hijja huchukua wanawake bila ya mahrim, na hilo ni kosa kubwa.

3. Kusafiri na vitu ambavyo ni haramu, kama vile camera na ala za miziki, utaona baadhi ya mahujaji akishavaa ihram anajipiga picha kisha anairusha katika mitandao ya kijamii, na hilo ni kosa la wazi.

4. Baadhi ya mahujaji wanaitakidi kwamba haijuzu kuvaa viatu vilivyo wazi, miwani, saa na mfano wa mengineyo, na hilo pia ni kosa, lililo sahihi ni kwamba hakuna tatizo mtu kuvaa vitu hivyo.

5. Baadhi ya mahujaji wanadhani ya kwamba kuingia katika ibada ya Hijja kunaanza baada ya kuvaa ihram, kwahiyo anajizuia kufanya yaliyo katazwa baada ya kuvaa ihram na hilo ni kosa, jambo lililo sahihi ni kwamba mwenye kufanya Hijja anatakiwa kujizuia kutokana na makatazo baada ya kunuiya (kuhirimia), na siyo baada ya kuvaa iharam.

6. Baadhi ya mahujaji wanajilazimisha kuomba dua maalum wakati wa kufanya Twawaafu wakiwa kwa pamoja au mmoja mmoja na hilo ni kosa, hakuna dua maalum ya kuomba katika Twawaafu.

7. Katika Al Kaabah kuna sehemu inaitwa Ruknul Yamaani, baadhi ya mahujaji wanaibusu sehemu hiyo na hilo ni kosa, Ruknul Yamaani inaguswa tu ikiwa kuna wepesi kutokana na msongamano, na kama hakuna uwezekano basi atapita tu bila kuashiria chochote.

8. Wakati wa msongamano mkali baadhi ya mahujaji wanaingia sehem inayoitwa Hijri Ismail, na wanaofanya hivo wanakuwa hawajatimiza Twawaafu, kwasababu sehemu hiyo ipo ndani ya Alkaaba.

9. Baadhi ya mahujaji wakimaliza Twawaafu hawafuniki bega la kulia mpaka wanamaliza ibada na hilo ni kosa, anatakiwa afunike bega pindi anapomaliza kutufu.

10. Baadhi ya mahujaji wanadhani ya kwamba rakaa mbili za Twawaafu ni mtu aswali nyuma ya Maqaamu Ibrahim nalo pia ni kosa, bali rakaa mbili hizo zinaswali mahala popote ndani ya Msikiti wa Makka, haitakiwi

kuwaudhi wenzake kwa kulazimisha kuswali nyuma ya Maqaamu Ibrahim.

Umrah Na Hukumu Zake

**Maana Ya Umrah:** Ni kumuabudu Allah kwa kufanya mambo yafuatayo:

(a) Twawaafu.

(b) Kufanya Saayi baina ya Swafaa na Mar'wa.

(c) Kunyoa nywele au kupunguza.[175]

Hukumu Ya Umrah

Umrah ni wajibu kulingana na kauli za Wanachuoni.[176]

Kutokana na hadithi ya Aisha radhi za Allah ziwe juu yake pindi alipomuuliza Mtume rehma na amani ziwe juu yake: Je inafaa kwa wanawake kupigana Jihadi? Mtumre akajibu kwa kusema: (Ndiyo! Mwanamke ana Jihadi isiyokuwa na mapigano, nayo ni Hijja na Umrah).[177]

---

175_ "Al Mumtii Sharhu Zaadil Mustaqnii" cha Shekh Ibn Utheymiin، Vol. 7، Uk. 8.
176_ "Al Mugh'niy" Vol. 5، Uk. 13. Na "Raudhwatu Twaalibiina" Vol. 3، Uk. 17.
177_ "Musnadi Imamu Ahmad" Vol. 6، Uk. 71،165. Na "Sunanu Nasaai" Vol. 5، Uk. 86. Na "Al Ir'waau" Vol. 4، Uk. 151.

Sifa Za Umrah

Muislamu anapotaka kufanya Umrah anatakiwa afanye mambo yafuatayo:

1. Aoge na aondoe nywele za kwapani pamoja na nywele za sehemu ya siri, na ajipake manukato, na hiyo ni Sunna kwa wanaume na wanawake, inafaa pia hata kwa wanawake wenye hedhi na nifasi.

2. Ni Sunna pia kuswali rakaa mbili.

3. Atahirimia kwa kusema: “Labayka Umrah”.

4. Baada ya kuhirimia ataanza kuleta Talbiyah ambayo ni kusema: “Labayka Allahuma labayka, labayka laa shariika laka labayka, innal hamda wanneemata laka wal mulku laa shariika laka”, kwa wanaume watasema maneno hayo kwa sauti, na kwa wanawake watasema bila ya kuinua sauti zao.

5. Anaetaka kuhirimia akiwa na khofu ataweka sharti katika kuhirimia kwa kusema: “Nikipata dharura ya kunizuia kufika Makka nitakatisha ibada”.

6. Anapofika katika Msikiti mtukufu wa Makka

ataingia kwa kutanguliza mguu wa kulia huku akisema: “Bismi LLahi wasswalaatu wassalaam alaa Rasuuli LLah, Allahuma ghufirliy dhunuubiy waf tahliy abuwaaba rahmatika”

Maana yake: Kwa jina la Allah na rehma na amani ziwe juu ya Mtume wa Allah, ewe Allah nisamehe madhambi yangu na unifungulie milango ya rehma zako.

7. Kisha ataenda kuanza Twawaafu, na ataanza kwa kuligusa Jiwe jeusi (Hajarul As’wadi) na kulibusu ikiwa itakuwa ni rahisi kwake, na kama itamuwea vigumu ataashiria kwa mkono wake wa kulia na atasema: Allahu Akbaru.

Maana yake: Allah ni mkubwa.

8. Kwa muda atakaokuwa katika Twawaafu anatakiwa amtaje sana Allah na amuombe kwa chochote anachotaka.

9. Atakapofika upande wa Ruknul Yamaani atapagusa ikiwa itakuwa ni rahisi kwake kufanya hivo, na kama itamuwea vigumu atapita bila ya kuashiria chochote.

10. Anayefanya Umrah wakati wa kutufu bega lake la

kulia linatakiwa liwe wazi, na hiyo ni kwa Twawaafu ya Umrah au Twawaafu ya mwenye kuhiji akiingia Makka.

11. Katika kufanya Twawaafu atatembea haraka katika mizunguko mitatu ya mwanzo ikiwa kufanya hivo hakuta waudhi wenzie.

12. Akimaliza kufanya Twawaafu ataelekea Maqaamu Ibrahim na kuswali rakaa mbili.

13. Kisha ataelekea sehemu ya kufanya Saayi, na takapo karibia Swafaa atasoma Aya ifuatayo: {**Hakika vilima vya Safaa na Marwa ni katika alama za Mwenyezi Mungu. Basi anaye hiji kwenye Nyumba hiyo au akafanya Umra, si kosa kwake kuvizunguka. Na anaye jitendea mwenyewe kheri basi bila ya shaka Mwenyezi Mungu ni Mwenye shukrani na Mjuzi**}. [Al Baqara: 158], kisha atapanda mpaka afike katika kilele cha mlima wa Swafaa sehemu ambayo anaiona Alkaaba, ataielekea Alkaaba na atainua mikono yake na kumshukuru Allah, kisha amuombe anachotaka.

14. Atakapo maliza dua atateremka na kuelekea Mar'wa, akifika katika alama za kijani atakimbia kadri ya

uwezo wake mpaka mwisho wa alama bila ya kuwaudhi wenzie, kisha atatembea mpaka Mar'wa, na akiwa Mar'wa atafanya kama alivyofanya akiwa Swafaa.

15. Atakapo maliza mizunguko saba atanyoa nywele au kupunguza, lakini kwa mwanamke atapunguza kidogo katika ncha za nywele zake.

16. Kwa kufanya hayo Umrah yake itakuwa imekamilika.

Nguzo Za Umrah

Umrah ina nguzo tatu:

1. Kuhirimia.

2. Kufanya Twawaafu.

3. Kufanya Saayi baina ya Swafaa na Mar'wa.

Mambo Ya Wajibu Kati Umra

1. Kuhirimia katika mipaka.

2. Kunyoa nywele au kupunguza.

| | |
|---|---|
| Matunda Ya Kuamini Vitabu | |
| 4- Kuamini Mitume | |
| Mitume ni akina nani?: | |
| Kuamini Mitume Kuna Ambatana Na Mambo Yafuatayo: | |
| 5- Kuamini Siku Ya Mwisho | |
| Makusudio ya siku ya mwisho: | |
| Kuamini Siku Ya Mwisho Kuna Ambatana Na Mambo Yafuatayo: | |
| Kuamini Siku Ya Mwisho Kuna Ambatana Na Kuamini yote yanayokuwa baada ya kufa, kama vile: | |
| Matunda Ya Kuamini Siku Ya Mwisho | |
| 6- Kuamini Qadari | |
| Maana ya uamini Qadar: | |
| Kuamini Qadari Kuna Ambatana Na Mambom Yafuatayo | |
| Umuhimu Wa Itikadi Sahihi | |
| Kutilia Umuhimu Itikadi Sahihi | |
| Malengo Ya Itikadi Sahihi Ya Kiislamu | |
| Kupenda Na Kuchukia Kwa Ajili Ya Allah | |
| yafuatayo: | |

| | |
|---|---|
| Umuhimu wa kupenda na kuchukia kwa ajili ya Allah katika itikadi ya Uislamu: | |
| Mifano Ya Kuwapenda Makafiri: | |
| Somo La Pili: Shirki Na Vigawanyo Vyake | |
| Shirki Na Vigawanyo Vyake | |
| Maana ya shirki: | |
| 1- Shirki Kubwa | |
| Maana ya shirki kubwa: | |
| Shirki Kubwa Na Hatari Zake | |
| Shirki Kubwa Na Aina Zake | |
| 1. Shirki Ya Ibada: | |
| 2. Shirki Katika Mapenzi: | |
| 3. Shirki Katika Matamanio: | |
| 4. Shirki Katika Twaa: | |
| Shirki Ndogo Na Aina Zake | |
| Aina Za Shirki Ndogo: | |
| Shirki Kubwa Na Hatari Zake | |
| Vigawanyo Vya Shirki Ndogo | |

| | |
|---|---|
| Tofauti Kati Ya Shirki Kubwa Na Shirki Ndogo | |
| Kuyazuru Makaburi | |
| Vigawanyo Vya Kuzuru Makaburi | |
| (a) Kuzuru makaburi kuliko ruhusiwa kisheria: | |
| (b) Kuzuru ambako ni bidaa: | |
| (c) Kuzuru ambako ni shirki: | |
| Unafiki Na Aina Zake | |
| Unafiki maana yake: | |
| Aina Za Unafiki | |
| Uchawi Na Viini Macho Na Mengineyo | |
| 1- Ukweli Kuhusu Uchawi: | |
| 2- Je! Uchawi Unaathiri? | |
| 3- Madhara Ya Uchawi Kwa Jamii Nzima Na Mtu Mmoja Mmoja | |
| 4- Hukumu Ya Uchawi Na Wachawi | |
| 5- Vipi Utaikinga Nafsi Yako Kutokana Na Uchawi? | |
| Somo La Tatu: Shahada Mbili | |
| Shahada Mbili | |

| | |
|---|---|
| Elimu ya tauhidi: | |
| Maana Ya Uislamu | |
| Haki Ya Allah Kwa Waja Wake | |
| Maana Ya Ibada | |
| Aina Za Tauhidi | |
| Aina Ya Kwanza:Ni tauhidi katika elimu na itikadi | |
| Aina Ya Pili: Ni tauhidi katika utashi na makusudio | |
| Aina Tatu Za Tauhidi | |
| 1. Tauhidi Ya Uungu. | |
| 2. Tauhidi Ya Ibada. | |
| 3. Tauhidi Ya Majina Ya Allah Na Sifa Zake. | |
| Tauhidi Athari Zake Na Ubora Katika Ibada | |
| Maana Ya Laa Ilaaha Ila ALLah | |
| Maana Ya Kushuhudia Ya Kwamba Muhammad Rehma Na Amani Ziwe Juu Yake Ni Mjumbe Wa Allah | |
| Ibada | |
| Ibada ambayo ni sababu ya kuumbwa wanadamu | |
| Masharti Ya Ibada | |

| | |
|---|---|
| Misingi Ya Ibada62 | |
| Somo La Nne: Swala | |
| Twahara | |
| Hukumu Yake: | |
| Aina Zake: | |
| Kukidhi Haja(Kujisaidia) Na Adabu Zake:66 | |
| Udhu68 | |
| Maana Ya Udhu | |
| Dalili Yake | |
| Fadhila Za Udhu: | |
| Faradhi Za Udhu | |
| Sunna Za Udhu | |
| Yasiyo Pendeza (Yasiyofaa) Katika Udhu | |
| Namna Ya Kutawadha | |
| Ya Pili: Udhu ulio kamili | |
| Vitenguzi Vya Udhu | |
| Tanbiihi: Mambo Muhimu Yanayo Paswa Kuyataja | |

| | |
|---|---|
| Kupaka Juu Ya Khof Mbili | |
| Kuoga | |
| Vinavyo Wajibisha Kuoga | |
| Namna Ya Kuoga | |
| Kutayammamu | |
| HedhiNa Nifasi Na Istihadhwa: | |
| Kwanza:Maana Ya Hedhi: | |
| Pili:Maana Ya Nifasi: | |
| Tatu: Maana Ya Istihadha: | |
| Nne: Baadhi ya Hukumu za Wenye Hedhi na Nifasi: | |
| Tano: Hali za mwenye Istihadhwa: | |
| Sita: Baadhi ya hukumu za Mwenye Istihadhwa: | |
| Swala | |
| Maana Ya Swala: | |
| Hukumu ya Mwenye kuiacha swala: | |
| Nguzo za Swala: | |
| Masharti ya Swala: | |

| | |
|---|---|
| Mambo Ya Wajibu Katika Swala: | |
| Sunna za Swala: | |
| Swala Ya Jamaa: | |
| Fadhila zake: | |
| Hukumu yake: | |
| Idadi Inayotakiwa Ili Kukubalika Jamaa: | |
| Nyudhuru Zinazo Ruhusiwa Kuacha Swala Ya Jamaa: | |
| Baadhi Ya HukumuZinazo Ambatana Na Maamuma: | |
| Baadhi YaHukumu Zinazo Ambatana Na Imamu: | |
| Swala Ya Mgonjwa: | |
| Swala Ya Ijumaa | |
| Hukumu yake: | |
| Je Swala Ya Ijumaa Ni Wajibu Juu Ya Nani? | |
| Hekima Ya Kuamrishwa Kuswali Ijumaa: | |
| Masharti Ya Kukubalika Swala Ya Ijumaa: | |
| Swala Za Iddi Mbili | |
| Hukumu yake: | |

| | |
|---|---|
| Muda Wake: | |
| Sehemu Ya Kuswaliwa Idd: | |
| Namna Yake: | |
| Swala Ya Kupatwa Kwa Jua Na Mwezi: | |
| Namna yake: | |
| Swala Ya Kuomba Mvua | |
| Hukumu Yake: | |
| Namna Yake: | |
| Swala Za Sunna: | |
| Swala Ya Jeneza | |
| Hukumu Yake: | |
| Sharti Zake: | |
| Nguzo Zake: | |
| Namna yake: | |
| Baadhi Ya mambo Muhimu Katika Swala Ya Jeneza | |
| Somo La Tano: Zaka | |
| Zaka | |

| | |
|---|---|
| Maana Ya Zaka: | |
| Umuhimu Wake Na Hekima Ya Kuwa NiSheria | |
| Dalili za Uwajibu Wa Zaka: | |
| Tofauti kati Ya ZakaNa Kodi: | |
| Je Kodi Inaweza Kutosheleza Kuliko Zaka? | |
| Masharti Ya Zaka: | |
| Hukumu Ya Anayezuia Zaka: | |
| Mali Ambazo Zimewajibishwa Na Sheria Kutolewa Zaka: | |
| Kutoa  Zaka Ya Dhahabu Na Fedha Kwa Pesa Za Kawaida: | |
| Kiwango cha Zaka kwa pesa za kawaida: | |
| Zaka Ya Wanyama | |
| Masharti ya zaka ya wanyama: | |
| Jeduwali Linalo Onyesha Viwango Vya Zaka Za Wanyama | |
| Zaka Ya Ngamia | |
| Zaka Ya Ngo’mbe: | |
| Zaka Ya Kondo/ Mbuzi: | |
| Mali Ya Biashara | |

| | |
|---|---|
| Maana yake: | |
| Masharti yake: | |
| Kiwango cha wajibu ndani ya mali ya biashara: | |
| Aina za mali za biashara: | |
| Zaka Ya Nafaka Na Matunda | |
| A- Vinavyotolewa: | |
| B- Kiwango chake: | |
| Uzinduo Juu Ya Zaka Ya Nafaka Na Matunda | |
| Mambo Muhimu Katika Zaka | |
| Zaka za Hisa na Mikataba ya kifedha ya riba: | |
| Jinsi ya kutoa zaka katika Hisana Mikataba ya kifedha ya riba: | |
| 1- Zaka ya Hisa: | |
| 2- Zaka ya Mikataba ya kifedha ya riba: | |
| Wanaopewa Zaka | |
| Makusudio yake: | |
| Kwanza: Mafakiri. | |
| Maana Ya Fakiri: | |

| | |
|---|---|
| Mas'ala muhimu Juu ya Fakiri: | |
| Pili: Masikini: | |
| Maana Ya Msikini: | |
| Tatu: Watendaji wake (Wanaosimamia ukusanyaji na ugawaji): | |
| Maana Yake: | |
| Nne: Wanao liwazwa nyoyo zao: | |
| Maana Yake: | |
| Tano: Watumwa: | |
| Aina Za Watumwa: | |
| Sita: Wenye Madeni: | |
| Maana Ya Wenye Madeni: | |
| Aina Za Wenye Madeni: | |
| Saba: Katika njia ya Allaah Mtukufu: | |
| Maana Yake: | |
| Nane: Msafiri: | |
| Maana Ya Wasafiri: | |
| Wasioruhusiwa Kupewa Zaka | |

| | |
|---|---|
| Zakaatul Fitri | |
| Hukumu yake: | |
| Hekima ya kuwekwa sheria yake: | |
| Muda wa kuitoa: | |
| Wanaopewa zakaatul fitri | |
| Je Zakaatul hii inawahusu mafakiri wa mji huo unaotolewa Zaka tu? | |
| Somo La Sita: Swaumu | |
| Swaum | |
| Maana Ya Swaum Katika Lugha Ya Kiarabu: | |
| Maana Ya Swaum Katika Sheria: | |
| Nafasi Ya Swaum Katika Uislamu | |
| Ubora Wa Swaum | |
| Dalili Juu Ya Uwajibu Wa Swaum | |
| Swaum Ni Wajibu Kwa Mtu Gani? | |
| Kuonekana Kwa Mwezi Ramadhan Na Hukumu Zake | |
| Nyudhuru Zinazo Mfanya Mtu Ale Mchana Wa Ramadhan | |
| 1. Safari: | |

| | |
|---|---|
| 2. Ni Mtu Asiyeweza Kufunga Katika Maisha Yake: | |
| 3. Mgonjwa Anaetarajia Kupona: | |
| 4. Mwenye Hedhi Na Nifasi: | |
| 5. Mjamzito Na Mwenye Kunyonyesha: | |
| Mambo Yanayo Haribu Swaum | |
| Adabu Za Swaum | |
| Adabu Za Wajibu Katika Swaum | |
| Mambo Yanayo Pendeza Kwa Mtu Aliyefunga: | |
| Swala Ya Tarawehe | |
| Swaum Ya Sunna | |
| Athari Zinazo Patikana Kwa Kufunga Sunna | |
| Somo La Saba: Hijja | |
| Hijja | |
| Maana Ya Hijja: | |
| Dalili Za Kufaradhishwa Kwa Hijja | |
| Fadhila Za Hijja | |
| Malengo Ya Hijja | |

| | |
|---|---|
| Sharti Za Hijja | |
| Mipaka Ya Hijja | |
| Baadhi Ya Mambo Muhimu Kuhusu Mipaka Ya Hijja | |
| Ibada Ya Hijja Na Nguzo Zake | |
| 1- Kuhirimia | |
| Aina Za Kuhirimia: Kuhirimia kupo aina tatu: | |
| Mambo Ya Wajibu Kwa Mwenye Kuhirimia | |
| Sunna Za Ihram | |
| Mambo Yasiyofaa Kwa Mwenye Kuhirimia | |
| Al Talbiyah | |
| Maana Ya Talbiyah: | |
| Hukumu ya maneno hayo: | |
| 2- Kufanya Twawaafu | |
| Maana Yake: | |
| Hukumu Ya Twawaafu: | |
| Sharti Za Kutufu | |
| Sunna Za Twawaafu: | |

| | |
|---|---|
| 3- Kufanya Saayi Baina Ya Swafaa Na Mar'wa | |
| Hukumu Yake: | |
| Sharti Za Kufanya Saayi: | |
| 4- Kusimama Katika Viwanja Vya Arafah | |
| Hukumu yake: | |
| Hukumu Ya Mtu Aliyepitwa Na Kisimamo Cha Arafah | |
| Baadhi Ya Mambo Yanayo Ambatana Na Kisimamo Cha Arafah | |
| 5- Kulala Muzdalifah | |
| Hukumu Yake: | |
| Hukumu Ya Mwenye Kuacha Kulala Muzdalifah | |
| 6- Kurusha Mwe | |
| Hukumu Yake: | |
| Muda Wa Kurusha Mawe | |
| Sharti Za Kurusha Mawe | |
| Hukumu Ya Kumuwakilisha Mtu Kurusha Mawe | |
| Kunyoa Nywele Au Kupunguza | |
| Hukumu yake: | |

| | |
|---|---|
| Muda Wa Kunyoa Nywele | |
| Baadhi Ya Mambo Muhimu Katika Kunyoa Nywele Au Kupunguza | |
| 8- Kuchinja Mnyama | |
| Maana ya kuchinja mnyama: | |
| Vigawanyo Vya Wanyama | |
| (a) Ni mnyama anayechinjwa kwa ajili ya kumshukuru Allah: | |
| (b) Ni mnyama wa lazima: | |
| Na tofauti iliyopo katika kuchinja kwa kumshukuru Allah, na kuchinja kwa ajili ya kuziba mapungufu: | |
| Sharti Zinazo Paswa Kukamilika Kwa Mnyama Anaechinjwa | |
| 9- Kula Mina | |
| Hukumu ya kulala Mina: | |
| Watu Ambao Siyo Wajibu Kwao Kulala Mina | |
| Makusudio ya kulala Mina: | |
| Makaosa Wanayofanya Baadhi Ya Mahujaji | |
| Umrah Na Hukumu Zake | |
| Maana Ya Umrah: | |

| | |
|---|---|
| Hukumu Ya Umrah | |
| Sifa Za Umrah | |
| Nguzo Za Umrah | |
| Mambo Ya Wajibu Kati Umra | |
| Yaliomo | |
| | |